# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report Of

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GANZE CONSTITUENCY, HELD AT GODOMA SECONDARY SCHOOL

ON

Friday, 3rd May 2002

**VERBATIM REPORT OF CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GODOMA CONSTITUENCY, HELD AT GODOMA SECONDARY SCHOOL ON 3-05-2002**

**Present**

Prof. Yash Pal Ghai - Chairperson
Mr. Abubakar Zein Abubakar - Commissioner

**Secretariat staff in Attendance**

Mr. Naholi - Programme Officer
Josephine Ndung'u - Verbatim Recorder

Meeting was called to order at 10.00a.m with Com. Zein in the chair.

**District Coordinator:** Jambo la kwanza ningependa kumuomba mshirikishi wa tume ya kurekebisha Katiba, Daniel, atuongoze kwa kumuomba mmoja wetu atuongoze kwa maombi. Asante.

**Daniel Baya:** Asante sana. Ningemuomba dada Esther pale atuongoze kwa maombi.

**Bi. Esther:** Natuombe. Baba wa Mbinguni tunakushukuru asubuhi ya leo kwa kuwa (inaudible)

**District Coordinator:** Asante sana Esther. Ningependa kuchukua fursa hii kwa kumupatia Headmaster wa hapa, Bwana Hanjari dakika moja sasa hivi ili aweze kutukaribisha rasmi katika shule hii. Asante.

**Wilson Hanjari(Headmaster):** Mwenye kiti wa tume hii ambaye ni Professor Ghai, Commissioners walioko pamoja naye, Coordinator wetu wa District, wageni walioandamana na Chairman, mabibi na mabwana. Langu ni fupi, kwanza ni kuwakaribisha katika Godoma Secondary School. Mjisikie muko huru. La pili, ni kuwa kufika upande wa kujisaidia, upande huu, tumetenga ni wa akina mama, upande huu, tumetenga ni kwa akina baba. Kwa hivyo kama ukitatizika, tuko na wazaidizi hapa kwa hivyo utaweza kusaidiwa. Kwa wakati huu, nachukua fursa hii kumwalika Coordinator wetu wa district.

**District Coordinator:** (inaudible) Ijapo umeingia na hujajiandikisha pale nje, tafadhali tikianza kikao, toka kuna meza pale tuandikishe kila mtu, uwe na maoni huna maoni, tafadhali tuna registration desk pale nje, uje upate kujiandikisha wale walioingia, kitambo tungekuwa tumeanza. Commissioner Zein, tafadhali tujurishe tuko na nani. Lakini kabla hapo, niko na CCs Members ambao walikuwa wanatakikana wawe hapa lakini so far tuko na mmoja tu pale. Bwana Kitao ambaye anatoka sehemu ya Bamba. Ni mmoja wa wale kamati. He is one of the committee members, he comes from around here. The others are yet to come. They come from other areas. Asante sana. Commissioner Zein.

**Com. Abubakar Zein:** Sasa naweza kuwaamkua rasmi. Habari ya asubuhi. Tume ya kurekebisha Katiba kama mnavyojua inakusanya maoni ya wakenya ili kurekebisha Katiba yetu. Sasa ukiwa kama anavyosema huyu mshirikishi wetu Daniel, ukishaingia pale kuna mahali pa kunjiandikisha. Ukishajiandikisha kwenye form kama hii ikijaa, tunaletewa sisi. Sisi tutatumia majina ilivyoandikwa, kufuata orodha hiyo kuwaita watu ili waweza kutoa maoni yao. Ukishaitwa, tuna microphone ambazo ziko hapa, mtu utapewa. Daniel? Akija mtu kutoa maoni anakaa wapi?

**Daniel Baya :** Pale.

**Com. Abubakar Zein:** Mtu utakuja kutoa maoni yako uwe pale. Ukiitwa jina lako uje kutoa maoni, kuna njia kadhaa za kutoa maoni. Njia ya kwanza ni kuwa uwe umeandika maoni yako katika maandishi. Na ukiwa umeandika maoni yako katika maandishi, unaweza kutupa maandishi hayo bila kuongezea au ukitaka kuzungumzia maandishi hayo, tutakupa dakika tano, ili ugusie yale mambo muhimu uliyo yaandika katika maandishi yako. Hiyo ni njia ya kwanza.

Njia ya pili, unaweza kutoa maoni yako bila maandishi, ukaja ukatoa maoni yako kwa mazungumzo peke yake. Na ukiwa utazungumza kwa mazungumzo peke yake, utapewa fursa ya dakika kumi. Halafu ukimaliza kutoa maoni yako, Professor Ghai au mimi tunaweza kuwauliza maswali. Sawa? Sijui kama tumeelewana mpaka hapo? Halafu ukimaliza kutoa maoni yako, kuna Binti pale, anaregister, utatakiwa uandike jina lako pale, na ujiandikishe. Baada ya kutoa maoni sasa. Ukishamaliza kutoa maoni, unaandika kwenye register pale unatia sign yako.

Lingine muhimu la sisi kufahamu ni kwamba, unaweza kutoa maoni yako kwa lugha ya Kiswahili, unaweza kutoa maoni yako kwa lugha ya Kiingereza, unaweza kutoa maoni yako kwa lugha ingine yoyote ya Kenya. Ikiwa unataka kutoa maoni yako kwa Kigiriama, unaruhusiwa kufanya hivyo, na tuna yule Binti yuko pale atatafsiri.

Jambo lingine muhimu kufahamu ni kwamba sisi tunakusanya maoni haya na kuyarekodi. Haya maoni tunayarekodi, ili tusipoteze hata neno moja. Professor Ghai na mimi, tutakuwa tukiandika hayo maoni. Lakini maoni tunayarekodi kwa tape recorder, na huyu bwana mnamuona anarekodi kwa video ndiyo neno hata moja lisipotee. Yeye atarekodi sehemu tu lakini yale ya kurekodi kwa tape recorder yataendelea mpaka yatakapomalizika. Tunaanza kazi sasa, mpaka saa kumi na mbili jioni. Ikifika saa kumi na mbili jioni, ikiwa kuna wananchi ambao hawajatoa maoni yao, tutakaa mpaka tutakapo maliza kusikiza maoni yao. Sijui kama tunaelewana?

Lingine la muhimu kufahamu ukishatoa maoni yako ukiwa unakata kwenda zako kushughulikia mambo mengine muhimu katika maisha yetu kama Wakenya una ruhusa ya kufanya hivyo.

Lingine la muhimu, ukiwa unaona jina lako liko mbali unaweza kumwambia huyu Bwana na umuombe ruhusa uende ukirudi hata kama jina lako limepitwa, tutakurudishia. Sijui kama tuko pamoja. Lakini juu ya huu utaratibu nilio waambia, tungewaomba radhi tuubadilishe kidogo ikiwa mahitaji yanatulazimu tufanye hivyo. Na nitawapa baadhi ya sababu ambayo inaweza kutufanya sisi mutupe ruhusa tubandirishe mfumo huo au utaratibu huo. Akaja mama mmoja wetu ambaye pengine ni mja mzito. Tutawaomba ruhusa tumpe fursa ya mbele, tusimfanye achelewe sana. Sijui kama mmetupa ruhusa hiyo. Akaja mtu mzee sana hawezi kustaamini kukaa chini na kungojea sana. Sijui kama mtatupa ruhusa tumpe fursa pia yeye. Sawa. Au akaja mtu mgonjwa. Pia anahitaji kupewa fursa ya mbele, au hafai kupewa fursa ya mbele? Sawa sawa. Kufika hapo kuna mtu yeyote mwenye swali lolote. Ndiyo ndugu.

**Swali:** Nasema hivi, ikiwa mtu pengine maoni yake ni mengi zaidi, na anataka kuyazungumza yote ili aweze kumaliza yote yale yalio katika kigutugutu kilicho ndani ya moyo wake basi pia apewe ruhusa hiyo, ili aweze kuyamaliza, na nyinyi mchukue maoni yake yote kwa ukamilifu. Kama ulivyo tangulia kusema uko tayari hata kuongeza masaa. Ili kila mmoja atosheke kwa shughuli hii. Asanteni.

**Com. Abubaka Zein:** Asante Mzee wangu. Hayo unayosema mzee wangu. Sisi huwa tunafanya. Huu ni utaratibu tunaouweka, ili kutupa muongozo. Lakini ikiwa hujakamilisha mambo yako ikifika dakika kumu zimeisha, kitu utakachoambiwa, Mzee sasa fanya haraka na uyafupishe. Lakini utapewa fursa hiyo kumaliza maneno yako. Ndio ndugu.

**Swali:** Swali langu la husiana na huu muongozo. Nadhani ni kama muongozo. Sasa katika huu muongozo kuna vipengele vingi hapa dani. Natumai zi lazima mtu aongee kuhusu kila kipengele dani ya huu muongozo. Labda atachukua kama mambo matatu

hivi. Kwa mfano labda atachagua hapa structures and systems of Government. Halafu basic rights, halafu Land and property rights. Nikaongea kuhusu mambo haya peke yake. Iko ruhusa ya kufanya jambo kama lile. Asante sana.

**Com. Abubakar Zein:** Tukasema huo ni muongozo ndugu yangu. Unaweza hata uuweka kando, hutaki kusema yaliomo humu. Useme yali muoyoni mwaka kama alivyosema huyu mzee. Pia unaruhusa hiyo. Umepewa muongozo huu, ili ukuongoze. Kwanini? Nivizuri kuzungumzia shinda zetu. Lakini ni bora zaidi ikiwa utazungumzia shida na useme mapendekezo yangu ni haya ili kuyatatua. Sijui kama tunaelewana. Sawa?

**Swali:** Swali langu nikusema, mtu akishakuwa ameandika karatasini tunasema akienda akitoa pale itakuwa ni basi? Mtu akiandika yale mapendekezo yake na akienda akitoa kwa wale, atakuwa amemaliza, ama ni vipi?

**Com. Abubukar Zein:** Nimesema, ukiwa umeandika maandishi unaweza kuyatoa bila kuzungumza, na ukiwa wataka kuzungumzia, kuwaeleza wenzetu yale umezungumza katika maandishi yako, utapewa dakika tano utaje yalio muhimu.

**Swali:** Mimi swali langu linahusiana na yale mapendekezo ambayo tunaenda kutoa. Pengine naenda kutoa pendekezo ama oni ambalo linagusia mtu ama watu. Nasema pengine naweza kutoa pendekezo ama maoni yangu na nikawa pengine kwa kusema sema itabidi nitoe mfano wa kugusia mtu. Je na hakikishiwa kwamba ya hapa yataishia hapa ama kuna hali ya kwamba nikigusia mtu, pengine nikitoka hapa inaweza kuwa nianze kuulizwa maswali?

**Com. Abubakar Zein:** Nafikiri hili ni swali nzuri, na swali hili, lina majimbu mawili. Jibu la kwanza ni kwamba, kwa mujimbu ya sheria ilioyounda sheria ya tume hii, ya kurekebisha Katiba, inasema wazi, hakuna mtu yeyote atakaechukuliwa hatua yeyote, kwa maneno anayoyasema katika mkutano wetu au asioyasema. Kwa nini, kwamba ukiyasema yakimuudhi mtu, shauri yake, au huelewi hivyo? Ikiwa kuna mwingine amekwambia lazima ukasema mambo fulani, uje hapa usiyaseme, pia hiyo haitakuwa hatia kwako. Na ikiwa kuna mtu yeyote atatishwa, ni vizuri atupe taarifa haraka. Maanake sheria inasema ni hatia kumutisha au kumwambia mtu asingesema hivi au lile. Lakini juu ya kusema hayo, na mimi mi mpwani mwenzenu, mimi natoka Mombasa. Kwetu Mombasa wasema je? Ukitaka kuzungumza na watu hata kama magumu tumia lugha laini. Au siyo hivyo? Ukitaka kuzungumza na wazee tumia lugha muruwa, au siyo hivyo? Kwa hivyo tutumie lugha ambayo tunaweza kusema mbele ya wakina mama, mbele ya wazee, bila matusi. Sijui kama wanifahamu. Asante sana. Sasa ningetaka kuwajulisha kwa watu ambao wako hapa. Nia anze kwa mkono wangu wa kushoto, kwa kumuomba Chairman awasalimie.

**Prof. Yash Pal Ghai:** Hamjambo

**Response:** Hatujambo

**Prof. Yash Pal Ghai:** Mambo ya Katiba ni magumu kusema kwa Kiswahili. So I will have to speak in English when it comes to matters of the Constitution. The purpose of our meeting here is not to talk to you about the process or about the Constitution

changes, the purpose of our visit is to receive your views and my colleague Commissioner Zein has explained the procedure that you shall follow but I should like to add that after if this meeting you still have other views that you want to give us, you can write those views and give to the District Coordinator and we shall receive and consider them. So I want to say how glad I am to see you here and I look forward to hearing your views on the Constitution changes. Karibu sana. (clapping)

**Com. Abubakar Zein:** Ningependa kumuomba Bwana Naholi awasalimie na awajulishe kwenu kwa wale vijana wanaofanya kazi.

**Bw.Naholi:** Asante sana Professor Ghai, Commissioner Zein, District Coordinator wetu hapa Kilifi, wazee, akina mama na vijana. Hamjambo? Hamjambo tena?

**Response:** Hatujambo:

**Bw. Naholi:** Yangu ni kusema asante sana kwa kufika na vile Commissioners wamesema ni kuchukua maoni yenu. Hapa nimekuja na Staff kutoka huko Office zetu kuu Nairobi. Niko na Josephine pale.

**Bi. Josephine:** Hamjambo?

**Bw. Naholi:** Na kwa majina mimi naitwa George Naholi. Asante sana. Kuna anayetusaidia hapa na ni mtoto wa kwenu hapa. District Coordinator au Headmaster anaweza kusema jina. Esther. Kwa hivyo tuko hivyo. Na wengine mtawajua. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Naholi. Ningependa pia kumtambulisha kwenu. Sio kwamba hamumjui, nadhani mwamjua vizuri, lakini ni kumpa hadhi yake tu kwa kumtaja kwamba Bwana DO yuko hapa na sisi. Kama unaweza kuwasalimia.

**District Officer:** Bando na mkaribisha Bwana Chairman na kamati yake na waambia mjisikie kwamba mko Bamba. Watu wa Bamba nawasalimia, hamjambo?

**Response:** Hatujambo

**District Officer:** Toeni maoni yenu bila uoga ili wale walikuja hapa wapate kile walikuja kuchukua. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana DO. Ningependa kusema pia, Mheshimiwa Waziri tulikuwa tumezungumza naye jana, na leo asubuhi, na yuko jiani, atakuja kwenye kikao hiki. Sasa ningependa kumuita, mtu atakaye zungumza kwanza. Na

mtu amutayarishie microphone pale. Bi Kadzo Wa Charo. Kama hayuko karibu, Kadzo Kaingu. Asante mama. Karibu utoe maoni yako. Uende pale mama utapewa microphone uzungumze. Ungemupa microphone hapa azungumzie hapa karibu.

**Kadzo Kaingu:** *Nahenza ahoho mashome, sina pesa zakumupa hata makale mandashoma, hata mbereni vidzashinda.*

**Bi. Esther**: Well she saying that she is recommending free education because she want her children to go to school but she does not have the money for that education. So she needs free education.

**Kadzo Kaingu:** *Hata ko mbereni undakala hudzashindwa, kafuna pesa.*

**Bi. Esther:** She is just trying to emphasize the fact that she needs that special education because if we are to continue paying for the children then she will have no alternative but not to educate her children.

**Kadzo Kaingu:** *Hudzaremezwa hundakala hunaenza kushoma, sina pesa vidzashinda.*

**Bi. Esther:** Okey, she does not have any more. It is just that part of free education.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mama. Uende pale u sign. Uandike jina pale Mama. Tafadhali. Namuomba Kavumbi Walandu. Nafasi tunamupa Kavumbi Walandu. Asante Mama. Karibu pale.

**Kavumbi Randu:** *Haya hudzire mimi Kavumbi wa Randu tabu ni noni?Ni ahoho wanaehenza kushoma, ende sikuli. Kwehu kuna shida bomu hata kaiyadimikika kamare. Ache manakusuka nyere kwa dzua na madzi ahoho manahenza mashomw zhomu menderere na maenderero , machero ni kudza naswi hukadza kala hadzo.*

**Bi. Esther:** She saying that there is a general problem in this area in that the children want to school and they want to progress but the problem is that there is no water in this place. So the main problem is that there is no water. So they are hoping for a better future if there will be water.

**Kavumbi Randu:** *Sikuli ni chafu hata kayadimikika kwa habari ya tabu ya kwehu. Hata ye muhoho kukicha anamala madzi adzimwagire akala andakwenda sikuli, madzi be ni mutsana wa dzua ndo upate madzi ga kumpa mwana.*

**Bi. Esther:** She is trying to emphasize the fact that, that water is so important because that child need to go to school, there is no water to bathe. When she comes back, there is no water to drink and all that. So her main problem or the main problem is water.

**Kavumbi Randu:** *Hunaehenza sna mufuunge mukono , mufusaidie ario ahoho ehu nao maenderere na maenderero madzo machero ni kudza hukambola hatu dza vivi hahe.*

**Bi. Esther:** She is saying that she asking for your assistance that you help them to solve that problem so that in the future there will be a better community.

**Kavumbi Randu:** *Muhoho ni kalamu, pesa nazo kazioneka kamare hata za kugula go mabuku ni tabu. Wario ahoho mufusaidie, mufunge mukono, hali ya ahoho ehu nao mandambola hadzo.*

**Bi. Esther:** She is saying that she needs the assistance also because there is no money to buy the books. They do not have money to buy the pens for the children to keep on going to school. So they still need your assistance for that.

**Kavumbi Randu:** *Go mangine kwa jumula …………….( inaudible))*

**Bi. Esther:** Okey, she doesn't have any more. That's all.

**Com. Abubakar Zein:** Could you thank her for me. Mwambie asante kwa kinyumbani. Asante sana mama. Mama ngoja mama. Subiri kidogo. Mwambie asubiri kidogo. Mama jina lako kwanza.

Nasemaje ndugu zangu, naona tumeongezeka. Nilisema kwamba mimi nitatumia orodha ya majina haya niliyopata, nikiita mtu jina, ndio aje atoe maoni yake.

**Bi. Esther:** *Munaambwa ni mayo iha, andaiha madzina vira mudzodziandika madzina haratu. Sasa usagale mpaka dzinaro richihiwa haratu udze haha , udze unene . Usidze haha kabla kudzahihiwa.*

**Speaker:** ***Sawa ? Ni karakara enh ? Hapa pana mama ambaye ataanza kutoa maoni yake.***

**Kadzo Charo:** ***Mimi ndimi Kadzo wa Charo.***

**Bi. Esther:** Her name is Kadzo Charo.

**Kadzo Charo:** *Kwehu kuna tabu , sipitali muhaka pesa mino sina, nahenza ikale ya bule.*

**Bi. Esther:** She is saying, the main problem here is that there are no hospitals around and then again you can't go there without money. She want that to be scrapped off. She want the hospital bill to be scrapped off so that it will be free services at the

hospital. That is what she wants.

**KadzoCharo:** *Kungine urathi wehu nahenza ukale barabara ,husaidie kwa vivi. Kare hudzire na magulu kwasababu kahuna pesa za kudzirira.*

**Bi. Esther:** The other problem is the roads. Transport is a problem. Right now she has walked a long distance because she doesn't have the money and then the roads are also in bad condition. She doesn't have any more. That is all she has to present.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana mama. Joseph Kazungu? Fursa hii anapewa Joseph Kazungu. Joseph Kazungu yuko? Hayuko. Nitamuacha Joseph Kazungu. Furaha Katana. Huyo ndio Furaha Katana, anakuja kutoa maoni yake.

**Furaha Katana:** Ningetaka kutoa pongezi kwa waakilishi wote waliofika hapa Katiba, mabibi na mabwana. Nia yangu nikuona Katiba hii ibandirishwe. Kwanini? Tunasitikika sana kwa kugandamizwa kwa kila aina ya jambo tunalofanya. Mambo ambayo haza yanayotugandamiza huku kwetu ni uongozi. Tunaviongozi ambao mara nyingi tunawachagua lakini katika matakwa yetu hawatutimizii. Tuanaviongozi ambao wanatushirikisha katika viti vya wanachama. Na tiukiangalia msimamo wa hao viongozi wanaotuwakilisha na kutuunganisha katika vyama, matamshi yao ni matamu, tukiangalia vitendo. Kwa hivyo, tungeomba Katiba hii iwe na muwelekeo kwa kila raia ambaye anaishi katika Kenya hii.

Pili, tunahitaji tuwe na kiongozi ambaye atakuwa ni Mpwani, hayo ni kuambatana na majimbo. Tuwe kila kilio tutakacho kuwa nacho kina sikizwa na tunatimiziwa miradi yetu.

Tatu, tungeomba viongozi wote hasa hawa walinzi, policemen, wawe wakiwa na viwango vya adhabu ambavyo huwa wanapewa bali na kunyemelea upande wa rushwa. Hayo mambo hayo ya ufisadi, ningeomba katika Katiba hii mpya tusione mnyanyasano wowote. Kila mwana raia awe anafurahia ule ushauri atakuwa ameutoa.

La nne, tungeomba matakwa ya Rais, usimamizi wa Rais, usiwe mikononi mwake bali uwe kwa Wabunge. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Furaha Katana. Mr Hajali? Bwana headmaster

**Wilson Hanjari (Headmaster):** My names are Mr. Wilson C. Hanjari and the first thing that I have to express upon are different appointments. The first one is the Presidential. It is my feeling that through the different posts that he is supposed to be holding during his term in office, for example being the Commander in Chief, Chancellor to the Universities, Chairman of the ruling party and etc. Some of these posts should be relinquished so that at least he is given enough time to look at the affairs of the citizens.

On nominated MPs and Councillors, it is a feeling that this one should be done away with given that if at all there was need to increase the number of MPs and Councillors then more wards and what we call Constituencies should be established otherwise it does not serve any purpose to have many nominated Councillors and MPs as possible . Then when it comes to the Ministrial appointments especially, I am quoting that because of the problem of each of the sitting MPs undergoing a lot of problems so as to acquire a seat and given that these seats are not given on a plate, then each of the parties that gets a sitting MP into the Parliament, should be given at least some Ministers and it should not simply be a one party affair. And then on the appointment of Ministers, a guideline should be there to determine the level of education of the Minister or any other person to be appointed to such positions.

Another point that I have to put across here is the idea of devil worshiping. Of late we have been having several cases for example increase in accidents, fires in school and so on. And the probability of these things increasing is more and these people sometimes we know, sometimes we just guess but I just propose that if it is possible when these people are identified they should be taken to court and given harsh sentences.

Then on judiciary and the treatment we are getting from some lawyers, there has been an increasing rate of what we call conmanship, where one is to be refunded some money but the lawyer takes it. These complaints have been on. What we know is that the law society of Kenya has been doing something to that extent, for example de-registration of the firm and so on. However these foundations are not still harsh. They should be given more harsher conditions for example de-registering and these people taken to court immediately so that they are jailed.

Then on police arrests we are talking of what we call warrant arrest. This has been neglected for so long to the extent that if for example there is a problem you are simply arrested without that warrant and any effort to ask more questions gives you more problems. So we are just requesting that if it is possible, these warrants be enforced so that even when you are taken to court the judge should ensure that such documents are available and any errant police to be sacked accordingly.

On the security for headteachers, we talk of recently increased insecurity especially in boarding schools and we are talking of sometimes thugs entering into schools. Sometimes students molest and kill the headteachers. Now the Government is supposed to interven in the following ways:

1. The headteachers be allowed to buy guns at a reasonable price and use them and the conditions for acquiring permits should be fair.
2. The Government should come up with a clear policy on the security of headteachers or amend the Education Act so as to incorporate an insurance policy that will compensate the bereaved family. Thank you.

**Com. Abubakar Zein:** Thank you Bwana Hanjari. Anayefuatwa ni Reverend Kasiwa. Endelea Mzee.

**Rev. Albert Kasiwa:** Mimi maoni yangu ni kusema tungependelea serikali yetu iwe inatambua maskini na yule mwenye uwezo sawa sawa. Maana

**Com. Abubakar Zein:** Asante Mzee. Taja jina lako ndio tuli-rekodi. Tunarecord majina. Sema tu jina lako nani.

**Rev. Albert Kasiwa:** Pole. Mimi jina langu naitwa Rev. Albert Kasiwa. Nasema hivi tungependelea ama kuonelea serikali yetu ingekuwa inatambua maskini na yule mwenye uwezo sawa sawa. Kwa hivi sasa inavyo onekana ni kama maskini ndiye mwenye shida kubwa zaidi katika watu wetu wanaokaa Kenya. Anavyo hudumiwa yule mwenye uwezo kuna tofauti kubwa sana na yule ambaye ni maskini. Popote. Kwa hivyo kama angehudumiwa yule maskini kama vile anavyohudumiwa yule mwenye nguvu, hapo inaonekana kungekuwa na Kenya moja na mambo mazuri ambayo yangekuwa yanawafaidi wote badala ya kufaidika wale wenye nguvu na wale maskini hawana la kufanya. Tukiendelea kusema kwa uchache ni kusema maskini wowote anapoingia, anapotafuta usaidizi nini, anavyo hudumiwa, sivyo anavyohudumiwa yule mwenye uwezo. Na hili limekuwa jambo ambalo linawafunja moyo sana wale maskini katika Kenya. Kumekuwa ni kama kwenye huru wa watu wenye nguvu na maskini. Ambavyo hilo limekuwa tatizo na tutaona kama ni tatizo kubwa sio ndogo. Kama likitambulika na kufanywa vizuri labda watu wetu katika Kenya watafaidika. Maskini atambulike kama vile anavyotambulika yule mwenye nguvu, popote. Nikitaja ni sehemu nyingi. Nafikiri watu wengi wanaona hivi hata kwa macho na nini. Kwa hivyo jambo kama hili, naona lingekuwa msaada kama likitekelezwa. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Rev. Kasiwa. Asante sana. Tafadhali andika jina lako kwenye register kwamba umetoa maoni. Asante. Hussein Mwatsahu.

**Hussein Mwatsahu:** My name is Hussein Mwatsahu. I would like to talk on actually three parts of the Constitution. The first is the Structure and Systems of Government; it is my feeling that the current structure and system of Government encourages a lot of nepotism. In the first Government, we saw the Kikuyus consolidating their hold on power and authority of this country in the sense that we had almost entire Government made of Kikuyus. Judiciary, the Legislature, the Cabinet, a large part of Cabinet was made up of Kikuyus and administration, Provincial Commissioners, District Commissioners, Division Officers and I feel that this only happened because the kind of system we had at that time or that we still have today encouraged and also made it easy for that kind of situation to occur. Again, after when Moi took over, there was a general purge of Kikuyus and they were replaced this time by the Kalenjins who have today I think 65% of senior positions in Government, parastatals, and this has always been able to prevail because of the current structure and system of Government. So we do not know, if we still retain this structure when Moi goes, we might now get another one now a Luhya like say Honourable Mudavadi and then the system will change. We shall have again Luhyas taking over all positions of Government and authority which leaves people like us in the Coast Province as subjects in our own country. We have no control of our resources. We have no control of our

basic rights, we have no control of our anything. So I would suggest that we have a system of Government that is sensitive to regional interest and needs and that is a Federal System of Government.

Secondly, on the basic rights of individuals which includes food, shelter and clothing. On the question of food, the Coast Province is fertile but from the colonial times, agriculture has always been used as a weapon. The growing of crops, permission to grow certain crops, like we had during the colonial times. Africans were not allowed to grow coffee and tea and pyrethrum and all those crops that would make them rich. Now, currently the system is, we are being told that everything can't grow in the Coast Province. But I think everything can grow here but the problem is, if we have a Government that is sensitive to the people then it will put in place the necessary infrastructure to make sure that we are self sufficient in the production of food. Actually every kind of crop can grow in the Coast Province if we have the right policies, the right ideas, the right people at the right places. We can grow and be self sufficient in food. Currently the situation is, we only grow food that is enough for a month or two because mostly the farming method is subsistence. There is no machinery, there is no ferterlizer, there are no inputs, yet we have several officers here Agricultural Officers, Extention Officers but when we do not have these tools, we cannot grow enough food. So first, the basic need of food is being ignored and we are being subjected to poverty which is actually man made poverty because there are remedies and there are ways and means of solving this problem.

Third, land and property rights; it is a shame, a very big shame and very saddening that today, thirty nine years after indipendence seventy per cent of us do not own land. That is legally we do not own it. Although we do own it in a way according to our clan systems. Land tenure systems are on clan basis but basically legally, we do not own this land. Such that if the Government has any project in this area the only thing it has to do is give us a notice of three months, one month they come with bulldozers, they pay us very little for our small houses. They grab that land and then they do whatever project they want to do. A very good example ,when they were building the barracks at Mariakani. I think it had lots of people there. They only paid for their houses but they did not pay for their land. They did not want to know where those people would go. So basically, we in the Coast Province apart from settlement schemes the rest of us don't have title deeds like in this area in Bamba division and Ganze division. The only people who have title deeds are the group ranchers. Otherwise the other peasants have no title deeds. Therefore, they have no legal ownership to land. So I feel that if we have a system of Government that is sensitive to our needs and aspiration the first and most important thing that they would do is to change this land tenure system, so that title deeds are mandatory and easily available to everyone of us so that also we can prosper, we can get loans to buy machinery, we can cultivate bigger shambas as long as there is security of land tenure. Thank you very much.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Hussein. Sasa tungemuomba Enock Kadza

**Enock Kadza:** Kwa jina naitwa Enock Kaza na yangu ambalo nitazungumzia itakuwa ni machache maanake kidogo nitaweza sema yamesemwa mengi tayari. Lakini nitaguzia kwa sababu imenibidi lazima nifike hapa nami nizungumze.

La kwanza ambalo ningetaka kuzungumzia ni kuhusu hali hii ya umasikini ambayo tumezungumzia katika taifa letu la Kenya.

Tunaonelea kwamba kama kungekua na njia nzuri ya Katiba ambayo itapangwa kwamba mwananchi wa Kenya hii atakuwa na uwezo wa kumiliki sehemu mmoja wapo ya ardhi, ambayo itaweza kumufanya yeye awe na stabakali ya title deed ingeweza kumsaidia kuondoa umaskini. Kwa mfano kama sisi katika eneo hili la mkoa huu wa pwani tunaona katika sehemu hii yetu hasa Bamba, sehemu yetu siko na mchanga mzuri ambapo tunaweza kukuza vyakula na kuondoa umasikini huu. Lakini tunajikuta kwamba hatuna uwezo wa kuendeleza kilimo hiki au kukuza nafaka tofauti tafauti kulingana na hali ya uwezo wetu ambao ni duni.Ikiwa pengine tungekuwa na title deeds tunaona kwamba tungekuwa tumeweza kupata mikopo ya kujiendeleza, kujinufaisha kama wengine ambao wanafanya shughuli kama hizi katika sehemu moja katika Kenya hii yetu. Kwa hivyo kuchangia hapo sehemu hiyo moja ya kipengele hicho cha kusema kwamba tunataka tuwe na uwezo wa kumiliki vipande vyetu vya ardhi na matitizo yetu mengi ya mashamba tunaona kuna kesi nyingi sana za kuhusiana na mambo ya mashamba kutokana na kutokuweko na hali ya kumiliki sehemu zetu za ardhi.

Vile, vile ningetaka kusema kuhusu upande wa elimu. Elimu kulingana na sehemu hii yetu ya mkoa wa Pwani tunakuta kwamba elimu yetu iko chini. Na kuwa chini kwake basi tunaona inachangia kulingana na hali ya mapato yetu ya kila siku. Hali ya mapato yetu ya kila siku, tunakuta kazi ambazo tunazo huku, nyingi sana tunategemea hali ya ufugaji na ukulima. Na katika hali hiyo ya ufugaji na ukulima ndio tunaona pale kile kipengele cha mwanzo ni kama ambacho kinaoana au kinafanana kulingana na vipengele kama vile ambavyo tumezungumzia hapo mwanzoni ya kwamba tukiwa na vyeti vya kumiliki ardhi tungeukwa tuna uwezo wa kupata title deed ambazo zinaweza tupate mikopo ya kuendeleza vilimo vyetu vya ufugaji na ukulima. Ambapo pengine watoto wetu, tungeweza kuuza mifugo yetu ikiwa na afya nzuri tupate pesa za kutosha za kuelimisha watoto wetu. Hayo ndiyo machache ningetaka niyazungumzie kwa sababu mengi nikama tayari yamezungumziwa singetaka kupoteza wakati. Nimesema asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Enock. Anayefuatia ni Lawrence B. Kirao. Karibu Mzee.

**Lawrence B. Kirao:** Mimi jina langu, ni Lawrence Benjamin Kirao. Maoni ambayo yako akilini mwangu na moyoni mwangu,ni kwamba tumekwisha pata uhuru wetu kwa muda wa miaka ambayo takriba haipungui arubaini. Lakini, tukiangalia hii Kenya yetu iko na majimbo kadha wa kadha. Na katika majimbo hayo tuseme huko Kikuyu tumepata uongozi, tukauona. Huko Nandi, uko mpaka sasa, unafuata nyayo. Sasa basi, mimi ningependa kusema hivi. Ikiwa yeyote serikali itakayo kuja sisi hatuna neno nayo. Lakini mkuu wa kila mkoa, awe anatoka sehemu ile ile ambayo yeye amezaliwa katika mkoa huo. Mkuu wa mkoa awe ni wakutoka mkoa huo huo,hivyohivyo kuteremka chini, DC pia awe ni mtu wa kutoka hapo hapo, DO pia. Tukifika kiwango cha Chief na Sub-chief, wao ni kama walivyo kawaida. Hakuna taabu. Lakini, nitafanya mengi kidogo hapo. Kitu ni kwamba wale waitwe na serikali, wapewe mtihani wachaguliwe wale wanaopasa kushilikia huo wadhifa wa uchief na usubchief. Halafu warudi huku, waje watafute kura kutuka kwa raia ili waende sambamba na raia bila kuonyesha wazee ama wakaazi wa sehemu wanao akilisha kalamu kwamba mimi nimeandikwa na Serikali, huwezi kunifanya chochote.

Pili, jambo la pili ni kwamba, hapa kwetu kuna matatizo mengi sana, sehemu yetu hii haina mimea ya kujitegemea kama vile

kahawa, majani chai na vinginevyo kadhalika. Lakini hapa, Mungu pia hakutuacha patupu. Alitupa zawadi zetu za miti ambayo inaweza kutuletea sisi mazao kama wenzetu. Lakini haiwi hivyo. Tukiangalia sisi tuna mikanju, korosho. Serikali ilisema itatunjengea mtambo wa korosho ,ukakanyangika mpaka sasa haufanyi kazi kisawa sawa. Hivyo tunapenda, ikiwa itakuwa yule mkuu ni mtu wa hapa bila shaka atufufua hayo ili watu wapate kulima kwa bidii mikanju, wazalishe korosho wapate manufaa. Kuna huu mti tuliotumaini kabisa. Huo mti ni mnazi. Poleni. Mnazi tunataka, tangu tulipopata uhuru bila shaka watu wa science wamekuwa wengi sana. Wafanye utafiti wa huu mnazi. Kutoka ule ukanja mpaka yale marivu yanaweza kutumika vipi. Hata na sisi tukapata pesa kama vile Kenya yetu inavyouza kawaha katika sehemu zile ambazo kahawa inamea. Kifungu hicho dani yake kina huu mnazi wenye tembo. Hii nafikiri inaweza kutafutiwa namna na watu wa science mpaka ikaweza kusafirishwa ng' ambo ili ituletee mazao na sisi. Na ikiwa haikuwa hivyo,ale ambao wanauza kidogo kidogo katika mitaa na vijiji Katiba hii ambayo sasa leo tunaitunga sisi watu wa Bamba, iwe wanapewa fursa ya kuwa hawatoki hapa wakifika pale wanashikwa. Ana kijerikan cha shilingi mia nne kichwani, hapa ashikiwe acha,jiwe shilingi elfu moja, faini hapo hapo bara- barani. Haya tunapenda Katiba hii iyakomeshe kwa sababu yanatuumiza.

Jambo jingine, ni hali ya ukulima. Hii nchi yetu hivi ilivyo ni ngumu sana. Na sisi kwa jumla kwa sababu ya kunyanyaswa na mambo mengi ambayo yanatufanya hatuwezi kujiendeleza sana, hatuwezi kununua vifaa vya kulimia. Sasa hii Katiba mpya ambayo inatungwa, kila location at least iwe na tractor moja ya kulimia watu watakodisha ili wajaribu. Mchanga sio mbaya hivyo, lakini hali ya kulima na kile kijembe cha mkono na hali ya kilimo mvua ya sasa ni hivyo, ndivyo sivyo? Ikiwa umechimbuliwa sawa sawa na tractor umekodisha zile acre hata kama ni acre mbili, utakuwa umelima utakuwa unaweza kujipatia chakula na angalau gunia mbili tatu ukauza kwa matumizi ya nyumbani. Nafikiria nina mengi lakini wakati nao na hali, nawapa nafasi wenzangu. Hii hall yote imejaa hapa ina maoni tofauti tofauti. Pengine hayo ninayosema mwenzangu anamulwa zaidi aje aseme na yachuliwe yaende mapka yafike huko tulioambiwa yatafika ili tuone majimbu yake, kwamba moja au mbili tatu imechukulilwa. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Lawrence Benjamin Kirao. Anayefuatia ni Martin Bongo.

**Martin Bongo:** Majina yangu ni Martin Bongo na nitatoa mapendekezo yangu haraka haraka maana ni mengi kidogo. Kwa maoni yangu Kikatiba ningeonelea Serikali ambayo itaundwa baada ya Katiba hii mpya iwe ya majimbo. Na kwa kila jimbo katika Serikali hiyo iongozwe na Governor. Katika Serikali ya majimbo kutakuwa na Serikali kuu na hiyo Serikali kuu iongozwe na Rais. Na Rais huyo wa hiyo Serikali kuu asiwe Amri Jeshi mkuu awe ni Rais tumemuchagua maana tukifanya uchaguzi hatuchagui majeshi tunachagua kiongozi wa nchi. Majeshi waachiwe wanajeshi waliofanya ujeshi ama walio train kwa mambo ya kjeshi,lakini Rais wetu asiwe amiri jeshi mkuu.

Katika hiyo pointi ya tatu kama nilivyo nakili, asiwe na uwezo wa moja kwa moja wa kuteua ma-judge, mwanasheria mkuu, wakuu wamakampuni na mashirika ya serikali. Huyu raisi wetu, asiwe na uwezo wa moja kwa moja maana akiwa na uwezo huo, unachangia sana ufisadi. Badala yake, kamati itakayo jumuisha watu wa kanisa, wafanyi biashara, na wanasiasa wote na

wapate majina ya watu pengine watakao pendekezwa na Bunge ili ichuje yale majina ya watu wale, kisha watawasilishwa kwa Rais halafu pale, ndio ikiangaliwa mienendo ya mtu ambaye amefanya kazi kwa mashirikia ya Serikali ama kwa sector ya kibinafsi mtu yule anaweza akawa anafaa kuongoza shirika ama kampuni ya Serikali. Lakini Rais akiwa na uwezo wa moja kwa joma mara nyingi tunaona ya kwamba wanaochaguliwa huwa wanakaindi au huwa wanahalifu uteuzi ule maana huwa ni mawazo ya mtu mmoja na mara nyingi mawazo ya mtu mmoja hayawi vizuri sana. Kwa hao wanakenya ambao tuko karibu watu millioni thelathini. Kikatiba kamati iweze kuhoji mtendaji kazi wa kwa Serikali kama pengine ameteuliwa, na tuona mwenendo wake si mzuri. Ile kamati iwe na uwezo wa kumuita yule mtu na kumuhoji. Na ikiwezekana hiyo kamati inaweza kupendekeza kwa huyo Rais kwamba huyu hafai, na akafukuzwa kazi. Mara tunaona wakati mwingi mtu pengine amewekwa ni mkurugenzi mkuu wa hali mashauri ya badari ya Kenya, anakorofisha pale, kisha anatolewa pale anapelekwa pengine. Sasa vile ni kama kueneza ule ugonjwa ameanzisha pale akapeleke pengine. Ndio maana utaona viwada vyetu vimefilisika vingi kwa watu ambao hawafai lakini kwa sababu ni uteuzi wa mtu mmoja hatuwezi kufanya kitu.

Wakati wa mambo ya dharura kama vile uchokozi wa taifa lingine. Mataifa jirani yanaweza kuleta shida basi Rais asiwe na uwezo wa moja kwa moja wa kutangaza pengine vita kwa nchi ile. Awe anaweza kuita baraza la mawaziri na wakuu wa kijeshi waweze kutakabadhi mambo vile yatakavyokuwa ndio hatua ichukuliwe.

Kikatiba, Rais asipitishe vipindi viwili viwili vya miaka mitano mitano. Hata kama ni mzuri na mna gani. Pengine katika ile miaka kumi, tutakuwa tumepata mwingine mzuri zaidi ambaye kushinda yeye tutamchangua. Kwa hivyo Kikatiba, Raisi awe na vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Kikatiba, baada ya kuisha ama kushindwa kwa jia ya kura, vile vipindi, ule muda wake wa vipindi viwili, miaka mitano mitano, kama atakuwa ameshida ameenda mpaka kipindi cha pili. Unajua sasa kipindi cha mbili pale, lazima aachie mtu. Sasa yule ambaye atachaguliwa, kuna kile kipindi cha mpito ambacho nichakupokezana madaraka. Napendekeza katika Katiba mpya ile iwe ni siku sitini, sixty days ambazo yule Rais mpya tuliye mchagua, atakuwa amejitayarisha kuchagua mawaziri wake, baraza la mawaziri halafu siku sitini sikiisha basi rais yule aweze kupeana madaraka.

Kikatiba, kila sub-location kwa upande wa afya kuwe na vituo kama viwili, vya matibabu. Maana kumekuwa na shida sana. Kwa mfano huku kwetu kituo cha afya ama kihospitali tulichonacho ni hapa Bamba. Sasa ukiangalia mtu anayetoka Ndingiria wale wanaokujua, ukitembea kule hata ukifika hapa huo ugonjwa umeongezeka. Msaada unakuwa ni vigumu sana kuupata maana vituo vya afya viko mbali mbali. Kwa hivyo Kikatiba, kuwe kama vituo viwili vya afya kwa kila sub-location.

Kikatiba makundi haya ya watu, gharama zao ya matibabu zigharamiwe na Serikali. Tukisema ziwe za bure ni urongo. Maana hakuna kitu cha bure. Zigharamiwe na Serikali. Watu wakati ya mwaka mmoja hadi miaka kumi na minane. Kundi la pili, watu wa miaka hamsini na zaidi wale wazee vikongwe, Ambao hawawezi kufanya kazi tena. Serikali labda ingekuwa gharama kuwagharamia upande wa matibabu watu wale maana hawawezi kufanya kazi tena. Na sisi Waafrika tunajua kuwa

dependence ratio huwa inasumbua sana. Wale working class wanabebeshwa mizigo mizito sana. Serikali ingesaidia wale working class ndio wawe more productive kusaidia kwa njia hiyo.

Kikatiba, kila location iwe na kutuo cha polisi. Kila location. Maana usalama kwetu sisi ni muhimu sana. Sasa kila location ikiwa na kituo cha polisi kutakuwa hakuna shida sana ya kwamba watu wamevamiwa huko Mapotea mpaka Bamba ndio wapate msaada wa askari. Kama kuwe location ile kuna kituo cha polisi, inakuwa ni rahisi sana kupata usaidizi. Kikatiba Sub-chiefs, na ma-chief, wawe watu ambao angalau wamehitimu kidato cha nne. Maana tumeona kama huku kwetu ma-subchief wengi ni wa shule ya msingi wameishia pale. Sasa maongozi yanakuwa magumu maana sasa mtu ambaye elimu yake iko chini zaidi inakuwa ni vigumu wakati mwingine. Kwa hivyo, Kikatiba iwe sheria inaonyesha wazi kabisa ya kwamba mtu kuwa subchief kuchaguliwa ama kuajiriwa, awe angalau amefika kidato cha nne.

Kikatiba, kuwe na utaratibu ya hawa ma-chief kupandishwa vyeo. Mimi kwa maoni yangu ninaona itakuwa ni vizuri kama chief atapandishwa cheo na awe DO. Maana yule chief sasa anajua mambo ya huku. Lakini DO ambaye ametoka shule moja kwa moja amesomea bure mambo ya uongozi akiletwa kama huku kwetu itakuwa ni vigumu, maana taratibu za huku, mila za huku hazijui sasa inakuwa ni vigumu. Lakini sasa hawa ma-subchief ama chief wakibandishwa cheo, afike chief, apandishwe cheo, afike DC, mambo ya huku anayajua. Wakuu wa mashirika, wawe wenyeji na jimbo hilo.

Vyama vya kisiasa, viwe vitatu. Tunaona vyama vingi huwa na visuko suko na shida. Lakini kama Katiba itakuwa inaruhusu vyama vitatu nafikiri vyama vitatu ama hata vinne si vimbaya.

Kikatiba, Rais awe mtu ambaye atapata zaidi ya asilimia hamsini ya kula zote zitazopigwa. Kula zote za nchi awe anapata zaidi ya asilimia hamsini ndio achaguliwe kuwa ni rais.

Kikatiba, uchaguzi uwe wa daraja tatu. Maana tumeona wakati mwingi watu wanachukuwa advantage kwa kuwa uchaguzi wa madiwani wa wabunge na wa urais unafanywa pamoja sasa inakuwa ni vigumu sana huku kwetu hasa sehemu za mashambani watu wanakuwa exploited hawawezi kufanya uamuzi vizuri sana. Lakini tukianza kwa mfano uchaguzi wa madiwani, tuje uchaguzi wa Wabunge halafu uchaguzi wa urais itakuwa ni vizuri zaidi.

Kikatiba, judge mkuu na ma askofu kumi na wawili wahusike na shughuli hiyo ya kuapishwa kwa Rais mteule. Rais ambaye atakuwa amechaguliwa, judge mkuu na maaskofu kumi na wawili, washughulike na hiyo shughuli ya kumuapisha.

Kikatiba, mipaka ya jadi ya mashamba itambuliwe. Mipaka ya jadi ya mashamba. Traditional boundaries. Unajua kama huku kwetu, kuna Mapotea ranch, kuna Giriama ranch. Lakini katikati ya hizo ranches kuna mipaka watu wanaishi sasa ile mipaka itambuliwe.

Kikatiba, kuwe na uhuru wa kuwabudu lakini usajili wa mashirika ya kidini ufanywe baada ya malengo ya mashirika hayo yanatambulikana maanake ikiwa yatasajiriwa kiholrela horera basi tunaweza kusajiri hata wabudu shetani na ikaleta shida.

Kikatiba elimu ya msingi igharamikiwe na Serikali. Elimu ya msingi kwa sasa tuko na mfumo wa kutoka darasa la kwanza mpaka la nane. Igharamikiwe na Serikali.

Kikatiba, msichana anapopata mimba nje ya ndoa, awe anasoma ama hasomi. Sheria imurinde kwamba atakaye mpachika mimba ile baada ya msichana ule kuzaa kuwe kuwe na utaratibu mzuri kwamba atamuoa virui. Kama hata muoa, kuwe sheria ina mlinda yule msichana kwamba anapozaa yule msichana basi yule mwenye kumpachika mimba ile agharimike chakula na elimu ya mtoto atakayezaliwa mpaka yule mtoto afikishe miaka kumi na minane.

Mishahara ya Wabunge na madiwani ilipwe na Serikali kuu Kikatiba. Na Kikatiba wenye viti na ma mayor, wachanguliwe na madiwani. Lakini kuwe na sheria ambayo inawalinda wale ma mayor. Mara tunaona wakati mwingine mayor anakuwa ni mzuri halafu madiwani wanafanya jama, wanamung'oa. Hakuna sheria ambayo inawalinda ma mayor lakini kuwe na sheria ambaye itamlinda yule mayor anapochaguliwa, aendelee mpaka kile kipindi kiishe.

Kikatiba, waziri asiwe na uwezo wakufuja baraza. Hasa serikali za wilaya.

**Com. Abubakar Zein:** Dakika tano zimeshakwisha. Sasa uanze kufupisha.

**Martin Bongo:** Sawa. Kikatiba, waziri wa kilimo na biashara asiwe na uwezo moja kwa moja, kutoa leseni za kuagiza bidhaa kutoka nje. Maanake hii imefuja sana. Imeharibu viwanda vyetu. Viwanda kama Kenya Cashew Nuts. Viwanda kama Ramisi Sugar Company zimekufa kwa sababu sukari inatoka Egypt, inatoka wapi.

Vyeti muhimu kama birth certificate, vitamburisho vya kitaifa vingekuwa vinapatikana kwa makao makuu ya wilaya.

Katiba yenyewe iandikwe kwa lugha rahisi ambayao inaweleweka. Katiba yenyewe. Maana nyinyi wana sheria mnaiandika kwa lugha ya kisheria sasa Wanakenya wote si wanasheria. Inakuwa ukiangalia imeandikwa kisheria unachanganyikiwa.

Kikatiba, mashirika ya ufadhili, yasimamie pesa zao wenyewe. Kikatiba wataalamu wa kigeni, wachunguzwe sana kabla ya kuruhusiwa kufanya kazi hapa nchini. Na hao watalamu wa kigeni wanapokuja wasipewe uraia pia. Wafanye kazi, wamalize kama miaka miwili warudi kwao.

Kikatiba, waakilishi wa Bunge hasa sehemu za mashambani wawe ni wazaliwa wa zile sehemu. Mara tumeona wakati mwingine ni kama tunalaliwa. Mtu yule anakuwakilisha si wa kwenu na amekaa huko huko, sasa wananchi hawana uwezo

maana ni kama yule mtu amefanya kubandikwa . Sasa inatuletea shida.

Katika katiba, tarehe ya uchaguzi mkuu iwe wazi. Katiba iruhusu kabisa, ionyeshe watu kabisa tarehe ya uchaguzi mkuu.

Miswada yenye kuleta utatanishi kama ule wa Donde Bill. Wananchi pia waruhusiwe kuueleza ule mswada, watoe maoni yao. Ni hayo na nasema asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Martin Bongo. Tunayemuita sasa ni Leonard Zumbe. Bwana Dzumbe. Taja jina lako uendelee

**Leonard Dzumbe:** Kwa jina naitwa Leonard Dzumbe nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kuwasilisha pia maoni yangu juu ya Katiba. Kwanza nataka nitambue the supremacy of the Constitution. Kwamba hii Katiba baada ya kwamba imeundwa kuwe na kipengele ambacho kitakataza kabisa ifanyiwe marekebisho na Bunge. Kile kipengele kinacho sema marekebisho yafanywe na 65% ya watu wa Parliament hiyo si nzuri, kwa sababu ikuruhusiwa namna hiyo itaanza kuingiza haya mambo ambayo itakuwa ni ya ubinafsi kama vile ilivyokuwa hapo awali. Kwa sababu inasema kwamba Katiba imefanyiwa amendments thirty nine times. Na katika hizo thirty nine times haikufaa kitu, ikasababisha kuwe na hii Commission. Ikiwa kutatakikana kuwe na amendments katika the main Constitution, kufanyike kama hivi inavyo fanyika hapa kwamba tume ichaguliwe na kama kuna malalamishi mengi ifuate mstari kama huu. Hiyo ndio nilitaka niseme tu kuhusu the supremacy of the Constitution.

Now allow me to speak what I was to speak which is now written that was verbal. But what I wanted to present is as follows. It is on the role of local community in development. Na hii nitazungumza kingereza kwa sababu mambo mengine hayasemeki Kiswahili.

It is already a known fact that the Government is withdrawing itself from some of its tradition functions and as a result communities have become more and more active in governing their own development affairs. Now,the degree and speed in taking over such functions depends on the ability of the community to organize themselves and the external support in doing so. However, as much as the community would wish to take up the functions that had been traditionally owned by the Government there are some aspects in the Constitutional, legal and regulatory frame work in Kenya that hinder the process of putting development in the hands of the community. They lack a legal organ to take a leading role in overseeing and managing all developmental affairs and functions. Even the blue book on district focus strategy for rural development does not recognize any organ below the sublocation and more it is not recognized by the Constitution of Kenya. It lacks legitimacy. However if the sublocation organ were recognized it does not usually provide sufficient cohesion and trust among the various villages or groups. The district focus strategy for rural development and local authorities overlap each other which brings confusion, the Provincial Adminstration the DC, the DO the Chiefs and Assistant Chiefs taking charge of the developmental issues in a given area,

without having the necessary or popular mandate in doing so. This is aggravated by the fact that the administrative functions are mixed with the development functions. More often than not developmental measures are imposed on the people, with administrative powers of the Provincial Administration. As a result, such projects are not sustainable, they are not owned and driven by the people. And the problem that we incur is huge loss of public investment funds.

The issues that I would like to put to the Constitution now is as follows. The formation and election of a village development committee called VDC as the lowest organ of development at the grassroot level, and linking it of such sanctions to the implementation of a joined agreed intergrated long term village development plan. Three major advantages can be realized.

One, community based projects implemented individually by projects committees tend to be dominated by the interest of individual pressure groups. And it has already happened several times in this country and huge sums of money have gone to the waste. Cases reports like the women groups to the tune of 240 million was assigned by the Government, but because these groups operate as single groups such funds were wasted. And even the youth groups. Nothing is being seen at the moment. So a VDC could suffice. These individual projects committees which have been the case, always tend to reduce their commitment rather soon after initial establishment. Such as the cattle dips. Group members may lose interest they start quarrelling or depart to another place living behind project that are not maintained and not sustained. By that a lot of investment cost are lost having such projects operated under a unified VDC structure and the responsibility for project implementation given to a project committee or task force formed by the respective Self Help Group members but operating under the VDC umbrella lead to considerable higher chances of sustaining the required utilization as well as quality of operation and maintaince of the projects.

Secondly, the advantages of forming a VDC project as the lowest organ at the village level, that members of a VDC are representing the community as a whole. VDC therefore, function as the best unit for the democratisation process at the grassroot level. This is not in the same way possible for individual projects committees as they mostly lack ligitimacy because of their representation. This VDC by the way recognize the traditional clans who form as the best unit in that place.

Thirdly,what I would like enshrined in the Constitution is the recognition of the community and the rights of the communities to manage their own development affairs including funds . The particulars should be left to an Act of Parliament also mentioned in the Constitution. Because currently, funds are normally controlled at the district level and nothing trickles down to the communities.

Four, the representative system in the village development committee should be extended upwards, starting from the community up to the district level. Three levels below the district could be as follows.

1. A village level with an elected VDC.
2. Then the location with a location council, made of chairmen and secretaries.

3. Then , the divisional level with a division council made of representatives from the location council. Details regarding this arrangment should be spelt out in an Act of Parliament.
4. The district level self government structure must be clearly defined. Why? Because the present duo system with the District Focus for Rural Development Committees and the local authorities are inefficient and hardly give room for true democratic representation.

**Com. Abubakar Zein:** Your five minitues are up. You should be summarizing now.

**Leonard Dzumbe:** The composition and mandate of the District level councils and its administrative wing, all development wings must be specified with details outlined in an Act of Parliament.

5. There should be a provision to the interest that the various levels may handle their own funds relatively independent and with defined boundaries. That is in the Constitution there should be fiscal decentralisation. Funds at the district, funds at the division, funds at the location, funds at the village. Each one to have its own fund, no more funds to be handled at the district. And also they should have the right to mobilise internal and external funds, this should be granted to the village, location and the district level.

In conclusion, village development committees, potentially constitute an important factor of local governance and development but operate outside the existing legal and regulatory framework. This does not only weaken their prospects of long term sustainability it also hinders the emergence of a truly people driven development.

Conclusion number two, development once it is the full responsibility of the community and they have a degree of freedom to ask accordingly will become more people centred, more broad based and more sustainable. Its impact of poverty reduction will thus be more signicant than it is currently. Thank you very much.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Leonard. Sasa fursa hii tunampa Jackson Katana

**Jackson Katana:** Mimi naitwa Jackson Katana Mangi. Nafikiri nitaanza maelezo yangu kama ifuatavyo. Katika utangulizi wa Katiba hii, nitumetaja amani, umoja na maendeleo. Kwa hivyo Katiba lazima itaje, amani, umoja, na maendeleo. Na kanuni za kuongoza sera ya dollar. Uongozi bora uajibikaji, wazi, ukatiba na uongozi bila ufisadi na aina yeyote chafu kwa Katiba. Kwa sababu Katiba imeudwa na wananchi kupitia kwa maoni, Bunge halina uwezo wa kubadilisha sehemu yeyote bila wananchi wenyewe kupitia kwa maoni.

Tuwe na tume ya kurekebisha Katiba. Muundo na aina za Serikali. Tufuate muudo wa majimbo ambapo mamlaka ya nchi na Bunge yamegawanywa baina ya Serikali kuu na majimbo maalumu. Sababu Serikali ya majimbo itakuwa karibu na wananchi

zaidi pia kwa maendeleo kila jimbo litafanya bidii ili lisiwachwe nyuma. Pia upande wa unyanyasaji kutoka kwa kabira zile kubwa zitaisha. Kila kabila watakuwa na utawala.

Naona hakuna jia zinaoweza kufuatwa ili uwezo ufikie viwango vya Serikali. Kwa mfano katika wilaya za mitaa, ni katika viwango hivyo kunapatikana ufisadi wa hali ya juu sana. Sasa ningependekeza maafisa hawa wachaguliwe na raia na pia budget ifanywe na Serikali, odi ile inakusanywa na Serikali za mitaa iende kwa Serikali, ili kuondoa ufisadi.

Bunge; jukumu la Bunge lipanuwe. Kuwe na wananchi na kuwe na Bunge la chini, yaani jimbo. Wananchi wawe na haki ya kumrejesha nyumbani mbunge wao kwa njia ya kura ya maoni. Wabunge wafanye kazi kutegemea matakwa na maagizo ya wananchi. Kusiteuliwe Wabunge kabisa hivyo ni kuharibu uchumi wa nchi kupitia kwa mishahara minono. Wananchi wakate kauli kuhusu mishahara ya Wabunge. Sio wajipangie wenyewe kama waliofanya wakati huu. Tuwe na chamber zaidi ya moja, ili mambo madogo madogo ya mashinani, yaweze kuangariwa kwa karibu. Kwa mfano miradi vijijini, njia ndogo ndogo mfano bara bara ya Mariakani- Bamba .

Mamlaka ya nchi; vipindi viwili, miaka mitano mitano. Jukumu la Rais iwe ni kuangalia jinsi viongozi wa majimbo wanavyoongoza Rais awe kama mshauri mkuu. Ukipatikana na kashifa ya ufisadi, uzinzi na kadhalika. Na pia, hatuhitaji utawala wa mikoa.

Serikali za mitaa; Mayor achaguliwe moja kwa moja na wananchi vipindi vya miaka mitano. Mabaraza yawe chini za wizara na Madiwani waweze kuongoza kupitia Bunge, Chamber yao. Mishahara ya Madiwani, na wote itoke kwa Serikali kuu ili kupunguza ufisadi. Mapato ya kodi yaende kwa Serikali, moja kwa moja, halafu wanapata grant ndio wananchi waweze kukagua.

Elimu kwa Diwani iwe kidato cha nne, mtihani wa lugha hautoshi. Awe na ujuzi wa kazi, trade yeyote, ili aweze kuleta maendeleo. Awe na sifa ya uongozi. Diwani awe mwaminifu. Kuwe na kura ya maoni endapo Diwani amekosa kutimiza matakwa ya wananchi. Kusiwe na kuteua madiwani. Waziri afunje baraza endapo kuna ufisadi.

Haki za kimsingi; masharti kuhusu haki za kimsingi hayatoshi. Hukumu ya kifo, isiondelewe kabisa. Katiba lazima ichangie kuhusu haki za kimsingi. Usalama, afya, maji, elimu, makazi, chakula, ajira kwa Wakenya wote. Rais lazima ahakikishe kwamba Wakenya wote wanafurahia haki za kimsingi kama usalama, afya, maji, elimu, mkaazi, chakula na ajila.

Katiba isisitize usalama, chakula, afya maji, yaani Katiba isisitize haki za kimsingi. Katiba itekeleze elimu ya lazima na bure kwa wote kwanzia darasa la kwanza, hadi kidato cha nne. Wakenya wanahaki ya kupata habari za kiserikali.

Katiba lazima ihakikishe uakilishaji wa wafanya kazi kwa vyama vya wafanya kazi. Katiba ihakikishe haki zote za kimsingi kwa wananchi.

Haki za makundi; haki za wanawake zielezwe hivi. Urithi wa ardhi na mali, ghasia za nyumbani na kadhalika. Matakwa ya walemavu yahakikishwe na Katiba. Walemavu wa aina zote wahakikishiwe elimu na haki zote za kimsingi. Katiba ihakikishe elimu ya lazima kwa watoto kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Na wale walio anguka darasa la nane elimu ya ufundi, yaani elimu ya maarifa ya lazima tena iwe bure. Katiba ihakikishe makundi yanapewa ujuzi ,maarifa na msaada wa kunzisha mradi.

Haki za umilikaji wa ardhi; mtu binafsi aweze kumiliki ardhi. Serikali na inahaki kuchukua sehemu ya ardhi kwa sababu maalum lakini lazima inunue kutoka kwa raia. Kwa mfano wakati wa nyuma Wamisri waliuza ardhi yao kwa ajili ya njaa, wakati wa Yusufu. Serikali haina haki kusimamia matumizi ya ardhi. Kuwe na haki kwa wale wanaorithi. Haijalishi ni wanaume au wanawake. Wanaume na wanawake waweze kumiliki ardhi.

Makubaliano baina ya makabila, yafutiliwe mbali. Mfano wa Masai, Mazrui na kadhalika yafutiliwe mbali kabisa. Umilikaji wa ardhi bali bali na jimbo au mahali popote katika nchi paondelewe. Kama mtu ametoka jimbo la pwani anataka kufanya biashara ya kilimo jimbo lingine, aweshe kukodisha kwa makubaliano fulani. Sio kununua. Kila Mkenya lazima amiliki ardhi.

Usimamizi wa rasilimali za kitaifa; kila jimbo liweze kusimamia rasilimali zake. Bunge lina haki kuidhinisha matumishi ya fedha na ukusanyaji. Ili kuweza kukusanya mapato kwa serikali, ni lazima Katiba ihakikishe kwamba wananchi wanapata mtaji wa kuanzisha miradi ya kuzalisha mali. Kwa mfano huku kwetu kwa utenengazaji wa chumvi, utengenezaji wa sabuni na kadhalika. Kuwe na usawa wakati wa utumiaji wa rasilimali hasa upande wa ajira. Kuwe na kiwango cha sabini na tano kwa mia kwa wale wanaojiriwa kutoka jimbo na ishirini na tano kwa mia majimbo mengine. Na pia kuwe na usawa wa ajira kwa mfano labda mtu anaweza kuwa na ujuzi fulani halafu kuwe kuna yule mwenye kampuni labda ni Muhindi halafu yeye analipwa pesa nyingi labda tuseme elfu thelathini na wanafanya kazi moja. Na yule Mkenya analipwa labda elftu tatu. Hiyo itakuwa ni unyanyasaji wa hali ya juu sana kwa sababu ni ubaguzi wa rangi. Kwa hiyvo nafikiri nitakoma hapo. Nafikiri ni hayo tu niliyotaka kusema.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Jackson. Andika register na utoe nyaraka yako. Anayemfuatia ni Christopher Menza.

**Christopher Menza:** Asante. Mimi kwa majina ni Christopher Menza Tungui kutoka Midoina Sub-location. Kwa maoni yangu, mimi kwanza nitaunga mkono wale wanoasema kwamba tuwe na serikali ya muundo wa kimajimbo. Serikali hii ya muudo wa kimajimbo nafikiri italeta uwezo zaidi karibu na mwananchi. Hili ni langu la kwanza.

La pili, kwa maoni yangu ningependelea Katiba iweze kutambua kamati ya maendeleo vijijini, ama kamati za vijijini nazo ziweze kupewa mamlaka ya kusimamia kama vile maswala ya ardhi. Ardhi ya kijijini, isiweze kupatiwa mtu bila idhini ya kamati ile ya kijiji kukubaliana na kuidhinisha kwamba ardhi hii ipewe mtu fulani.

Pia kamati hizi za kijijini, ziweze kusimamia maswali kama ya utoaji wa uraia, yaani vitambulisho vya Kenya. Kwamba mtu yeyote atakayetaka kitambulisho akishaidhinishwa na kamati hii ya kijijini, basi kusiwe na pingamizi ama kupita hapa na pale, aende kwa officer wa kitambulisho na atengenezewe, apate kitambulisho chake.

Pia kamati hizi za kijijini, ziweze kupatia mamlaka ya kusimamia miradi yote ya mendeleo ili kuweza kuondoa umaskini kwenye vijiji vyao. Pia kwenye kamati hizi za kijijini pia, ziweze kupatia mamlaka ya kutatua makosa madogo madogo, kulingana na mila na desturi za wanakijiji. Pia ningependekeza kwamba Katiba hii ijao kuwe na mahakama katika ngazi za tarafa, ili kwamba kamati za vijijini zinaposhindwa kutatua matatizo ya wanakijiji, basi mlalamishi anaweza kwenda moja kwa moja kwa moja kwa hakimu ama kwa judge atakayekuwa kwa ngazi ya tarafa. Labda ningesema nitakomea hapo. Nimesema asante niko na memorandum yangu ambayo nimeandika na nitapeana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Christopher. Anayemfuatia Christopher ni Bwana Allan Kazungu. Karibu.

**Allan Kazungu:** Jina langu ni Allan Kazungu. Nina machache tu ya kuchangia. Jambo la kwanza ni kuhusu hali ya manufaa inayotokana na kodi anayetoa mwananchi. Naona kuwa mwananchi anaumia sana. Kwa kuwa hapo nyuma kabla uhuru, mwananchi ambaye alikuwa anatakikana kulipa kodi, alikuwa ni kuanzia umri wa miaka kumi na nane, kuendelea. Lakini sasa inaokena mwananchi wa umri wote hata watoto wachanga wanalipa kodi. Lakini manufaa inayotokana na kodi hizo ni kidogo. Wakati huo elimu ilikuwa ni bure, yaani huduma zote za msingi zilikuwa ni bure zote, elimu, barabara, hospitali, na hiyo ilikuwa inatokana na malipo ya wale watu wachache kuanzia miaka kumi na minane kuendelea. Tunaona hiyo ilikuwa mwananchi wa kawaida, mwananchi wa chini kabisa alikuwa ananufaika kutokana na kodi hiyo. Kile unachonunua unagharimia kabisa ni la maana kuwa wananchi wote watoa pesa nyingi zaidi. Lakini nayo manufaa yamekuwa ni kidogo zaidi. Sasa hiyo tunataka irekebishwe maana tunaona mpangilio ya namna ya wananchi kunufaika ni sharti kuliko vile ilivyokuwa hapo mbeleni. Mwananchi hafikiriwi sana isipokuwa imekuwa ni njia moja ya kumnyanyasa mwanachi tu bila kujali ananufaika kivipi.

Kwa hivyo hata ningesema kwa (inaudible) lakini pia waangalie pale zamani wananchi, waangalie katika reference kama wale watawala wa siku zile za nyuma walikuwa wakipanga vipi, mpaka huduma hizo zote zikapatikana bila shida.

Jambo lingine ni mahakama. Kwa maoni yangu , mahakama wakati huu huwa raia wa kawaida ama raia yule mnyonge ambaye hana pesa hafanyiwi haki. Haki huwa inapatika kwa yule mtu ambaye anauwezo wa kifedha. Ama ako na madaraka fulani. Hao huwa ukifanya kesi na yeye hata kama haki iko kwako wewe munyonge lazima itapotea. Kwa hivyo bila shaka wataalam wa hii Katiba, waangile namna ya kurekebisha kitu hicho.

Vile vile, viongozi huwa ni kama ambao wako juu ya sheria. Hiyo inahimisa sana ufisadi. Ningetaka hiyo ibadilike. Nikurudia mambo haya ya kodi. Kuna kodi nyingine ambayo kama mimi naonelea ni njia moja ambayo Serikali imebuni kumnyanyasa

raia. Kama ile bima ambayo inasemekena ni afya kwa taifa. Ni raia wachache sana mimi nafikiri ambao wanayoiona faida yake. Na inakuwa si hiari. Kila muajiriwa yeyote huwa tayari analipia hiyo huduma. Kwa hivyo inaonekana kuwa raia hana ujanja isipokuwa ni mtu wa kutoa tu kabla kupata faida. Kwa hayo machache, nasema asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Kazungu. Anayefuatia Bwana Kazungu, ni Bwana Wilson Kaingu.

**Wilson Kaingu:** Asante kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu.

**Com. Abubakar Zein:** Mzee wangu taja jina lako kwa sababu tunarekodi

**Wilson Kaingu:** Jina langu naitwa Wilson Kaingu. Ninatoa maoni yangu. Maoni yangu ni kwamba mwananchi wa kawaida ambaye anaishi katika sehemu hii ya kwetu anaishi maisha magumu ambayo hayawezi. Mali zake zinapochukuliwa asipokuwa na pesa, basi mali yake itapotea. Maanake utakwenda kwa wenye uwezo na utaambiwa lete kitu kidogo. Uiangalia kile kitu kidogo ni zaidi ya elfu mbili , tatu na maskini yule hana kwa hivyo hiyo hali hiyo Katiba yetu ingeangalia sana maskini vile anavyoishi katika ulimwengu huu. Ningependa maoni yangu pia yule maskini vile ambavyo anaangaliwa kwene uwezo pia maskini aweze kuangaliwa kama binadamu ambaye pia naye ambaye anastahili kuishi.

Kitu kikingine ni kwamba hata kwa upande huu wa elimu. Maskini aangaliwe kwa upande wa elimu pia na yeye awe na nafasi ya a kwenda mbele. Lakini kwa kuwa uwezo hana, Katiba hii kama ingeweza kuwasaidia wale maskini waweze kuendelea mbele katika maisha ya ulimwengu. Asante sina mengi. Mengi ni yale ambayo yamekwisha tajwa na ndugu zangu hawa. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Kaingu. Anayemfuatia ni Bwana Francis Mvoi.

**Francis Mvoi:** Asante mwenye kiti. Majina yangu ni Bwana Francis Karisa Mvoi. Ningetaka kutoa mchango wangu katika mkutano huu wa Katiba. Mimi nagusia sehemu mbili au tatu katika Katiba hii ambayo tunaitaka. Mimi maoni yangu, tumejaribu hii Katiba ya sasa na inaonekana haikutufaa sana maanake tumebadilisha mara thelathini na tisa. Kwa hivyo hiyo haifai. Ni maoni kwamba, ningependelea mvumo wa majimbo. Na kupendelea mvumo wa majimbo sio ati ni ukabila, ati tutakuza ukabila. Si kukuza ukabira. Lakini mali ya Sserikali itagawanywa sawa sawa katika mikoa hiyo kukiwa kuna Serikali ngumu katika majimbo. Hii pia italeta mashindano makubwa katika Kenya kila jimbo litataka kuendelea mbele. Na hiyo itakuwa ni maendeleo kwa taifa la Kenya. Lakini Katiba ya sasa, imekuwa na kasoro nyingi sana. Imekusa ufisadi, tume mbalimbali zmeundwa kupigania ufisadi na hatujafanikiwa.

Na hii Serikali ya sasa, imekuwa na mamlaka mengi sana. Kwa mfano pesa za Serikali wakati wa budget zinagawanywa. Kuna ngazi nyingi sana ambazo hizi pesa sina tembea. Na unaona zikifika mashinani huku muda wa kutekeleza kazi ya pesa

hizo hakuna na wanaambiwa warudishe pesa hizo hazikutumika. Sasa inalegezwaje hiyo pesa kwa Treasury na hata bara bara yetu haina murram? Kama ingekuwa Serikali ya majimbo pesa hizi zingetumika hapa, hatungekuwa na taabu ya usafiri kama vile bwana chairma umeona. Hali ni mbaya sana. Kwa hivyo ninapendelea tuingilie hii Katiba ya Majimbo, ilikuwako. Lakini kwa ulafi ikaondolewa. Kwa hivyo, nafikiri wakati umefika ili yule mwananchi alinyanyaswa kwa siku nyingi mali zake hazifaidi, afaidi na yeye kwa Katiba ya majimbo. Si ukabila. Kwa hivyo mimi maoni yangu ni kwamba Serikali ijayo, Katiba izingatie majimbo.

Na katika kile kifungo cha Pension Act Bwana Chairman, wafanyi wengi wa Serikali wamekufa bila kupata malupulupu yao. Mtu ana retire mwaka huu anangojea miaka mbili anakufa. Na Serikali iko. Katiba haizungumzii habari ya pension Act. Kama hii pension ingekuwa kwa majimbo, ingekuwa mtu haendi Nairobi aende huko ananyang'anywa, anarudi hapa kitupu. Hii Katiba hii iangalie habari ya wale walio stahafu.

Na kumalizia Bwana mwenye kiti umaskini ukubwa umeletwa na elimu. Elimu imekuwa ghari matibabu yamekuwa ghari. Ni wakati sasa Katiba ya Kenya izingatie elimu ya wote, elimu bora. Kila mtoto wa Kenya ajivunie elimu., iwe ya bure. Si ya bure na strings nyingi sana. Hapana. Ikiwa ni ya bure ni ya bure. Na hata kama matibabu ni bure. Iwe ni bure. Isiwe hata na cost sharing, hivi na hivi. Serikali ina mamlaka na ina haki ya kulinda wananchi wake. Kwa hivyo Katiba hiyo kama ingizingatia haki hizo nafikiri tutakuwa na Serikali nzuri na kila Mkenya alipo atafurahia kwa Katiba hii ya mfumo wa majimbo. Asanteni sana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Karis a. Anaye mfuatia ni ndugu Samson Kahindi.

**Samson Kahindi:** Kwa majina naitwa Samson Kahindi. Niko na maoni kidogo ambayo ningependekeza katika Katiba hii ya wakati huu. Kwanza nataka nizungumzie kuhusu masilahi ya mwananchi. Tunaona ya kwamba Serikali hii yetu ambayo tuko nayo wakati huu inakaa kama imedharau mwananchi kabisa kabisa. Nataka kuzungumza hivyo kwa sababu ya upande wa employment. Tunaona kwamba kunao wengi ambao hawajapata kazi. Kunao wengi ambao wameenda shule, wameenda tena colleges lakini bado hawajapata kazi. Sasa nataka kupendekeza kwamba angalau Serikali iwe inajali masilahi ya mwananchi katika kiwango cha chini kabisa. Kama pengine tuseme tuna mwanchi fulani ambaye ameenda college fulani, pengine ya medicine ama college ya teaching. Wakati akitoka kule hata kabla hajapata kazi, apewe kitu kidogo ambacho kitam-sustain mpaka wakati ule ambapo Serikali itakuwa imeimarika kupata fedha za kumuajiri huyu mwananchi.

Nataka pia nije katika kiwango cha chini kabisa kwa mwananchi. Nayo tunaona ya kwamba wananchi wengi wanaishi below the poverty line kwa sababu wanaishi katika hali ya umaskini sana. Katika hali ya kusaidia huyu mwananchi, tunapendekeza ya kwamba katika Katiba hii Serikali ambayo itaundwa ihakikishe ya kwamba kila mwananchi anapata kiwango fulani kwa mwezi, awe ni mzee. Tuseme yule mwananchi ambaye amefikisha kwango cha miaka kumi na minane ama ishirini yule ambaye amemaliza shule, apate kiwango fulani kwa mwezi, iwapo hana kazi, tunazungumza kuhusu wale ambao hawana kazi wawe

wanapata kiwango fulani hata kama ni shilingi mia tano kama ni elfu moja kwa mwezi ili kuhakikisha ya kwamba maisha yake yanaendelea vizuri.

Jambo lingine ambalo nitaka kuzungumzia hapa ni kuhusu kutetea mwananchi kimaisha. Tunaona ya kwamba tunaishi katika nchi ile moja. Kuna wengine wako na kazi wengine hawana. Lakini ile difference ambaye iko in fact hata kwa wale ambao wako na kazi hiyo difference inakaa kubwa sana. Kwa mfano tunaangalia mfanyaji kazi fulani kama ni Mbunge, ama kama ni civil servant yeyote yule lakini anapata kile kiwango cha mshahara cha juu kabisa cha mtu ambacho anapata kiko juu zaidi kuliko yule anayepata kiwango cha chini. Na tunapata kwamba wao wanaishi katika nchi ile moja,uchumi ni ule mmoja, bei za bidhaa za dukani ni zile zile. Lakini tunapata kwamba mmoja anapata pengine ni four hundred thousand, halafu mwingine huko anapata five thousand shillings. Hiyo difference unapata ya kwamba ni kubwa sana. Kwa hivyo katika kurekebisha hii Katiba mimi nilikuwa napendekeza ya kwamba anangalau kama yule mfanyaji kazi wa kiwango cha juu atapata four hundred per cent, na yule wa kiwango cha chini apate ten per cent of the four hundred per cent,ambayo itakuwa ni kama fourty thousand. Ingekuwa kidogo ina-equalise mambo kidogo. Kuliko mmoja apate pesa nyingi four hundred thousand na mwingine anapata five thousand huku chini. Hakuna ile haki ya kisawa sawa.

Kitu ingine ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia ni kuhusu hizi powers za President. Tunataka hizi power za President ziwe limited kidogo. Kwa sababu tunapata ya kwamba ana powers nyingi ambazo zimepita kiasi. Kwa mfano hizi power zingine za kuruhusu wafungwa. Mmoja amekosea katika kifungu cha sheria na amehukumiwa kufungwa maisha lakini kutoka na hali hizo, tunaona ya kwamba Rais tunasikia anatoa msamaha. Kuna ule masamaha wa Rais. Sasa tunapata ya kwamba, hali hii inauimiza wananchi sans haza yule ambaye amekosewa. Sasa mtu wako ameendwa kufungwa, na pengine ameua. Unasikia tena baada ya mwaka kama mmoja amepata msamaha wa Rais. Hiyo inakuwa ni mbaya. Hizi powers tunataka zipunguzwe na ziwe katika judiciary sana sana. Kwa hayo machache, naona nitaachia hapo.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Samson. Ungeenda pale utoe walaka wako, u-sign register. Nadhani tumeongezeka wengi. Nikuwakumbusha tu, ukiwa na mswada wako umeandika, hutaki kuzungumza unaweza kupeleka pale uka-sign ukapeana mara moja mswada wako. Ikiwa unangojea kutoa mswada na maneno machache, subiri tukuite. Ikiwa unataka kutoa maneno bila mswada, bila usubiri tukuite. Sawa. Kuna mtu ambaye amekuja na wale watoto pale nyuma. Kuna mwalimu amekuja na watoto. Mwalimu yuko hapo? Watoto wanataka kutoa maoni? Wako na shairi, basi watayarishe waje baada ya kumwita mtu mmoja, wawe tayari kutoa shairi. Watoto wako tayari kutoa shairi kwenye kikao hiki pia tunakubali. Sawa jamani.

**Audience:** Sawa

**Com. Abubakar Zein:** Anayekuja ni John Kombe.

**John Kombe:** Kwa majina naitwa John Kombe na niko na machache ya kusema. Mwanzo napendekeza pawe na Serikali ya majimbo. Na katika majimbo haya, napendekeza kuwe na Serikali ndogo kila jimbo liwe na Serikali yake ambapo hapo kutaundwa Serikali kuu. Kuwe na Serikali za majimbo na katika Serikali hizo waungane na waunde Serikali kuu.

Naunga mkono kuhusu vyama vingi. Na ningependelea vyama hivi viwe angalau vitatu. Visizidi vitatu kwa sababu tumeona vyama hivyo sana sana huwa vinaundwa kwa misingi ya kikabila.

Uwezo wa Rais, upunguzwe kwa mfano tunaona ya kwamba kuwa huyu, huwa ndiye anaajiri majudge na permanent secretaries. Kuundwe tume ambazo zitakuwa zikiajiri watu hawa.

Rais asiwe juu ya sheria, yaani above the law. Awe kama mtu mwingine. Hii huwa itaondoa matumizi mabaya ya mamlaka. Misuse of power. Na asiwe mkuu wa majeshi. Rais asiwe mbunge, achaguliwe tayari na wananchi.

Wale ambao wameacha kazi, ama retirees, wasipate fursa nyingine ya kuongoza mashirika au sehemu nyingine. Ni hayo machache.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana John Kombe. Sasa tuwakaribishe watoto tusikie watoto wana yapi ya kusema. Watasema yao kupitia shairi. Watoto msiogope, njooni tu huku mbele, njooni.

**Rodger Sayo:** Jina langu ni Rodger Sayo.

**Kadzo Francis:** Jina langu ni Kadzo Francis.

**Joshua Dickson:** Jina langu ni Joshua Dickson

**Fred:** Jina langu ni Fred tunashairi, karibuni.

Baba na mama ni nani mwema?
Ni baba au mama?
Baba na mama ni nani mwema?
Titi la mama nilinyonya
Tumboni mwa mama miezi tisa
Ni nani mwema?
Baba na mama ni nani mwema
Karo ya shule baba analipa, nguo, malezi ananua

Ni nani mwema?

Baba na mama ni nani mwema

Asanteni.

Katiba, Katiba hebu tuelezee, Katiba ni kitu gani?

Wengine hutuambia, ni mkusanyiko wa majina,

Katiba ni kitu gani? Hebu tuelezee

Katiba yaendeleza matarajio mema, ikiwemo elimu yetu, kujenga haki zetu, hasa za watoto

Katiba ni kitu gani? Hebu tuelezee

Pia twaeza sema, Katiba sheria kuu ya nchi ilindayo masilahi

Katiba ni kitu gani? Hebu tuelezee

Shukrani. (clapping)

**Com. Abubakar Zein:** Jamani hebu wapigieni watoto makofi. Hayo hayakutosha jamani. (clapping) Unaona mtu anaweza kutoa maoni hata kwa mashairi. Watoto wametoa maoni yao kwa mashairi. Makofi tena. Mwalimu asante sana na uwashukuru walimu wenzako. Nasema asante sana mwalimu. Baada ya watoto kupata furlsa kutoa maoni yao. Tunamfikia Bwana Lennox Mwacharo

**Lennox Mwacharo**: My name is Lennox Mwacharo. I have brought the following proposals for the Constitution. Constitutional Supremacy- the public should be involved through referenda in amending the Constitution in all parts. Selected committee should conduct the referendum as in the case now.

As far as citizenship is concerned, anybody born in Kenya should be regarded as an automatic citizen. Constitution should allow for dual citizenship in special conditions. That is marriage in case somebody marries another person from another country or political exiles. Identity cards as in the case now should be used as evidence of citizenship.

Political parties should be seen in community as development aspirants. They should not just aim at politics and other tribal driven issues. The Constitution should regulate their formation, management and conduct. The number of course should be limited. We should have at least four parties. They should be financed by the public funds but on their own struggle. The should correct and advice the state on any issues they feel are wrong.

Structures and systems of Government. We should adopt the federal system of Government. This enables the less developed region to share and enjoy their resources effectively. For example other areas have got more universities than other areas. Other areas have got more polytechnics than other areas. This has dragged down those non-developed areas and they have been as people who are not development conscious.

Parliament should vet appointments of all senior civil servants and other senior posts in Government and in Government owned companies. Moral and ethical qualification should be introduced. People should have a right to call their MPs by a vote of no confidence. Women should struggle to get their way through the Parliament just like their men counterpart. The Government should consider and determine the salaries and benefits of MPs.

Executives; qualifications for a Presidential candidate should be at least thirty years and above. And if possible be of university level and if not so have twenty years experience and above in the parliament. Tenure of presidency should be two terms and should be rotational. From one region to another. If we have one President from the Nyanza Province, next time we have one from another province. Powers of the President should be reduced especially that of appointing prominent people to the Government, except for Ministers.

You find that if somebody is financially unable he can't just go through a suit in a court of law and find the rich man taking advantage of the poor man. This should not be so.

Widows should have access to their late husband's property and be given full power to inherit such wealth. You will find in other areas women are not given any right to inherit wealth when the husband dies then the whole wealth is taken over by the brothers or other relatives of the deceased. This should not happen. Women also should be given special appointment in the community leadership. Chairpersons of schools or leadership and any other honour.

Land and property rights; legal communities should have the ultimate ownership. That is land should be owned by the local person. The Government should have the power to compulsory hire acquired private land if the land is not well utilized, if the land is too big to be owned by an individual. Preferably each person should at least have a maximum acreage of one hundred. The excess should be subdivided to other people who have no land. If there are squatters who have lived in that land for more than ten years, the land should be subdivided to them. The word squatter should be removed because if we are squatters, then where didi we come from. Yet this is our own Kenya. Land should not be sold without the consent and endorsement of the family members. That is the husband should not have a right to sell land without contsulting the wife or the children.

No foreigner should own land when indigenous residents have not acquired any. All land should be subdivided and the title deeds issued to the residents.

Local Government; Mayors and Council chairmen should be directed directly by the people. They should serve for five years just as they have been elected as councillors to serve for five years. Education qualification should be at least form four and above. There should be moral and ethical qualifications also. The Local Government should determine their remuneration.

Basic rights, there should be a dispensary for a distance of at least seven or four kilimeters to enable the citizens enjoy healt facilities. There should be tapped and clean water in every village to relieve the communities of the problem of water especialy in same dry areas like Bamba and other places in the country.

There should be compulsory free education for all primary school going children. The Government should look for ways to construct classes. That is the end of my presentation.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Weka tu pale u-sign. Christine Kahindi?

**Christine Kahindi:** Kwa majina naitwa Christine Kahindi. Mimi naunga mkono wenzangu walio ongea kuhusu majimbo. Hilo naliunga mkono sana.

Nikuzungumzia langu la kwanza nazungumzia kuhusu urithi. Katika hii hali ya urithi, tunaona kwamba akina mama wengi huwa wananyanyaswa. Wakati bwana amekufua, ile mali ambaye angerithi, inarithiwa na mtu wa ile mbari ambapo mama yule huwa ameachiwa watoto, ana kazi ngumu yakuwangaalia, awasomeshe, ana kazi ngumu ya kuwapatia chakula. Sasa kule kurithiwa kule si kwamba atafaidika. Lakini ni kuwa ananyanyaswa kiasi ya kuwa ile mali ikiisha yeye atabaki tu akihangaika. Kwa hivyo nataka kwamba huu urithi uwachiwe yule mama ambaye ataachwa pamoja na watoto wake.

Jambo lingine ni kwamba kuna hii hati ya mashamba. Wakati bwana anapotafuta zile hati za mashamba ni lazima aandike jina la bibi yake, pamoja na watoto. Ili wakati anapoondoka mali ile iwe pamoja na shamba litarithiwa na family yake. Si kwamba atafute mtu wa nje amwandikie ama amwandike jina. Wakati imekuwa mbaya yule hana ile haki ya kumiliki kwa sababu jina lake litakuwa haliko pale. Kuna wengine ambao imetokea hata imekuwa mbaya kwa akina mama. Ni kama bibi ameolewa, amezaa binti yake. Halafu, akiwa amezaa binti yake tena yule baba sijui huwa ameshikwa na shetani gani anamrundia yule binti wake anakuwa bibi yake. Mtu kama huyo anapopatwa, lazima apatiwe adhabu kali. Kuna mambo ya mikopo. Wakati mtu yeyote, baba, mama anataka mkopo, lazima apewe mda kidogo ili ajitafutie halafu ndio kuwe na mda wa kulipa. Tena malipo yale, yasiwe ya juu kiasi ya kwamba hata kama ni kufanyia kazi mkopo ule, huwezi kulipa.

Kuna lingine kuhusu kule kuishi; kama sehemu hii yetu ya Bamba. Tumekumbwa na shida nyingi kuhusu maji na barabara, zimechukua mda. Na ikiwa Serikali imeonelea kwamba lazima ituhusishe katika hii hali ya Katiba, akina mama wangependelea sana hii shida ya maji iangaliwe sana. Yaani mifereji ya maji iwe itapatakaa baada ya kama hatua kidogo. Ili mama ama familia ile iwe itapata maji bila shida.

Na kitu kingine ni hospitali. Tunaona kwamba ma hospitali ziko hatua hatua ambapo mama akishikwa na shida hata kama ni mtoto, baba itambidi atembee mda mrefu. Ambapo hata kama ni ugojwa wa kumudoa mama yule ama baba yule si ajabu atakufia njiani. Serikali iangalie kwamba hospitali ziko karibu na mahali pa kujifungulia akina mama pawe karibu ili huduma zao

wazipate karibu.

Na bara bara pia. Hi hali ya bara bara imekuwa mbaya mda mrefu. Ikiwa serikali imeamuwa kwamba sisi tuhusike katika Katiba. Naiangalie sana kuhusu bara bara hasa hizi sehemu zetu za vijijini. Unapotaka kwenda kama town utapata shida, utatembea mda mrefu kwa sababu ya bara bara. Ikiwa Katiba inataka sisi nasi tuhusike na ituangalie vilivyo. Tuangaliliwe bara bara, tuangaliliwe maji, hospitali hii itatufanya sisi nasi tujisikie tuko Kenya hii. Sio mtu anatembe tu dakika moja mtu anafika hospitalini na wengine wanatembea mwendo mrefu mpaka anafikia wakati anakufia jiani. Lazima Serikali iangalie haya mambo.

Na kwa ajira za watoto; tunaona wazazi wengi hawana ile nguvu ya kuwasomesha watoto wao ama kuwafundisha. Sasa serikali ijaribu kuchunguza. Baba je hajiwezi kweli, ama ajifanyisha. Maanake kuna wazazi wengi kweli wanajifanyisha kama hawana lakini ukimwangilia utampata yuko na mali ya kufundisha mtoto. Lakini sasa ambaki tu. Sijui kama anataka mtoto yule awe jambazi kesho au sijui huwa anamwakilisha vipi kimaisha. Kwa sababu yule mtoto anapokosa elimu, kesho yake atakuwa jambazi. Kwa sababu atakuwa anadai haki yake wewe hukumusomesha. Hivi basi, tunaomba Katiba hii kwamba watoto wawe wanangaliwa vilivyo kwa elimu, na kama kutakuwa na mtu yeyote ambaye hawezi kumpeleka mtoto shule, aangaliwe. Ni kweli kwamba anajidanganya ama anadanganya watu kwamba hana kitu. Na ikiwa anandangaya watu kwamba hawezi kufundisha, achukuliwe hatua ili asomeshe watoto. Maana hii ndio itapunguzu huu umaskini.

Na jambo lingine ni kuhusu elimu. Tunaona ya kwamba hata sisi wazazi wa huku chini, tunajaribu sana kufundisha watoto. Lakini wakati wanapopita wanapo jaribu kwenda shulei ya upili, wakifika kule watakuta kwamba yale masomo bora hawayapati. Wanaachiwa tu masomo yale ya chini na hata hapo wakitoka shule hawa wezi kupata kazi kwa sababu elimu wamepata ile ambayo haina msingi. Lakini tunaona kwamba, watoto wasehemu za chini wanapopata fursa ya kwenda skuli za chini masomo yale yale ambayo wenzao wanapata , yale bora ndio nayo wayapate. Ndio watakuwa wanagawanya huyo usawa. Sio watoto wa huku chini. Wafikapo huko wanapatiwa yale masomo ambayo hayawezi kuwapeleka popote hali watoto wengine wanapatiwa yale masomo ambayo yananawafaidisha hata wakitoka hapo tayari wanapata kazi. Hiyo itakuwa ni ubaguzi. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Christine. Sign hiyo register hapo halafu baada ya Christine ku-sign register, yule binti atakuja achukue karatasi alioandika mzee Kahindi. Mzee Kahindi nimesema nitampa fursa ile nitawapa wazee. Lakini akamua atoe maandishi kwa hivyo ashatoa maandishi yake kwa hivyo ata-sign tu register. Na ikiwa kuna bi-kizee au mzee ambaye yeyote, mzee wakiume au wa kike ambaye anahitaji kupewa fursa azungumze atakuwa amechoka kukaa. Akitualifu sisi tutampa fulsa ya mbele. Tulikubaliana hivyo. Sio

**Audience:** Ndio

**Com. Abubakar Zein:** Anayefuata ni Rodgers Baya.

**Rodgers Baya:** Kwa majina mimi naitwa Rodgers Baya. Mswada nishaandika. Nataka nizungumze kidogo tu kuhusu mswada huu. La kwanza hii Serikali inayokuja, sisi tunataka Serikali ya majimbo. Haswa mimi napendekeza hivvyo. Serikali inayokuja, iwe ni Serikali ya majimbo. Hii majimbo imezungumziwa tayari hapa na wenzangu na vile walivyo ongea, ni sawa. Majimbo siyo ati tunafukuza mtu. Lakini kila jimbo liwe linaweza likajumudu kihali na mali. Serikali kuu iwe pale vile vile. Ikiwa tutakuwa na Serikali ya majimbo, labda hizi haki zetu nafikiri zitatekelezwa vilivyo maanake kila mmoja atakuwa analima shamba lake.

Serikali yetu imetutangazia ya kwamba ifikapo mwaka wa elfu mbili, kila mahali patakuwa na maji. Kila mahali patakuwa na bara bara nzuri, kila pahali patakuwa na hospitali, kila pahali labda patakuwa na university ama institution na shule nzuri. Na kila mmoja atakuwa amepata kazi. Lakini mpaka dakika hii, hiyo yaonyesha haijafaulu ama haitaweza kufaulu. Labda tunaweza tukasema katika huku kwetu Pwani na haswa upande wa reserve kama huku Bamba, Vitengeni na Ganze watu wametaabika sana na maji. Maji ndiyo uhai na Serikali imetangaza hivyo, hilo janga la maji lakini sasa haitilii maanani. Tunaka hiyo Katiba ambayo inakuja, maji haswa yawe muhimu kwa binadamu. Kitu cha kwanza ni hicho, njia zirekebishwe ama zitengezwe ziwe na lami kusudi nasi ama watu wa hapa wajisikie ya kwamba nao wako katika Kenya. Hospitali, ziwe katika kila location. Skuli zijengwe vizuri na Serikali na ziwe za bure kuanzia nursery mpaka standard eight.

Ukulima, hizo ni haki za binadamu. Ukulimia tuwe tunaweza tukapata bidhaa ambazo zinaweza kutufanyia sisi huku tuwe tunaweza kupata mavuno, ama ukulima wetu uwe mzuri zaidi kama vile matinga tinga. Katiba hii iwe itahakikisha Serikali imetoa misaada hiyo kwa kila mmoja.

Kuna hawa watu ambao wamesoma na hawana kazi, na kuna wengine ambao hawakusoma na hawana kazi. Ingekuwa Katiba itakuwa na haki za binadamu ya kwamba mtu yeyote yule ambaye anaishi Kenya hii awe ambaye hana kazi, awe akipatiwa bashishi yeyote ile yakumwezesha yeye mwenyewe kujimudu katika maisha yake. Hiyo itapunguza labda wizi, ukora, ulaghai wa kila aina. Maanake wewe ikiwa ni zile pesa za kununua chakula utakuwa unazo.

Tukiendelea upande wa ardhi. Kila Mkenya, anastahili kupewa haki yakuishi hapa Kenya. Makao maalum ambayo yamechaguliwa na cheti apewe. (inaudible) wewe ukiambiwa hapa ni kwako, usipoambiwa hapa ni kwetu, hutayajali masilahi ya pale pahali. Kwa hivyo kila mmoja awe amepatiwa pahali ama cheti cha kumiliki pale. Sisi watu wa Pwani tumetengwa sana kuhusu kupewa title deed. Tumetengwa sana. Ndio tunaitwa ma-squatter huku kwetu. Mtu anaitwa squatter pahali ambapo yeye amezaliwa. Pahali ambapo yeye, mababu zake wako pale, pale, wamekufia pale pale na yeye anaitwa squatter. Hana pahali pa kwenda. Huyu mtu alizaliwa binguni akaangushwa. Kwa hivyo hilo neno la squatter katika mkoa wa Pwani liondoke.

Na kuna ile ambayo inaitwa GL. Government land. Kuhusu Government Land; Serikali inachukua pahali hapo, ama inamiliki ardhi ikimnyanyasa mwananchi wa chini ya kwamba hapo panamilikiwa na Serikali na yeye mwenyewe mwananchi ni Serikali. Sasa hatujui Serikali ni ipi. Tunataka Katiba iwe itahakikisha ya kwamba hizi ardhi ambazo zinaitwa ardhi za Serikali GL zigawanyiwe watu wale ambao wanaitwa squatter. Kuna sehemu zingine ukifika hapa pwani kuna watu wengine ambao labda ile Katiba ya zamani imekuwa ikiwajali wengine kushinda wengine. Kwa mfano kuna mazrui. Protectorate. Hao walipewa uwezo ama walipewa uhifadhi mzuri kuliko wale indigenous people ambao wanatoka huku. Treatment kama hiyo, sisi hatuitaki. Tunataka kila mmoja afurahie ama a-enjoy ile freedom yakuwa yeye ni Mkenya na anaishi Kenya. Na kwa hii Ten Mile Strip, ambayo Miji Kenda wengi wamefukuzwa kule. Wakapelekwa mashambani, mashamba ambayo yamekuwa misitu, na sasa hayo yameketi bure huko. Ambapo ukifika huko, ukitaka kujenga nyumba yako unaambiwa hapa wewe huwezi kujenga nyumba kwa sababu ya kuwa wewe huna kile kiwango cha kuketi huko. Tunataka hii iondolewe. Iko kama Kilifi plantation. Ni watu wengi sana wamefukuzwa kule. Tunapigana na njaa, tunapigania ardhi lakini ardhi iko vast, kubwa na watu wanaitwa ma-squatter. Kwa nini shamba lile lisigawanywe na watu wakapata vipande vyao wakawa wanamiliki ardhi ile.

Lingine ni Serikali za mitaa: Mayor na Chairman. Mimi maoni yangu ningesema hao wachaguliwe na wananchi wenyewe. Sio wachaguliwe either na Councillors. Hapana. Wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe. Na hao Mayors au Chairmen awe ni watu ambao wana elimu ya kujulikana. Councillors vile vile. Wawe wametoka kuanzia kiwango cha kidato cha nne. Huu ndio kuondoa umaskini wa akili na ujuzi. Huyu chairman na mayor akichaguliwa, awe anachaguliwa na wananchi kwa kipindi cha miaka mitano. (inaudible) hii itapunguza mizigo kwa zile local authorites.

Katiba ijayo ilinde sana na itilie maanani zile mila na haki zao. Tukiingilia usawa, tunataka hii Katiba ambayo inakuja iweke usawa kwa mke na mume. Mwanamke asifanywe mtumwa hata kidogo. Maanake yako makabila mengine ambayo mwanamke hufanywa kwamba yeye ni mtumwa.

**Com. Abubakar Zein:** Tungetaka kumkaribisha Bwana Waziri, na kumuomba Bwana Rodgers Baya aendelee.

**Rodgers Baya:** Asante. Nilikuwa nimefikia upande wa usawa. Tunataka Katiba yetu iseme ya kwamba kila mwananchi hapa Kenya ana usawa wa kuishi na kumiliki na hali kadhalika. Maanake utakuta kwamba labda Katiba ya Kenya ambayo iko, inajali masilahi ya mwanamume kuliko ya mwanamke. Mwanamke amefanywa kama mtumwa. Hiyo Katiba ambayo tunaitaka , kila mwananchi, awe na usawa katika Kenya.

Ufisadi unaweza kupungua katiba yetu itaamua ya kwamba kila mwananchi awe spy wa kipekee. Maanake sheria ama labda ile Katiba ambaye iko haitilii mkazo mambo ya ufisadi. Hata ukienda ukiuzungumza tena wewe hautachukuliwa na uzito fulani. Hatuna uhuru wa kueleza kwa uzito kinaga ubaga hali ilivyo. Kama vile nilivyo sema huu mswada wangu nimeuandika, hayo machache tu nilikuwa nataka ku highlight kusudi muyajue. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Rodgers Baya. Ili kukumbushana tu naona watu wengi sana wamezidi nakumfahamisha pia Waziri kwamba tumeshachukua maoni ya watu ishirini na moja walio zungumza na kutoa memoranda na wengine kama ishirini walio toa memoranda bila kuzungumza. Tunawaruhusu watu dakika tano wakiwa na memorandum kutupa highlights. Dakika kumi ukiwa na mazungumzo peke yake. Lakini kila mtu anahaki ya kutoa mswada bila kuzungumza ikiwa anataka hivyo. Sasa tungependa kumuomba Samson Koi? Hayuko. Mekane Charo? Kasichana Kazungu? Mama karibu. Esther? Utahitaji kutafsiri pengine.

**Kasichana Kazungu:** *Mimi naifwa Kasichana wa Kazungu.*

**Bi. Esther:** Her name is Kasichana Kazungu

**Kasichana Kazungu:** *Rangu mimi ni ra kuhusu mashomo*

**Bi. Esther:** Her main concern is about education

**Kasichana Kazungu:** *Ni ahoho, vesomesha na hudzakala hunasomesha adzukulu ehu.*

**Bi.Esther:** She has educated her children and now she is educating her grandchilren and there are no jobs for them.

**Kasichana Kazungu**: *Kazi kazipatikana hunazisikira maredioni.*

**Bi. Esther:** She hears about jobs in the radios

**Kasichana Kazungu:** *Ela zho zha mutu kuku be abwire kazi…*

**Bi. Esther:** And in this place there are no people who are being employed

**Kasichana Kazungu:** *Na fukiona mutu adzire ni wa kazi, hunashangaa*

**Bi. Esther:** so when they people coming these sides who are employed they wonder where do these people get jobs

**Kasichana Kazungu:** *Ra hiri ni barabara*

**Bi. Esther:** Secondly, is about the roads.

**KasichanaKazungu:** *Ra hahu , ni nzala*

**Bi. Esther:** It is about hunger,

**Kasichana Kazungu:** *Vikara kicho kitu kicho ndicho kidzanituma hata nidzakeresi haha. Sina zaidi.*

**Bi. Esther:** That is her major concern, and that is why she has come here. She has no more.

**Com. Abubakar Zein:** Mshukuru mama mwambie tumesema asante sana. Asante mama. Tunamuomba Alice Kahindi?

**Alice Kahindi:** Kwa jina naitwa Alice Kahindi. Tunataka utawala wa kura. Bunge itolewe kwa maoni ya kura kuonekana. Pia tunashida ya maji na barabara. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bi Alice. Tunamuomba Bwana George Charo? Hayuko. Bwana Ali Mwinyi?

**Ali Mwinyi:** Asanteni sana. Kwa jina naitwa Bwana Ali Mwinyi. Mkutano wa leo ningependa kuchangia pointi zangu kama tatu hivi kulingana na marekebisho ya Katiba. Na jambo la kwanza nimezungumzia hii sheria ambayo inasema `the President is above the law' Nafikiria sheria hii ingelifutwa. Kwa sababu kuna watu wengine ambao wanaamini ikiwa watakuwa Rais halafu hii sheria ya `the President is above the law' watatumia hii sheria vibaya sana. Kwa hivyo naomba hii sheria iangaliwe.

Pointi nyingine kuhusu majimbo. Sisi watu wa Pwani tungeomba kuwe na majimbo. Maanake kwa muda mrefu sana tumeona tumelaliwa sana kwa jia moja au nyingine. Mfano mzuri ni kama hali ya elimu. Nafikiri hapa pwani hakuna hata chuo kikuu. Na nafikiria ni wakati ambapo pia sisi angalau tungekuwa na chuo kikuu hapa pwani pia. Utaona kuna mambo mengine pia kama mambo ya utalii. Hapa Pwani tuko na beach hotels, tuko na mbuga za wanyama. Lakini utakuta kwamba kama unataka kufanyia hizi kazi za utalii mpaka uende Nairobi, Utalii College ukasomee huko. Sasa utakuta sisi watu wa Pwani hatuna access na hizi kazi za utalii. Maanake kuenda tayari mpaka Nairobi ukakae usome mambo ya tourism Nairobi, inakuwa ni ngumu kwetu. Kwa hivyo tunaona ya kwamba tuko na Beach Hotels hapa kuna touring companies lakini sisi hatuwezi kufanya kazi huko maanake hatuna access na ile institute ambayo inatoa education kuhusiana na mambo ya hiyo tourism.

Halafu upande mwingine ni kuhusiana na hizi post kubwa kubwa hapa Pwani. Unakuta kama mkubwa wa ports anakuwa pengine labda ni mtu wakutoka sehemu zingine, ama mkubwa wa poster. Unakuta sisi hapa Coast vijana tuko lakini tunashindwa kupata nafasi za kazi maanake kama mnavyojua Kenya hii yetu watu wanachukuana kulingana na ukabila. Sasa unakuta wewe kweli ni mkazi wa hapa Pwani lakini sasa wewe hupati nafasi ya kazi kwa sababu kama ni mtu mkubwa kama ni port ama ni wapi, si mtu wa Pwani. Kwa hivyo nafikiria pengine tukiwa na majimbo mambo kama haya yataangaliwa, pia sisi tungekuwa tumenufaika kutokana na hivi vitu ambavyo vinastahili tunufaike. Maanake mambo kama haya pia sisi tungelipewa

priority kama watu wa Pwani.

Halafu lile jambo lingine ni kuhusu ufisadi. Nafikiria hii mambo ya kwamba kwa mfano kama headmaster ama mtu anayesimamia shirika la umma, unakuta anafanya ufisadi. Halafu unakuta pale badala ashtakiwe ama mali yake ichukuliwe a compensate zile pesa amekula, anapigwa transfer. Sasa unakuta hii haitusaidii kama wananchi. Ambapo tunaomba kwamba Katiba ingeundwa kiasi ya kwamba watu kama wale wakishikwa, jambo la kwanza ni mali yao inachukuliwa ina recover zile pesa ambazo wamekula. Halafu kama kutakuwa na kushtakiwa lakini at least ile pesa ambayo ile amekula, isipotee namna hiyo kuwe na njia ambayo zile pesa zitarudi kwa lile shirika lililohusika.

Jambo lingine nilitaka kuzungumzia ni kuhusu uzembe baina ya wafanyi kazi wa Serikali. Utakuta kuna wafanyi kazi wa Serikali. Baadhi yao utakuta ni wazembe. Utakuta wamefanya kwa Serikali throughout unamuona yeye ni mlevi. Hata unashindwa kwamba yeye hufanya kazi gani. Na unashindwa yeye ako service kutoka January mpaka December anapata mshahara na ile kazi ambayo anafanya huioni. Na yule mtu unashidwa, ile kazi haiyonekaniwi na yeye hafanyi, na kuna mtu mwingine ambaye angepatiwa kazi hapo pengine angefanya vizuri. Kwa hivyo tunaomba hii Katiba iundwe in away watu kama hao pia wataondelewa wawekwe watu wengine watakaosaidia raia sio tuwapate watu ni walevi, mtu haendi kazini, vile unamuona yeye mtu huenda kazini kila siku. Kwa hivyo tunaomba Katiba yetu pia iangalie mambo kama haya.

**Com.Abubakar Zein:** Asante sana Ali muda wako umekwisha ungekuwa unafupisha sasa.

**Ali Mwinyi:** Sawa, na jambo la mwisho ni kuhusu kilimo. Tunaomba Katiba yetu ikiundwa mambo ya kilimo yapewe umuhimu zaidi. Unakuta kama pahali kama lake Vitoria like ni lake ambapo ninafikiria kama hii Katiba ingeundwa kihali ya kwamba lile lake litumiwe kufanya irragation kwa area hizi kama ukambani wapi, nafikiri ingekuwa vizuri sana. Hata pia ingesaidia katika poverty eradication. Kwa hayo machache na shukuru.

**Com. Abubakar Zein:** Anayefuatia ni Bwana Moris Nguma. Tunamuomba Bwana Moris Nguma aje atoe maoni yake. Katoka? Samson Shida? Wewe ndiye Samson Shida? Nimemuona ameinuka nikafikiria ni yeye. Anderson Ziro? Ni wewe Anderson? Karibu sana.

**Anderson Ziro:** My name is Anderson Ziro. Nitachanganya lugha hapo. As we have eight provinces, these provinces should become regions. Then (inaudible) then we elect the President. This president will be there for a period of time and for the resources of these provinces, I suggest that if we have this type of Government, the resources, eighty per cent or sixty per cent of whatever comes from that province or region remain in that area to cater for priorities of the needs of that area. If it is education, the first priority to go to education. If it is the roads, the first priority to go to roads. The president to remain there and the twenty percent or forty percent to go to the central Government. With the Central Government I suggest that this central Government only looks for essential things that is stand for security for example, only security and seeks funds from

other Countries .Those funds should be distributed to these regions so that they can be added to funds or to the taxes that will have already been collected to cater for the needs of these people.

I would suggest also, as we have eight regions then the President should come from a different region that is the Presidential post should rotate among the regions, so that the nationalcake is well distributed to the people. As I have already said that I am for regional Government I know experts know what is for regional Government so I should not talk much to elaborate but they sit and do what is necessary for Kenyans. Thanks. God bless you.

**Com. Abubakar Zein:** Asante Bwana Ziro. Tunamuomba Bwana Chewa Samuel

**Chewa Samuel:** Kwa jina naitwa Samwel Chewa kutoka Bamba. Kwa maoni yangu ninaunga mkono Serikali ya majimbo.

**Com. Abubakar Zein:** Nafikiri huyo Bwana anakuonya Samuel usije ukaanguka na hicho kiti.

**Chewa Samuel:** Serikali ya majimbo itarahisisha kazi, baina ya utawala. Kwa sababu nafikiri ingekuwa ni Serikali ya majimbo. Ofisi nyingi zngekuwa hapa hapa karibu nasi, hapa Pwani. Ukikuja wakati huu, ofisi zote kubwa kubwa ziko Nairobi. Ukitaka kuona mkubwa kama Rais haiwezekani. Kwa hivyo sheria zingine ni kama zile za kikoloni. Huwezi ukamuona Rais moja kwa moja hivi. Kwa hivyo sheria zingine zinastahili kuondolewa. Kama leo tumemwona Ghai, moja kwa moja huyu hapa. Je ingekuwa ni Rais ingekuwa hatuwezi kumuona,tungezuiliwa huko kwa Gate. Kwa hivyo vipengele vingine vinastahili kuondolewa. Tuwe tunaweza kumuona Rais na kumwambia shida zetu moja kwa moja.

Kuhusu pesa za mkoa yani jimbo ziwe zikikusanywa na kuwekewa katika Local Government. Seventy five per cent, yaani ile pesa itahitajika pale pale kwenye skuli, barabara ,halafu asilimia ishirini na tano iende kwa Serikali. Sina mengi yangu yalikuwa machache.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Chewa. Bwana Charo Katana? Samson Kahindi? Kahindi Karisa? Mangi Yaa yupo? William Pola? Ziro Wanje upo? karibu Bwana

**Ziro Wanje**: Asante sana kwa kupata nafasi hii. Mimi kwa majina naitwa Ziro Wanje. Jambo la kwanza mimi ninaunga mkono Serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo si kwamba ni kufukuza mtu pahali yuko ni kulingana na vile mambo yalivvyo kwa miaka arubaini na moja mpaka sasa. Majimbo mengine hasa sana kama Pwani, tunashida sana na kazi. Na hii ndio maana penginepo ikiwa kuna majimbo sisi pia tungeweza kupata nafasi za kazi au watoto wetu. Hili ni la kwanza.

Naenda sehemu ya pili. Elimu ya msingi iwe ya bure. Kwa sababu gani, sababu ni hii, mtoto husomeshwa na mzazi wake na hasa huwa wazazi wengi wameshaondoka duniani. Leo hii ikiwa elimu ya msingi ni pesa, tutabaki na magaidi wengi sana baada

ya sehemu sijazo au ya miaka itakayo fikia umri wa watoto wetu ambao tunaopata sasa.

Tatu, amri nyingine tena katika Katiba ambayo ni kali na najaribu kutoa maoni ya kuua. Hii amri ya kuua nafikri ni kali sana isipokuwa mtu akiwa ni mwizi, askari huyo afanye kazi yake kwa kumvunja mguu ili judge akaweze kufanya kazi hiyo yake ambayo amesha ajiriwa.

Jambo lingine la nne, ranch. Hizi ranches zinaleta vita kubwa na hata utengamano. Kwa sababu gani? Ni kwamba utakuta mtu ambaye hiyo sehemu ya ranch hakuna shamba lake na yeye ndiye ambaye anataka kumiliki hiyo shamba. Kwa hivyo ranch iweko ikiwa ni wale wale wenye shamba lile, lile.

Tano, uuaji kikatiba; mtu akiuwawa ikiwa hakujulikana x-ray iletwe mara moja mtu huyo asiondelewe mpaka ajulikane ni nani aliyemuua. Hii ndio itaweza kumaliza ugaidi. Hiyo ni tano.

Sita, akina mama; ulimwengu mzima akina mama waheshimiwe sana tena wao wenyewe wanajua hivyo. Kwanza ni shukrani sana ulimwengu mzima kama vile nilivyosema tena imejaa kwa sababu ya akina mama. Ingefaa akina mama hao, heshima kubwa kwao lakini nao pia wajaribu kuheshimu ndoa zao. Wanajionea wenyewe, sio wote lakini wengine hawaheshimu ndoa zao, ndio maana unaona sana wanalaliwa.

Jambo la saba; hospitali yoyote ambayo iko ya kiserikali, pawe na huduma tosha hasa za maghari. Kwa sababu kuna hospitali nyingine ambazo wakaguzi wako lakini watapeleka hapo mgonjwa na utapata mtu huyo wa kutoka saa moja hadi saa kumi na mbili ndio aweze kuaga dunia. Penginepo kama kungelikuwa kuna gari, angeweza kupelekwa mara moja badala ya masaa sita, angefika hospitali kubwa akapona hili pia lingekuwa ni jambo la maana kikatiba. Kwa hivyo, hayo ndiyo yaliyokuwa maoni yangu. Asanteni sana ndugu kwa kunisikiza.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Waje. Nina mwita sasa Bahati Sharif. Mary Josiah? Mwenda Katana? Ngongo Charo? Uko? Karibu Bwana Ngongo. Esther?

**Ngombo Charo:** *Asante ,ndimi Ngombo Charo, maoni gangu ni machache tu.*

**Bi. Esther:** His name is Ngombo Charo.

**Ngombo Charo:** *Ni muzee wa kijiji kisha ni mutu wa shukuli, mbomu wa shukuli kuko.*

**Bi. Esther:** He is an elder in the village and he is a head of a school there.

**Ngombo Charo:** *Kwa zhizho gangu mimi ni kwamba ni shida tu ya madzi ko Dodosa hata kuku Bamba ni zhizho.*

**Bi. Esther:** His main problem is the water problem there at Dodosa area

**NgomboCharo:** *Hiri , ni nzala kamare.*

**Bi. Esther:** Secondly, hunger

**Ngombo Charo:** *Hahu mimi ni muzee wa mudzi sihokera. Nahenza nisaidiwe zho nazho*

**Bi. Esther:** Thirdly, he is an elder in the village and he does not earn anything. He needs that to be considered.

**Ngombo Charo:** *Ni zhizho kare sina zaidi*

**Bi. Esther:** That's all he has. (Laughter and clapping)

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Ngombo. Najua limewafurahisha hilo. Lakini maoni ya Mzee tuyaheshimu kwasababu anazungumzia kuhusu utawala. Anasema ikiwa katika kiwango cha chini yeye ni Mzee wa mji na anafanya kazi hiyo, lakini halipwi chochote. Hayo ndiyo yalioyasema, tuyaheshimu, Asante. Ningependa kumuomba Mwemba Fred? Kombe Nzai? Fred wewe? Karibu Fred.

**Fred Mwemba:** Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia hii nafasi zote kuweza kuwa hapa pamoja tuweze kujadilina Katiba yetu ya Kenya. Mimi kwa majina ni Mwemba Fredrick kama vile mulivyoelezwa. Maoni yangu ya kwanza ni kwamba maoni haya yatekelezwe. Malalamiko kuhusu huu mjadiliano wa Katiba tayari yako. Watu tayari wanasema Katiba imeshatayarishwa lakini ni kwamba watu wamechukua fursa hii yakupatia watu mfano a au ishara ya kwamba wanashughulikia Katiba ya Kenya. Kwa hivyo itakuwa ni vyema zaidi maoni ya wananchi yaweze kutiliwa maanani na yaweze kutekelezwa.

Katika nchi yetu ya Kenya tumekuwa na kamati nyingi sana. Hata watu saa ingine wanasema nchi yetu ya Kenya ni kama ambayo inaongozwa na Kamati. It as if our country is being run by Commissions. There are so many and yet the results of the Commissions and meetings are not made public to the people. So it is my humble request that whatever we are discussing at this point here, let it be implemented for the benefit of our country Kenya.

Na pia tumesikika tu kwa vyombo vya habari kwamba kutakuwa na mjadala huu. Watu watakuwa wanakutana kuhusu kujadiliana Katiba na muda ambao tumepatiwa si mrefu sana ya kuruhusu watu wajitayarishe. Watu tutapata kwamba wengi

hawaelewi hii Katiba, tumeweza kushuhudia hapa kwamba watu wametoa malalamishi yao kuhusu haswa matatazo ambayo yamewakumba lakini si eti wanasema sheria fulani na fulani ni hivi na hivi inafaa ibadilishwe si hivyo. Kwa hivyo itakuwa vyema wakati au siku zijazo watu wapewe Katiba kabisa waweze kuzisoma na kuzielewa ili waweze kuchangia kabisa.

Ya tatu ni kwamba mamlaka ya Rais kuteua Mawaziri yasiwe yake ya kipekee. Itakuwa vyema ikiwa hizi nafasi zote kadhaa za wizara zitagawiwa kila mkoa. Isiwe kwamba mawaziri wengi wanatoka sehemu fulani ya nchi. Utapata kwamba kama Waziri ndio hao hao wa Bunge na ikiwa Rais atakuwa anateua Mawaziri kutoka sehemu fulani fulani basi itakuwa rahisi kwake kupitisha sheria ambaye yeye mwenyewe atakuwa anapendelea. Kwa hivyo itakuwa vyema Mikoa yote iweze kutoa Mawaziri na pia licha ya hiyo hao Mawaziri wote waweze kutoka kwa vyama mbali mbali. Isiwe tu ati kama ni Kanu peke yake. Chama ambacho Rais utapata kwamba yeye yuko katika hicho chama.

La nne ni kwamba tuwe na Regional au Provisional Development Fund. We should this Regional Provisional Development Fund for the purpose of financing local projects especially for youth groups. We also have so many projects which are not able to pick up because of lack of these funds. For example we have the Korosho Company in Kilifi. We all know that it was embezzled by well known Government officials and up to now nothing has been done concerning that. It is a very sad situation. So the Government should look into this issue. We have our Provinces like in Central, Rift Valley these are areas which are endowed with other resources like coffee, tea, but like in the case of Coast Province, our major resource that we can rely on are the National Reserves, Game Reserves, the Local Port but it is unfortunate that very little is being chanelled for the purpose of developing the local mwananchi or the region. So it is my humble request that not all the amount of money that is being generated from these authorities or these public funds should be chanelled to the National Treasury. No, I think a part need to be retained for the purpose of developing the local region.

Sixth, haya maoni ambayo tunaotoa katika mkutano huu yawe ni kila mara si wakati tu ambapo uchaguzi unakaribia. Watu watapata kwamba mara kwa mara, Serikali inachukua hatua ya kubembeleza au kufurahisha wananchi kusudi waweze kupata kura. Lakini itakuwa vyema zaidi kila mwaka au kila miaka miwili kuwe na mjadala kama huu tuweze kujua kama kweli hizi sheria walizitekeleza ama vipi au sheria fulani ilitufaidi ama nmana gani. Kwa hivyo itakuwa vyema namna hivyo. Si eti mara baada ya muda mrefu sana.

The seventh point, we should have the Government control basic human needs and staple food. If possible, the Government should also subsidise as in the case of health services with drugs. At the moment most of the services are being privitized and it is in this situation you find that most of the local people cannot afford their daily meal. A packet of Unga for example costs around thirty shillings which is just too high for somebody who has family of ten people to feed, that will not be enough even for lunch alone that cannot be enough and remember you have to cater for lunch, supper and probably breakfast. I call upon the Government to look into this issues. Very pressing services to the people should be met free. If not even free they should be subsidized.

The eighth point is that the Government spending is sometimes very extravagant at the expense of other services. For example we have very costly vehicles at the disposal of the Government officials. For example the Ministers. We have also this team which is going round the country. The vehicles which you are using consume a lot of fuel. There is so much demanded from the pockets of the tax payers. Other examples are the salaries paid to the Government officials,the Minisiters, the MPs, the lawyers which are just too high I think it is high time mwananchi should be considered. We have people like the police who are lowly paid and the services which they render to the people are commendable. I feel the salaries they earn are quite low and that is why they are temptediinto unbecoming behaviour like corruption in the case of traffic police.

**Com. Abubakar Zein:** Fred, muda wako umekwisha ungekuwa una summarize sasa.

**Fred Mwemba:** Okey imebaki mbili tu. Yes I think the salary of the police should be considered ,they are doing a good job.

Finally we should have centralization of services for the purpose of decreasing and improving the services to the Wananchi. This can be achieved by having majimbo in our country. We have for example in Nairobi very cheap equipment but when you come to Mombasa, similar equipment is so costly. So you wonder because most of them are imported and they pass through Mombasa get to Nairobi, from where they are despatched to other parts of the country. This is too costly to the mwananchi and it is a bureaucracy of its kind. So we have to look into this. That's all. Thank you.

**Com. Abubakar Zein:** Fred, napenda kushukuru sana lakini nataka usikie mambo mawili ni kuelezee. Tumeshauriana na mwenye kiti Prof. Ghai na anakubaliana na mambo haya nitakayo kuelezea. Fred kasema kwamba anahofia kuhusu maoni anayotoa na maoni yanatolewa leo na wanachi wengine jee yatadhiminiwa au itakuwa nikuchezeana shere? Anasema hivyo yeye. Na la pili anauliza kwamba kuna fununu kwamba Katiba imeshatayariswa haya ni mazungumzo tu tunafanya halafu baadaye tutawatolea Katiba tuseme ni hii ambayo ishatengenezwa. Tumeshauriana na Prof. Ghai na tutakupa mwelekeo wetu kama tume.

Kwanza sheria inatulazimu sisi kutilia manani kila neno linalosemwa hapa. Ndio maana tukawa tuna andika na kurekodi. Tuna rekodi kila neno. Na nyinyi mlioko hapa ni mashahidi kwamba fulani wa fulani kaja katoa maoni yake hapa. Sijui kama tunaelewana.

**Audience:** Ndio

**Com. Abubakar Zein:** Pili, ikishatolewa report itarudishwa kwenu muone yale yalioandikwa kwa report jee ni hayo tuliosema. Sawa sawa. La mwisho kumwambia, hakuna Katiba hiyo. Fununu hizo ni zile kawaida za Wakenyea za kuchangamsha akili. Sijui tunaelewana. Hakuna Katiba hiyo mimi nasema hivyo. Hakuna Katiba hiyo. Katiba tunaunda sasa.

Nyinyi mnatoa maoni, Kenya nzima inatoa maoni. Asante Bwana Fred.

**Fred Mwemba:** Asante nashukuru. Labada..

**Com. Abubakar Zein:** Ulisahau jambo. Haya malizia

**Fred Mwemba:** Now the recruitment of the civil servants including the forces should be equally and equitibly distributed. Ni kwamba utapata kabila fulani ndio wako wengi sana katika shirika fulani. Unapata police au jeshi wengi ni wa kabila fulani. Lakini unashndwa kwamba hawa Wakenya wengine kwani hawawezi kufanya kazi kama hawa wengine. Inakuwaje kabila fulani ndio inatawala ile kampuni. Kwa hivyo itakuwa ni vyema kama ni kuandika watu kazi iwe ni kila mahali katika nchi yetu ya Kenya. Kama ni jeshi au polisi, wawe wanazunguka. Lakini sio wanakuja kilifi na kuajiri polisi wawili wengine ni mmoja lakini unapata kule Central wanachukua wengi sana. Lakini sote tunatozwa hizo pesa kusudi tuweze kulipa mishahara ya hao watu..

**Com. Abubakar Zein:** Sawa sawa Fred. Tumefahamu. Asante, Fred ungeenda pale uandike register kwamba umetoa maoni. Na kama umeandika mambo, yawache pale. Kombe Nzai? Hayuko, Kahindi. Katana? Kahindi Ngowa? Kombe hatukupewa jina la pili. Limeandikwa Kombe tu wa kutoka Bamba. Zubeda Hassan? Kombe yuko? Hebu tupe jina la pili Kombe. Kuja kwenye microphone ndio liandikwe jina.

**Emmanuel Kombe:** Emmanuel Kombe. Mimi ningetoa maoni kidogo hapa kuhusu basic rights. Basic rights inamaanisha kuhusu elimu mwanzo na tungeomba elimu ya msingi iwe ya bure ili watoto wote waondoe ujinga. Kuwe na National schools na public Universities katika kila mkoa.

Kuhusu afya; napendekeza kuwe na kituo cha afya angalau kwa kila Sub-location. Kuhusu maji, Katiba itengenezwe ili angalau kila kwenye shule ya msingi, kuwe na kisima.

Pili ni wafanyi kazi wa Serikali, hapa ninagusia kuhusu machifu. Ningependekeza machifu wachaguliwe na raia wenyewe. Manaibu wa machifu waondolewe, badala yake kuwe na wazee wa vijiji kushughulikia masilahi ya wananchi kulingana na mila na desturi.

Tatu, haki za makundi mbali mbali; hapa nitagusia kuhusu wasichana. Wasichana wasilazimshwe kuolewa ili kupunguza kuvunjika kwa ndoa. Watu wanaotaka kuoana wafanye hivyo kupitia kwa wazee wa vijiji na kuweka sahihi ndoa yao katika ofisi ya chifu.

Nne kuhusu wajane; wajane wawe na haki ya urithi.

Tano, viwete wasomeshwe bure na Serikali na pia waandikwe kazi kama raia wengine.

Kuhusu mamlaka ya Rais; Rais asiwe na uwezo wa kuteua wafanyi kazi wa Serikali badala yake tume ya Bunge ifanye hivyo. Tume maalum kutoka Bunge iwe na uwezo huo kuteua wafanyi kazi wa Serikali kama vile ma Balozi, wakuu wa Ports hapa na kadhalika.

Rais lazima awe Mbunge. Rais, asiwe juu ya sheria. Yaani awe anaweza kushtakiwa akikaidi sheria kama vile huko Marekani.

Wabunge; wananchi wapewe uwezo wa kumkataa Mbunge wao hata kabla ya kipindi au vipindi vilivyo wekwa. Hii itahimiza uajibikaji wa wabunge wetu. Kusiwe na Wabunge wateule. Hawa huwa si chaguo la raia bali kwa upendeleo fulani.

Councillors; hawa wapewe mafunzo maalum ili wajue kazi yao kwa sababu utakuta wengi badala ya kufanya kazi ile ambayo pengine ina muhusu yeye, kazi yake ni kugombana na wafanyi kazi wa Serikali. Basi ikiwa italazimu wawepo wapewe mafunzo pengine kati ya miezi sita au miezi tisa hivi ili wajue wajibu wao. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Kombe. Andikisha register huko. Zubeda Hassan? Hayuko. Karisa Kahindi? Yuko? Karibu Bwana Karisa

**Karisa Kahindi:** Nashukuru sana kwa kupata wakati huu wa kuchangia Katiba hii yetu ya Kenya. Langu

**Com. Abubakar Zein:** Karisa? Taja jina lako kwenye microphone kwa sababu tuna record.

**Karisa Kahindi:** Jina langu naitwa Karisa Kahindi. Langu ni moja tu. Nachangia kuhusu Katiba hii ya Kenya iwe inaweza kutambulika kwa kila mwananchi baada ya utungaji huu wa Katiba hii. Katiba hii ya Kenya ikisha kamilika inatakikana iwe wazi wazi kwa kila raia na iweze kupunguza unyanyasaji na utoaji wa rushwa. Hii itaweza kusaidia pia kuchangia Katiba wakati ikiwa inahitajika kuvunjwa na kuundwa upya. Kwa mfano wakati huu tuko katika harakati ya kuunda Katiba lakini kuna wengi ambao hawajaelewa Katiba yenyewe ni nini. Iwapo tunaweza kujua Katiba ni nini, inaweza kuchangia sana kusaidia kuunda Katiba hii. Katika muundo huu wa Katiba, itaweza kusaidia haki za binadamu ikiwa mwananchi mwenyewe anajua sheria inamuhitaji afanye nini.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa Karisa. Tumefahamu kwamba unataka Katiba mpya watu wote wafunzwe wajue haki zao,Katiba mpya.

**Karisa Kahindi:** Kabisa

**Com. Abubakar Zein:** Unalingine?

**Karisa Kahindi:** Sina lingine.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Karisa. Ndugu Karisa, rudi hapa uandike kwenye register umetoa maoni. Ndugu Edward Mwaro? Alice J. Kiraga? Justine Karisa? Kizao? Ngoa Ziro? William Charo? Esther Karisa? Mary Katana? Mama ndio unaitwa mama Mary, basi kwa kuheshimu umri muache mama atoe yake halafu nitakuita.

**Mary Katana:** Kwa jina naitwa Mary Katana na nina maoni mawili tu. Oni la kwanza, ni naomba Katiba wakiketi tunajua Pwani ina watoto wengi ambao wame elimika na wanafanya kazi ofisi kubwa kubwa lakini badala ya wafanye kazi huku kwetu pwani wanapelekwa huku nchi za mbali na utakuta wakifika kule watu wengi wanafaidika wale ambao pengine hata kama ni kufagia tena wataajiri mtu huyo ambaye yuko mbali kabisa. Lakini naomba kama inawezekena au iwezekane wale wote ambao wanaweza kuketi ofisi hizi kubwa kubwa za huku kwetu pwani wawe wote watarudishwa huku kwetu Pwani ili watoto wetu wale ambao hawana kazi hata kama ni ya kufagia nao wakapate angalau riziki zao. Kwa hivyo maombi hayo nataka Katiba ifikirie sana kwa sababu watoto wetu wamesoma, hata kidato cha nne lakini hawana kazi. Wanatamani angalau kufagia. Angalau wamwagie maji maua. Lakini hawapati kwa sababu wengi walio elimika huku Pwani wanapelekwa huku nchi za mbali na wale wa mbali wakija huku, wana ajiri watu wao. Kwa hivyo jambo hili Katiba ifikirie sana, tena sana ili watoto wetu nao wakapate riziki.

Jambo lingine ninaomba nchi hii yetu hapa Bamba, location zetu hapa ni nne. Kwa hivyo naomba hospitali kwa kila location ili tupunguze magonjwa ya watoto na akina mama wakati wakujifungua, tupunguze hasara za akina mama na hasara za watoto na hata hasara za akina baba wasitembee muda mrefu kutafuta hospitali. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mama Mary. Mama Mary tafadhali andika jina lako pale kwamba umetoa maoni. Asante Mama Mary. Bi Esther sasa ni nafasi yako.

**Esther Karisa:** Kwa jina naitwa Esther Karisa maoni yangu haswa, jambo la kwanza ni kuwaunga mkono kuhusu Katiba. Jambo la kwanza kabisa ninaomba kama iwezekanavyo kuhusu maji. Sehemu hii yetu ya Bamba, ame umeendelea sana na ukame ni wazamani. Tulililia mfreji muda mrefu na kweli mfreji tumepata lakini maji inakuja kwa muda. Kama siku yoyote ambao kuna mkutano kama leo, kama ni wa DC kama ni wa DO pengine kutoka sehemu za nje a maji utayaona. Lakini kama ni wakati tu hakuna mgeni yeyote ambaye atafikia nchi hii yetu ya huku Bamba utakuta maji ni shida. Na hasa wakati huu kama vile jua ambavyo limeendelea hasa ukame umezidi ninaomba katika Katiba yetu hii kama inawezekena kukachimbwa bore holes. Nafikiri bore holes zikichimbwa wakati hakuna maji kwa mifereji lakini kuna bore holes zingetusaidia zaidi. Ninaomba

katika Katiba yetu, iungwe mkono katika hayo malalamishi ya upande wa maji.

Upande mwingine ni upande wa hospitali. Hospitali pia zimesemekana kwamba ni bure lakini tena kuna shida, kwa maana wakati una umwa na huna mapeni hapo unaona unapata shida. Unatakikana wewe mgonjwa uwe na pesa za kutoa kule ndipo upate matibabu. Ninaomba kama inawezekena hata hospitali zetu pia zingekuwa za bure.

Jambo lingine la tatu ni upande wa elimu. Upande wa elimu pia watoto wetu wanasurura wengi wakiwa hawana elimu. Hawana elimu ya kutosha kwa ajili ya matatizo ya kinyumbani na wengine hasa kama vile hata wenzangu wametangulia wamesema ya kwamba katika Katiba hii kufanywe uchunguzi maana wako wazazi wengine ambao wana wacha tu watoto wao wakisurura. Lakini kama hii Katiba itafanya uchunguzi juu ya Katiba nafikiri huu ugonjwa wa kukosa elimu ungekoma. Kwa hivyo nafikiri sina mengi zaidi ni hayo asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bi Esther. Tafadhali andika jina lako pale kwenye register. Asante. Bwana Karisa Nzai? Jonathana Kaingu? Lilian Mwakombe?Tsanga Kaingu? Kazungu Nyiro? Mzee karibu sana. Ikiwa ulikuwa umetoka nje kidogo na jina lako lilipita,unaweza kwenda kujitambulisha kwa yule Binti ukaangalia jina lako, halafu tutajua tutakufanya nini . Mzee karibu huku mbele. Mzee wangu taja jina lako.

**Kazungu Nyiro:** *Dzina rangu naifwa Kazungu wa Nyiro*

**Bi. Esther:** His name is Kazungu Nyiro

**Kazungu Nyiro:** *Mimi be na ahoho mario mana shoma*

**Bi. Esther:** He has kids who are in school

**Kazungu Nyiro:** *Vikara hariahu mino sina kitu babe yao naye kana kazi. Na ahoho Mario manashoma ahoho airi vikara mimi sina kitu na babe yao kana kazi.*

**Bi. Esther:** He doesn’t have money and their father does not have a job

**Kazungu Nyiro**: *Be zhenye were nahenza hii Katiba ahoho be mahalwe ni yo Katiba mashomeshwe. (laughing and clapping)*

**Bi. Esther:** He wants his children to be taken by the Constitution and be educated.

**Com. Abubakar Zein:** Ngojeni kidogo. Mzee wangu ? Mwambie Mzee angoje

**Bi. Esther:** Tafadhalini mpatieni nafasi

**Com. Abubakar Zein:** Tafadhalini mpeni mzee nafasi atoe maoni. Hata mimi nataka kujua jambo lililo wafurahisha nyinyi hata mimi nataka kujua. Ngojeni hata mimi nipate tafsiri.

**Bi. Esther:** Okey, he is saying that he has kids who are in school he is educating them but there is no money to educate them so he is asking the Constitution to educate the kids.

**Kazungu Nyiro:** *Kwa vizho sina manji bule mino ga kwangu ni gago ga hariau atite makale manda shomeshwa.*

**Bi. Esther:** He has no more. His major concern is that he wants those kids to be educated.

**Kazungu Nyiro:** *Sina zaidi gangu ni gago*

**Bi. Esther:** That's all he has.

**Com.Abubakar Zein:** Mwambie mzee nimesema asante sana. (laughter) Ngoja niwaambie jambo aliolosema Mzee sio jambo la kuchekesha, ni jambo la kufurahisha. Kwa nini? Ana haki mzee kusema Kikatiba iwe haki ya kimsingi watoto kupewa elimu ya bure. Anadai hivo yeye. Sawa?

**Audience:** Sawa

**Com. Abubakar Zein:** Haya. Anayefuatia ni Karisa Mwandonga. Karibu Bwana Karisa.

**Karisa Mwandonga:** Jina langu naitwa Karisa Mwandonga. Natoka Mitangani location, ni mzee wa kijiji. Katika Katiba ambayo inataka kuundwa sasa, ningependa sana haya mambo ya ardhi haswa hizi ranch tunapata wakati mwingine tunaweza kusema ni maonevu. Mtu unaishi mahari ambapo babu zako na baba zako walizikwa pale unakuja kuta wakati mwingine unaambiwa toka huna title deed hapa ni kwa fulani. Mtu ambaye ametoka mile nyingi kabisa aje akuondoe wewe, akae yeye. Hicho kitu ni chakusiktisha. Kwa hivyo ningeomba hii Katiba kama ingeweza kufikiria jambo hilo. Wale wanaohusika wakae karibu na sisi na wawe wakionana na wazee wale ambao wanaishi katika sehemu ile kupata maoni katika ardhi hii hapa ni kwa nani. Na mtu yule anayeishi pale alikaa pale kwa muda gani. Mpaka sasa leo aje aondolewe. Kwa mfano kama sasa mimi. Ni mzee nina miaka sitini karibu na nne hivi. Leo nije niambiwe niondoke mahari pale nilipozaliwa na ninaishi. Pale pale. Niwe sijui nitakwenda wapi. Hayo,Katiba ningeomba ifikirie sana jambo hilo. Hilo ndilo langu sina zaidi ni hayo hayo.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Karisa. Bwana Sirikali,karibu Bwana.

**Shikari Mkangi:** Mimi naitwa Shikari Kadenge Mkangi. Napenda hii Katiba yetu iangalie vile ambavyo nchi yetu imekumbwa na ukame. Inashida nyingi ambazo zimetatiza wananchi. Kwanza ni shida ya maji. Sasa hivi nafikiri kuna watu wengi ambao wana siku karibu nne hivi hawajala. Maanake shida ni ngumu sana. Kwa hivyo ningependa mfereji uwe karibu na sisi. Hospitali tupate na mambo ya shule tupate vile vile. Na mambo haya ya clinic za watoto pia tupatiwe vile vile. Nilikuwa sina mengi yangu ni hayo. Asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Shikari. Tafadhali andikisha jina lako pale kwenye register. Kijana ningeomba hapo usizibe njia hiyo maanake kuna watu wanapita wakiandika register hapo. Sasa ningemuomba mama Julia. Imeandikwa tu Mama Julia. Getrude Mwaeni? Karibu

**Getrude Mwaeni:** Kwa majina naitwa Getrude Mwaeni. Mimi sina mengi lakini nilitaka kugusia ya ule mzee ambaye alisema kuhusu watoto ambao hawana elimu. Wengine ni kama wale mayatima ambao hawana wazazi, wengine hawana kitu cha kujisaidia. Ningependelea kuomba ya kwamba hawa watoto wawe watasaidiwa na shule ya msaada. Wawe watasoma bure wale watoto ambao hawajiwezi.

Lingine ni kwamba, hawa watoto ambao hawajiwezi, kuna wale wavulana ambao wanaingilia masoma yao na kuwatia mimba halafu wanaacha masomo. Hao wavulana wanaendelea kusoma. Na hawa wazee wengine wanafanya kazi, wanaingilia pia hao wasichana. Halafu wanaacha masomo, wao wanaendelea na kazi zao wasichana wanaacha kusoma.

Lingine ni kwamba pia hao wazazi ambao wanaingilia wasichana wa shule. Wangekua wanachukuliwa hatua vikali sana kwasababu hao pengine wanasambaza haya magonjwa ya zinaa. Sina mengi yangu ni hayo tu.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Getrude. Kitsau Nzai, Kombe Hare,Karisa Charo? Karisa Charo yuko? Kazungu Kiraga? Mzee umesikia jina lako? Mzee wangu ndio Kitsau Nzai. Wacha Kitsau Nzai aje mberle kwanza. Kijana umesikia jina lako? Jina lako nani? Ushayatoa? Asante. Mzee wangu? Keti hapa Mzee.

**Kisau Nzai:** Jina langu naitwa Kitsau Nzai kutoka Ndigiria. Maoni yangu ni hivi; uongozi wa wenzangu kama mimi ningependa, mimi ni youth leader wa Ndigiria location, na ni Mzee wa kijiji wa sehemu hiyo ambayo ni Mwambani Sub-location. Maoni yangu na sema hivi, kuwe kuna kiwango kidogo cha sisi kupata kama usaidizi wa fedha maanake mambo ni magumu sana vile vilivyo.

Maoni yangu mengine tena, ningependa hivi ulinzi tunao lakini uongezeke tujue tunapata ulinzi mzuri ambao ni wa haki ndio

tunapenda sisi. Lingine tunataka bara bara zetu za mashambani ziwe nzuri yaani ziwekwe lami zote. Kitu kingine,hospitali ziko mbali mbali sana. Watu wanaumia sana. Naomba kwamba hospitali ziwe karibu karibu kama kuna mtu yuko na matatizo awe anaweza kupata usaidizi haraka.

Kitu kingine maji sehemu yetu ni shida sana, hata huu ukame ni sababu ya kwamba tunakosa mvua. Mvua ni mambo ya Mungu. Lakini ningependa mashamba yetu iwe na mifereji ya kunyunyuzia mimea yetu kwa mashamba hiyo itatusaidia. Sina zaidi ni hayo, kwa sababu na waachia wenzangu nao.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Anayefuatia ni Karisa Charo. Kama kuna mtu ametoa maoni yake akitajwa jina aseme tu ametoa maoni yale ya kuandika. Kazungu Kiraga? Kavumbi Kazungu? Shida Randu Nzai? Albert Mwaro? Karibu Mzee wangu.

**Albert Mwaro:** Mimi kwa jina naitwa Albert Mwaro Chenje. Natoa shukrani kwa kupata nafasi hii ya kutoa maoni yangu. Kwanza mimi napendekeza tuwe na Serikali ya majimbo. Kisha ninapendekeza hivi, watoto wote kutoka darasa la kwanza hadi la nane wapate elimu ya bure. Kisha ninapendekeza hivi tuwe na karatasi za kumiliki mashamba kila mtu. Na ninapendekeza kwamba mnazi, ulalishwe kwasababu ule ni mmea wetu wa Pwani tupate kufurahia.

Na ninapendekeza hivi, machifu wetu wote wawe watu wa kuchaguliwa na raia, siyo Serikali. Kisha ninapendekeza hivi kwamba, wale masub-hief wote wakae nje watolewe. Na ninaendelea kupendekeza kwamba viongozi wote wachaguliwe kutoka kule mtu amezaliwa. Ukiwa wewe ni Diwani wa sehemu hii usichaguliwe Ndigiria. Ikiwa wewe ni mzaliwa wa Bamba, uchaguliwe hapo Bamba sio uende uchaguliwe Mitangani. Ikiwa wewe ni wa kutoka Vitengeni uchaguliwe huko huko Vitengine, sio uje uchaguliwe Bamba. Hayo ni maoni yangu. Ikiwa wewe umezaliwa Mombasa, uchaguliwe kule kule Mombasa sio kuja kuchaguliwa huku kwetu Bamba. Hayo ni maoni yangu.

Pia vile vile napendekeza ya kwamba ulinzi uongezwe. Pia napendekeza kwamba muda wa Rais uwe wa vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Na pia vile vile ninapendekeza mayor na wenye viti wa miji wawe wakichaguliwa na raia. Itakuwa kazi ngumu lakini iwe hivyo hivyo. Kama vile wanavyochaguliwa wajumbe, vile wanavyo chaguwa hata Rais pia. Iwe hivyo hivyo. Pia vile vile ninapendekeza kwamba watu wa siasa wawe na muda wao wa miaka mitano mitano, isizidi na isipunguzwe. Pia vile vile napendekeza kwamba kuwe na uraia wa nchi moja. Uraia uwe wa nchi moja tu si uraia uwe wa nchi mbili.

Pia napendekeza kwamba mtoto akizaliwa na mama yake hajaolewa apate uraia. Pia vile vile napendekeza kwamba Katiba yetu hii tunayoiunda, iwe na ..

**Com. Abubakar Zein:** Mambo yamechacha mzee wangu. Yameisha?

**Albert Mwaro:** Yameisha. (Laughter)

**Com.Abubakar Zein:** Mzee Mwaro, usiende bila ku-sign register pale. Kama alivyo sema Professor Ghai tulipoanza ikiwa utambuka jambo sisi tushaondoka haina maana huwezi kutuletea. Ukae chini uliandike jambo hilo upeleke kwa mshirikishi ,District Coordinator. Ukipeleka litachukuliwa. Namuita Karisa Kalu? Karibu Mzee wangu.

**Karisa Kalu:** Mimi ni Karisa Kalu mzaliwa wa Bamba. Kwa hivyo ninaomba ukiwa unaunda Katiba jiheshimu kwanza wewe mwenyewe ndio ujue unafanya nini. Usiunde Katiba na wewe mwenyewe una wazimu. Ninataka uunde katiba na ujue mimi natoka wapi na ninaenda wapi. Kwa hivyo ombi langu kwa Katiba ninataka tuheshimiane usijaribu kunyanyasa mwenzako. Ujue chako ni chako cha mwenzio ni cha mwenzio. Ujijue hivyo. Kwa hivyo ninaomba mtu kama chifu, lazima asimamishwe kwenye msafara wa kupigiwa kura. Asingie tu kiholelaolela. Kumbe wengine hawakutaki wewe umevaa kirauni na watu wanachuki. Mtu kama DO, aende na kura maana yeye ni mwanadamu. Sio kunyanyasana, ukae na Katiba kwa roho safi. Si yule si mtaki na mumeunda Katiba. Hivi unaunda Katiba lakini unaunda adui wako, yule ndiye atakuzunguka wakati ukimukosea. Kwa hivyo kwa hii Katiba, atakae dharau cha mwenzake Katiba na imwangalie. Asiseme hii Katiba nimeunda tu hainifanyi kitu. Katiba umeiunda lakini inakuangalia wewe. Ukikosa unazungukwa na hiyo Katiba tu inakuweka korokoroni. Si unaidharau na umeiunda wewe. Kwa hivyo yangu siyo mingi ninaguzia tu vile vilivyo lakini haki ya Katiba ni kuangaliana na usione kijicho cha mwenzako Katiba yetu ikija tukae sawa. Na tuache kulaliana, sisi tumesoma wengine wamesoma kwa nini tunalaliwa. Tunataka sote twende sawa. Ukiwa wewe uko juu mimi nikiwa chini lakini iwe kisomo ni moja. Kwani mimi kule niliposoma sikufundishwa kujua? Kwa hivyo haifai. Katiba ni twendeni sawa. Ndio tutajenga Katiba kwa hali ya kisawa. Kwa hivyo sina mengi yangu ni hayo hayo. Lakini tuunde Katiba kwa roho safi.

**Com. Abubakar Zein:** Asante Mzee Kalu. Andika jina kwenye register Mzee Kalu asante. Changawa Mkamba? Karibu Mzee. Mzee Changawa, songeza microphone kwenye mdomo kidogo Mzee wangu. Hapo.

**Changawa Mkamba:** Naitwa Changawa Mkamba. Maoni yangu, nataka Katiba tuunde majimbo. Jambo la pili, mimi maoni yangu ninataka bara bara zetu zitengenezwe kwani zote ni mashimo matupu , hazitufai. Jambo la tatu, tunataka hospitali tuongezewe. Hizi hospitali zilizoko hapa, hazitoshi kabisa. Mtu analeta mgonjwa hapa, anaambiwa enda Kilifi. Pesa za kumpelekea hana. Unatafuta siku mbili, tatu hivi, huyu mgonjwa anashindwa anakufa. Kwa hivyo tunataka zile hospitali kubwa zilizoko kule ndani ndani ziletwe huku zitusaidie na sisi. Yangu ni hayo. Ni mimi Mzee Changawa Mkamba Kiti.

**Com.Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Kiti. Andika jina lako pale Mzee. Thomas Tabu?,Mkambu Kithi,Kazungu Nzai,wewe ndiye mzee Kazungu, karibu mzee wangu.

**Kazungu Nzai:** Asante sana kwa Katiba yetu. Tunataka iendelee kwa roho safi. Sisi tunashida moja.

**Com.Abubakar Zein:** Mzee wangu. Taja jina lako tulirecodi.

**Kazungu Nzai:** Jina langu ni Kazungu Nzai. Tunashida sisi ya watoto wetu, wamesoma kibarua hawana, wako hapa Bamba. Hapa kuna wazee wengine wamechaguliwa kufanya kazi na walianza kazi kitambo wame retire, wamerudishwa tena kwa kazi ambapo wanatudhulmu sisi hatutaki. Hayo ndio maoni yangu . Kazungu Nzai.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee wangu. Tafadhali andikisha jina pale. Aphonse Kaingu? Karibu Bwana Alphonse.

**Aphonse Kaingu:** Kwa majina naitwa Aphonse Kaingu. Kwanza ningetaka kutoa lawama kidogo kwasababu naona hii Katiba Wakenya wengi hawaifahamu na kuna jambo ambalo wanaharakishwa ili watoe Katiba pengine itakuwa hata haikuiva. Ninaona kwamba itakuwa makosa tukijumuisha Katiba na kura zinazo kuja. Mtu yeyote anaweza kutawala hii nchi lakini Katiba ni iwe ya maana ya kufaidi kila mwananchi. Kwa hivyo naona kuna hitilafu kidogo hapo. Tatizo kubwa ambalo tuko nalo hapa Kenya ni kwamba tumerundika uwezo mkubwa sana kwa ofisi moja kwa hivyo, kwa mtu mmoja. Hiyo ni hatari maanake uwezo huu mkubwa unaweza ukatumiwa vibaya. Kwa hivyo tukiweza kutoa ama kutawanya mamlaka haya ya ofisi hiyo kwa idara nyingine, nafikiri hatungekuwa hata na haja ya kugeuza Katiba wala kuwa na vyama vingi kwa sababu mamlaka yangelikuwa yanatumiwa kisawa sawa lakini kwa vile haviko hivyo, ndio kuna matatizo mengi.

Mimi kwa maoni yangu ningeliomba katiba ifuatayo. Ningeliomba Katiba inayotambua haki kama vile wimbo wataifa unavyosema, haki iwe ngao na mlinzi. Tuwe na Katiba ya majimbo, iwe ya mkoa, iwe ya nini, lakini iwe ni haki na mlinzi wa kila Mkenya, mtoto mchanga hata yule ambaye hajazaliwa awe na haki zake. Mzee awe na haki yake, kiwete awe na haki zake. Tukiwa tuna Katiba ya namna hii hatuna haja ya majimbo wala nini kwa sababu kila Mkenya atakuwa anapata haki yake.

Pili, tungelipenda Katiba ambayo inatambua wazee. Kuna wazee ambao wanazaidi ya miaka sabini. Na hatuwataji. Maskini pengine watoto wao hawana kazi, mzee naye anamiaka sabini si makosa yake kwamba watoto wake hawana kazi na mzee yule anaachwa anateseka. Kwa hivyo katiba ijayo iwe ambayo inatambua haki za wazee hasa wale ambao wanazaidi ya miaka sabini na tano ambao tukiwachunguza hawana lolote la kufanya. Hawana mbele wala nyuma.

Tungeliomba Katiba ambayo itaruhusu wanajeshi wetu ikiwa hatuko vitani wamekaa tu kambini, waweze kutumika kiserikalini ili kwamba wajaribu kutusaidia kwa miradi mbali mbali ambayo pengine Serikali ingetumia gharama kubwa kutafuta vibarua vya nje.

Tungeliomba Katiba ambayo inampatia Mkenya mmoja kazi moja. Kuna Mkenya mmoja anazaidi ya kazi ishirini na huku kuna vijana hawana kazi. Yeye ni mkuu wa idara fulani. Yeye tunaambiwa yuko hivi mara yuko hivi. Mkenya mmoja kazi

moja ili kwamba zile kazi zingine zichukuliwe na Wakenya wengine ambao hawana kazi. Kwa nini unarundika kazi nyingi kwa mtu mmoja.

Tungeliomba Katiba ambayo inaampa mamlaka mwananchi. Kwa mfano, hivi kuna njia ya Bamba, Mariakani, inatiwa murram. Si murram inayotiwa, ni mawe. Na hatuna uwezo wa kusema hatuyataki hayo kwa sababu amri imetoka juu. Kwa nini raia wasipewe mamlaka kwamba jambo ni baya na wanaona ni baya kwa macho yao,waweze kulikataa na likubaliwe kwamba halifai.

Ningeliomba Katiba ambayo, muajiri hawezi kuwa mwajiriwa. Kwa mfano Wabunge wetu walikaa tu dakika tano wakajipitishia mishahara mikubwa kwa sababu wao ndio waliokata shauri. Kwa nini walijipatia mishahara yao wenyewe. Wanoakena hao ni waajiri, tena ni waajiriwa. Hiyo Katiba inayokuja isilete kipengele kama hicho. Wawe wanaweza kupangiwa mishahara na kundi fulani, sio wao wenyewe wajikatie. Kwa maana tunaona kwamba wao walijikatia na hawataki kuwakatia wenzao. Kwa nini?

Tunaomba Katiba ifafanue hali ya kiwanda, agent, wholesaler na retailer. Siku hizi ni kwamba huyu agent ndio wholesaler, tena ndio retailer, kwa hivyo kazi hawezi kuirundika peke yake kwa nini sizigawanywe kama wakati wa hayati Mzee Jomo Kenyatta. Ilikuwa wholesaler ni wholesaler peke yake, retailer ni retailer peke yake na agent ni agent peke yake. Lakini siku hizi jamaa wamejirundika kazi hizo zote. Wananyanyasa wengine. Kwa hivyo wanakata bei na wanatuumiza.

Ningeliomba Katiba ambaye itachukua ule mwongozo wa kwanza. Maanake Katiba ya kwanza nikikumbuka vizuri sana ilikuwa inasema tunajipatia uhuru ili tuondoe ujinga, tuondoe magonjwa na tuondoe umaskini. Lakini tunaona mambo haya hayako. Maskini anaendelea kuwa maskini na tajiri anazidi kuwa tajiri. Kweli Katiba hiyo ningelitaka iwe ya haki. Umaskini tujaribu kuuondoa.

La mwisho, ningelipenda Katiba ambayo itatoa mwongozo ya kwamba unaweza kupanda bila kungoja mtu fulani kukutangazia kwamba umepanda. Kwa mfano nitachukuwa Mombasa Municipal Council. Mombasa Municipal Council ilikuwa inahitaji kuwa jiji kitambo sana lakini kwa sababu Katiba ya sasa inampa uwezo mtu mmoja tu mtu asema na iwe city ndio inachukuwa miaka mingi hata Kisumu ikawa city kabla Mombasa kuwa city. Kwanini tusiweke sheria kwamba town ikifika kiwango hiki, basi iwe city mara moja badala ya kungojea mtu. Hata kama ni promotion kwa nini mtu, kwa mfano mwalimu atoke na grade ya PI basi anakuwa PI mpaka baada ya miaka ishirini na mitano kwa sababu mtu hajasema apandishwe cheo. Nafikiri tungelikuwa na Katiba ya progression ukipanda, unapanda na kupanda hadi vile unavyoweza kufanya kazi. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Aphonse. Tafadhali andika jina kwenye register. Lonso Benjamin? Karibu

**Lonso Benjamin:** Kwa majina naitwa Lonso Benjamin Kaliki. Mimi nitachangia kuhusu Katiba hii. Kwanza nitaanza na haki

za kimsingi. Katika haki za kimsingi wengi waliokuja hapa waliochangia kuhusu Katiba hii ama kipengele hicho wamegusia elimu. Elimu iwe ya bure. Mimi naongezea elimu iwe ya lazima. Elimu ya msingi iwe ya lazima. Watoto wengi wako mitaani wana randa randa. Hawajasoma hata darasa la kwanza. Kwa hivyo elimu iwe ya bure.

Pili, nataka nizungumzie kuhusu mamlaka ya Rais. Wakati wa kuteua chairmen wa parastatals, Managing Directors na Minisiters. Unakuta kwamba Rais yuko na powers ama is above the law. Kwa hivyo atateua mtu ambaye anamtaka hata kama haja qualify kwenye hiyo department lakini yuko uwezo wa kumpa hicho cheo na atakaa hapo.

La tatu, nataka ni zungumzie kuhusu vyama vya kisiasa. Mimi ninaonelewa vyama vya kisiasa viwe vinne tu. Na kila chama kitoe pesa kutoka kwa miradi yao zisitoke kwa Serikali. Kwa sababu Serikali ina matumizi mengi sana. Ikiwa pesa za chama zitafanyia mambo ya kura, uchaguzi wa chama na mambo mengine, basi itabidi sasa mambo mengine yaachwe ili chama kifanyiwe uchaguzi wake.

La nne ni kuhusu kura. Pengine ufikapo mwezi wa kumi na mbili tunataraji kuchagua Wabunge na Councillors. Kuna sheria katika Constitution ambayo inasema Mbunge ni awe anajua kusoma na kuandika. Si kusoma tu na kuandika bali awe ana kiwango cha elimu ya form four. Na councillors pia wawe ni wa kiwango cha form four.

Lingine ni mamlaka ya korti; Our courts zimekuwa very reluctant hasa kusuluhlisha kesi za corruption. Katika vyombo vya habari tunasikia mara nyingi sana fulani anashtumiwa kwa kuiba ama kupora shirika kiwango fulani cha pesa. Na kesi hiyo unaisikia siku moja na itamaliza miaka ndio uisikie tena. Ama kiongozi mmoja fulani ambaye anauwezo ana hijack ile kesi ndiyo yale yanaisha. Yule ambaye amefanya ule ufisadi anasemehewa kwa sababu yuko na godfather. Kwa hivyo tuangalie korti halina mamlaka isipokuwa ni viongozi ndio wako na mamlaka. Majudge hawawezi kufanya kazi yao sawa sawa. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Subiri kidogo ndugu yangu tafadhali. Ulisema tuwe na vyama vinne peke yake vya kisiasa. Tutaviteua vipi vyama hivyo?

**Lonso Benjamin:** Vyama hivyo, tunaweza kuviteua namna hii, tuta vipigia kura. Kwa hivi sasa kuna vyama karibu arobaini, hivi vyama vitapigiwa kura na vine ndivyo vitakavyo chaguliwa kuwa vyama vya kitaifa..

**Com. Abubakar Zein:** Sawa asante. Asante sana. Tafadhali andikisha kwenye register. Jonathan Jefwa? Karibu

**Jonathan Jefwa:** Kwa majina ninaitwa Jonathan Jefwa natoka sehemu ya Bamba. Ningetaka kuchangia Katiba hii inayoundwa kwa mambo yafuatayo. Kwanza kabisa Serikali inayokuja ningependelea iwe ya majimbo kwa sababu wakati tuna Serikali kama hi,i rasilmali nyingi zinapotokana na jimbo fulani huwa zinabaki pale, kwa hivyo utakuta sehemu hiyo itachakuwa rasilmali hizo na ifanyie miradi yake pale.

Sehemu ya pili ni uraia. Uraia tunajua wazi kwamba vitambulisho tunapeana lakini hata hivyo kuna sehemu moja ambayo ina matatizo, ya ma title deeds na umilikaji wa mashamba. Hii napendelea kuwa, wakati unachukuwa kitambulisho pia uwe unawezo wa kupewa title deed ya pale mahali unapoishi.

Sehemu ingine ya tatu, hapa mara nyingine utakuta mambo vile yalivyo katika Kenya hii kwa sasa wale ambao ni matajiri wanapanga na wale maskini wanazidi kudidimia chini. Ndio maana unakuta mara nyingine watu wanapambana na kesi, yule mkubwa anaambiwa ameshinda na yule ambaye ni mdhaifu lakini ana ukweli anaambiwa hakushinda. Kwa hivyo hapo pia Katiba ifanye mambo ya kurekebisha sehemu kama hiyo.

Muundo wa Rais naonelea vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Halafu kuna kesi nyingine ambayo ni ya watu wazee, vikongwe. Kuna vikongwe haviwezi tena kushughulika na kujipatia riziki yao, kwa hivyo watu hawa ningeonelea Serikali inayokuja iwafanyie mpango ili watu hawa waweze kutunzwa vizuri mpaka wafikie wakati ule Mungu atakapo wachukua. Hii pia inakwenda sambamba na watoto mayatima ambao pia wanahitaji utunzi kama huo.

Pia nagusia upande wa elimu. Elimu yetu inatakikana ya msingi haswa nitaungana mkon na wenzangu ambao wamesema iwe ya lazima na ya bure, kuanzia darasa la kwanza mpaka la nane Kuwe na mpango ya elimu kwamba watakapotoka darasa la nane kusiwe na hali ya kuwa wale waachwe na wengine waende. Hii inaleta ukoroa maanake wale walioachwa nyuma wengine wanakuwa wakora. Lakini akiingia elimu ya upili itamuezesha kujipatia chakula chake. Na ikifika hapo sina zaidi. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Jefwa. Tafadhali andika jina. Sasa ningependa kumuita Daniel Baya ambaye ni mwanakamati wa 3 Cs. Tafadhali Daniel

**Daniel Baya:** Mimi natoa mapendekezo ya wanakamati la eneo la uakilishaji Bungeni la Ganze. Wanakamati hao ni kumi. Mwanakamati wa kwanza akiwa ni Mheshimiwa Bwana Katana Ngala. Wa pili ni Councillor Susan Biria, wa tatu ni Bwana Alfred Masha wa nne, Karisa Masha, wa tano ni James Kitsao Philip, wa sita ni Ruth Mramba, wa saba ni Martha Salama, wa nane ni Joseph Chengo Maro, wa tisa ni William Pola Mumba na wa kumi ni District Coordinator Bwana Daniel Mwaringa.

Mapendekezo ni kama yafuatayo. Kwanza muundo wa Serikali uwe ule ule wa kiungo cha kati ambako kutakuwa na Rais anayechaguliwa kama ilivyoko sasa. Makamu wa Rais wawe wanatoka kila eneo kubwa linalo wakilisha kama vile ni Province. Halafu kuwe na waziri mkuu mmoja ambaye atachaguliwa na Wabunge, ambaye ndiye atakuwa anashughulikia mambo ya Serikali Bungeni. Awe na wanachini wake wawili ambao pia watachaguliwa na waheshimiwa tuliowachaguwa waende Bungeni. Baraza la mawaziri litachaguliwa na Rais.

Sehemu ya pili; nguvu za eneo letu ambalo ni kama mabaraza yatasimamiwa na mayor kama ilivyo kawaida na awe amefika

angalau kidato cha nne. Councillor wetu wanaochaguliwa kama ni kiwango cha chini kabisa cha elimu basi iwe angalau darasa la nane. Hatuwezi kusema lazima form four kwa sababu watu wetu wengi wanapenda watu wa mashinani wawahudumie na wengi hawakusoma. Na hao wote wakae katika ofisi kwa muda wa miaka mitano peke yake.

Kipengele cha tatu ni vyama vya kisiasa. Kuwe na vyama vya kisisasa vingi, democracia hiyo iendelee kudimishwa katika nchi hii yetu. Vyama vya kisiasa visajiliwe vile ambavyo havikiuki kanuni na haki za watu ambavyo havina fujo, ambavyo ni vitulivu kwa maongozi. Vyama ambavyo ni vya kikabila vitupiliwe nje visisajiriwe maana vina hatarisha maisha ya wananchi.

Sehemu ya nne, ni ile tume ya uchaguzi. Electoral Commission ipewe mamlaka makubwa kuweza kutengeneza shughuli za uchaguzi kipeke yake bila kuingiliwa na kipengele chochote. Siku ile ya kuchaguana, siku ya kula, iwe gazetted mpaka public holiday ili watu wote wanaofanya kazi wapewe fursa ya kwenda kupiga kura. Usalama wakati wa uchaguzi. Tume hii ya uchaguzi ipewe usalama wa kutosha, ipewe ma afisa ambao watalinda watu kusiwe na mambo ya ghasia wakati wa uchaguzi ambao watu wengine maisha yao pia wanapoteza.

Kipengele cha tano ni kuhusu ardhi. Ardhi yetu hii lile eneo letu ambao litakuwa lina uwezo ardhi iwe chini ya mamlaka ya eneo letu ili eneo hili ambalo litakuwa na viongozi, wawe wana uweze wa kutoa title deeds kwa mtu ambaye amekaa mahali kwa muda wa miaka miwili na kuendelea. Na zile procedures za kupata title deeds, yale masharti, yawe nafuu kwa watu wetu. Wawe wanaweza kuzipata pasiwe na shida nyingi kupata title deeds na pia fee yake , iwe ambayo mtu wa kadiri anaweza kujimudu kupata.

La sita ni elimu; elimu yetu hasa ya msingi iwe ya lazima na ya bure. Kusiwe na mambo madogo madogo ambayo watu wetu hawawezi kujimudu kulipa. Tuhakikishe watoto wote wanasoma na kama watoto hawapelekwi shule, kuwe na viongozi kama vile DO na ma Chifu, wawe wanaweza kuhakikisha kuingia mji kwa mji kuhakikisha watoto wote wanafikishwa shule. Hiyo ndiyo elimu ya msingi, iwe ya bure na iwe ya lazima.

Halafu tunasema lika eneo lile ambalo litakuwa linawakilishwa kuwe na university moja. Angalu university zisikae huko Nairobi zote. Kila eneo kama hili eneo la Pwani liwe na angalau chuo kikuu kimoja. Kama ni ya Western kuwe na chuo kikuu kimoja. Kama ni ya Nairobi kuwe na chuo kikuu kimoja. Kila mahali namna hiyo.

Kuhusu uajiri, employment ,wakubwa wa mashirika ya kiserikali, parastatals na haya mashirika ya kibinafsi na ambayo si ya kiserikali angalau kila eneo liwe lina ajiri watu asilimia themanini na tano ya watu wakutoka sehemu hiyo. Si watu wakutoka pwani wanachukuwa wawili na watu wakutoka mahali pengine ndio wengi, isiwe namna hiyo tusaidie watu wetu. Wale ambao watakuwa wakutoka sehemu hiyo.

Sehemu ya nane ni kuhusu dini na mila zetu. Kuna dini zingine ambazo si nzuri zinahatarisha maisha ya wananchi. Dini kama hizi

tunasema hiyo Katiba ijayo iwe na kipengele kwamba dini ambayo itakayohatarisha maisha ya wananchi, isiweko iwe banned kabisa. Kwa sababu zingine zinakataza watu hata kwenda shule wanasema Yesu Kristo anakuja mwaka ujao. Dini kama hizo zisiruhusiwe kwa sababu zinaregesha maendeleo nyuma. Dini inayofaa na inamanufaa kwa jamii idumishwe.

Mila ambayo imepitwa na wakati, kama kule kuridhi wanawake,kwenye desturi zetu, mila kama hizo hasa wakati huu wa ukimwi, zifutiliwe mbali kabisa zisiweko, kwa sababu zinahatarisha maisha yetu.

Kipengele cha tisa ni kuhusu afya. Katiba hiyo mpya iwe na kipengele kitakachokipatia Serikali yetu auwezo angalau baada ya kila kilometre tatu kuwe na dispensary with a maternity wing ya kusaidia akina mama ambao wanakufa hata kabla ya kufika hospitali kwa matatizo ambayo yana husu uzazi.

Halafu, hawa watu wetu ambao wanafanya kazi katika hospitali za uma wanauwezo mkubwa wa kufungua clinic. Sasa yeye badala ya akae kule kuhudumia wananchi, anaenda 24 hours kufanya kazi katika clinic yake. Mtu yoyote anaye shirikia hospitali ya umma awe anafungika mkono kabisa, awe hana uwezo wa kufungua clinic ya nje maana tumesikia hizi kesi nyingi za madawa kutoka hospitali za umma zinapotea. Na madawa haya ni yetu sisi wananchi tukienda katika hospitali pengine ya Bamba au ya Ganze,iko hospitali lakini hakuna madawa na watu wetu hawazi kujimudu. Kwa hivyo yeyote ambaye anafanya kazi kwa hospitali ya Serikali kuwe na kipengere katika Katiba mpya ambacho kitamfunga asifanye private practice awe anafanya kazi hospitali ya umma. Na kama anataka kufanya private practice a resign kule afanye kazi private sector. Kwa hivyo watu wetu hii mambo ya madawa kuibiwa kwenye hospitali isiwepo na vifaa vingine viwe vya kuhudumia watu wetu.

Sehemu ya kumi, hili eneo ambalo litakuwa linasimamia liwe ni sehemu ya Pwani ama Western, liwe linapewa uwezo mkubwa kutoka kwa Serikali yetu hii kuu, ili kila angalau mwananchi baada ya kilometre tatu au tano kuwe kuna mfereji anaweza kupata maji, access to piped clean water. Yasiwe ya chini, iwe tunaweza kupata maji mazuri sijui Katiba hiyo itabadilishwa vipi lakini angalau mwananchi wa kawaida aweze kupata maji asante.

**Com.Abubakar Zein:** Asante sana Daniel Baya. Sijui Mheshimiwa kuna kitu ulikuwa unataka kuongezea.

**Hon.Noah Katana Ngala (Minister for Labour):** (Inaudible) Kwa hivyo nawashukuru kwa kujituma kuja hapa ili tuje tutoe maoni yetu. Basi mwenye kiti wa mkao huu kwanza nataka ni kukaribishe hapa katika sehemu ya Bamba. Tunashukuru sana kwamba ulikumbari uje hapa uje wewe mwenyewe halisi kuendesha mpango wa leo wa kusikiza maoni ya raia kulingana na taratibu ambazo ofisi yako imepanga. Kwa hivyo tunasema ni asante sana kwako kufika ni heshima kubwa sana ambayo umetupatia sisi watu wa sehemu hii ya tarafa ya Bamba na haswa zaidi katika kiti cha kuwakilisha cha Bungeni cha Ganze kwamba tumempata mwenye kiti mwenyewe wa tume hii ambayo imesikika kwa mda mrefu kuja hapa na kuja kuketi nasi siku nzima akitusikiza tukitoa maoni. Kwa hivyo tunakushukuru sana Professor Ghai kwa heshima kubwa uliotupatia. Na mshukuru pia Commissioner aliyekuja naye ambaye anayetuendesha katika mpango wa leo na wote ambao wamekuja katika kuhakikisha

kwamba siku ya leo Bamba  katika siku hii ya leo.

Tumengoja kwa hamu mambo haya ya Katiba na urekebishaji  wake katika nchi hii yetu ya Kenya kwa hivyo ni furaha kubwa na pia ni pongezi sana kubwa kwa Serikali pamoja na tume kutoa fursa hii kwa raia wake,wa nchi hii waweze kuwa na nafasi ya kuweza kutoa maoni yao na waweze wenyewe kusikika wakisema wenyewe bila kutishwa, bila kutiwa uoga wowote, jambo hili ni muhimu, uhuru huu ambao tunao siku ya leo ni uhuru ambao una maana kwa sababu tutakuwa tunajua kwamba Katiba itakapo undwa na sisi kama raia wa nchi hii tutakuwa tumeichangia kiasi fulani katika wakati huo.  Kwa hivyo tunasema ni shukrani kubwa.

Mimi nimesimama tu nijaribu kuunga mkono maoni yaliotolewa na yule ambaye amezungumza kwa niaba ya kamati ile ambayo iliteuliwa ya Bunge. Nafikiri tunataka tu tughusie maneno mawili matatu katika  msururu ule aliosema.  Lakini kwa jumla tunaunga mkono yale yaliosema na mengine ambao yaliosemwa hapa tuna furahia sana jinsi mnavyo changia agenda ya leo ya kurekebisha Katiba.  Kwa hivyo napenda muendelee na muyo huo huo katika hali ya kutoa maoni yenu.

Katika muudo wa Serikali nafikiri mmekuwa na mazungumzo mengi tangu mjadara huu uanze wa Katiba vile ambavyo ilikuwa inatakikana ifanyike. Katika yale ambayo tumeyasikia natuliyopanga katika muundo wa Serikali tunataka mamlaka mengi katika Serikali yapelekwe mashinani katika ule muundo wa Serikali pengine Katiba ya kesho itaupanga kule na Serikali ya kiungo cha kati lakini uwezo mkubwa upewe watu wa mashinani.  Maana hao ndio ambao wanaweza kukata uamuzi mambo yao, ndio ambao wanaweza kuketi na  wakazungumza na kuweza kujipangia maendeleo yao.  Kwa hiyvo hali hiyo itaweza kuhakikisha ule uhuru kamili, ya kwamba uwezo unapewa na unaweza kujiendesha mwenyewe katika mambo hayo.

Tunapendezwa ni kwamba, katika msemo uliosemwa hivi sasa kuwe na Rais wa nchi. Rais wa nchi awepo katika muundo wa Serikali awe ndiye kichwa wa hiyo Serikali.  Tunataka pia kuwe na makamu wa Rais katika muundo tunaozungumza na pia kuwe na waziri mkuu katika muundo wa Serikali tunayoizungumza.  Na yeye waziri mkuu apatiwe wasaidizi watakao mzaidia. Mambo ya Serikali yote usimamizi wake, uendeshaji wake uwe chini ya mkono wa waziri mkuu.  Awe ndiye mwenye kusimamia na kuangalia usimamizi wa Serikali.  Rais atakuwa yuko na uwezo fulani atakaokuwa amepewa na Katiba ili na yeye pia ajisikie kwamba anahusishwa na usimamizi wa Serikali iliyopo.  Kwa mfano pengine anaweza kuwa ni mwenye kuchagua mabalozi, ni mwenye kuchagua watu fulani, atapewa sheria fulani.  Makamu wa Rais naye atakuwa anazaidia pale ambapo sheria itakuwa ime mweleza aweze kuhudumu. Kwa hivyo nafikiri kitu muhimu katika hii Katiba ijapokuwa kuna mengine mengi, ni kujaribu kupunguza na kutoa nguvu zisiwe katikati zote, lakini ziweze kuteremshwa na ziweze kutawanywa hapa na pale ili ule usimamizi na uendeshaji wa Serikali uweze kusikika kwamba umegawanyika kisawasa.  Huo ni muundo wa Serikali jinsi ambavyo tunauona.

Mawaziri watakuwepo wachaguliwe na Rais na waziri wazaidizi na yale yote yakawaida. Huo ni muundo ambao utakuweko. Lakini uwezo mkubwa uweze kwenda katika chini na uwezo huu tunafikiria ungefaa uweze kuwekwa chini ya Serikali za mitaa.

Serikali za mitaa ndio zile za chini ambazo ziko kwenye sehemu za mashinani. Na watu wengi wako katika sehemu hizo wanaishi katika miji huko chini. Kwa hivyo wakiwa wamepewa mamlaka mazuri ya uwezo wa kuendesha mambo yao tunaona itakuwa inasaidia wale raia kuweza kukata uamuzi mambo yao wakiunganishwa kidogo katika sehemu za juu na labda wizara ambayo itakuwa inaangalia mambo hayo ya Serikali za mitaa. Lakini kuwe na uwezo mkubwa wa kuweza kusimamia mambo katika hali ya usimamizi wa mambo haya. Kwa hivyo Serikali za mitaa ni muhimu. Zinatakikana zipewe nguvu zaidi na ndio sasa mambo ya kule kupewa nguvu ndio kunazungumzwa sasa hata mambo ya wale watakaochaguliwa wawe watu wa aina gani. Maana akipewa nguvu wale ambao watachaguliwa ni lazima wawe ni watu ambao pia wanaweza kusimama na kuketi na kuzingatia mambo kulingana na uwezo mkubwa ambao watakuwa wamepewa. Kwa hivyo haya mambo ya Serikali za mitaa ni muhimu katika uongozi wa Serikali ili ionekane inahusisha raia wake katika hali ya kisawasawa. Kwa hivyo hizo ni sehemu muhimu katika Katiba yoyote.

Ni lazima tuhakikishe kwamba haki za raia zina heshimiwa. Katiba yeyote itakayo udwa isipokuwa na kuheshimu haki za raia itakuwa ni Katiba ambayo imepungikiwa sana. Na lazima raia na sisi sote tuhakikishe Katiba itakayo kuwa kesho ni Katiba ambayo itakuwa inarinda masilahi ya watu. Inahakikisha usalama wa raia katika nchi hiyo. Inahakiksha kwamba anaheshimiwa na haki zake. Na haki ni kama hizi ambazo tumezitaja hata za mashamba. Haki za mambo mengine, haki za elimu, hiyo Katiba lazima iwe itaweza kuweka ndani yake vitu ambavyo vitasomwa hapa Kenya na pengine popote, raia ataonekana kwamba amepangiwa mambo hayo na amegawanyiwa sawa katika mambo ya nchi yake. Kwa hivyo Katiba ambayo itakuwa haizingatii mambo haya ya kuheshimu haki za mtu itakuwa si Katiba ambayo itatufaa. Kwa hivyo lazima tuhakikishe kwamba Katiba ambaye tutakuwa tunaitaka sisi, haki za raiai zinaheshimiwa, zinadumishwa. Na hizo ndizo ambazo tumesema kwamba tunataka mambo ya ardhi wametaja yule msemaji alikuwa ametaja, mambo ya ardhi ni haki moja yao. Haki ile ya ardhi, mipango yake ni sehemu muhimu, tunafahamu sheria zinataka kuunganishwa sasa ziwe hazitakuwa sheria nyingi katika kitabu cha sheria za mashamba. Kwa hivyo tunataraji wale ambao watakuwa wanazungumza na sisi tukiwa tuko hapa tunachangia agenda ya ardhi tuwe tunahakikisha kwamba haki za kila raia katika upande wa ardhi zitazingatiwa vilivyo. Kwa hivyo katika hali hii tuliyo hivi sasa yale mengine yote ambayo yamesemwa katika kile kikaratasi ambacho baadaye tutakitoa kwa mwenye kiti hapa itakuwa ni mwongozo wa maoni yetu vile ambavyo tumeona. Tumetaja sehemu kadha wa kadha.

Elimu lazima iwe ndani ya Katiba. Hakuna taifa itakalo jengeka ikiwa watu wake hawakusoma. Hakuna jamii itakaye jengeka ikiwa watu wake hawakusoma. Kwa hivyo ni lazima na sisi katika ile haki ya kuchangia Katiba tuhakikishe kwamba kwa lazima vile na kwa njia yoyote ile, tunahakikisha elimu tunawapa watu wetu na iwe inaweza kuwa katika sehemu za sheria za Katiba kwamba elimu lazima kila mtoto apewe katika nchi hii. Kama ilivyo sasa. Isifutwe katika Katiba ijayo. Izidi kudumishwa na ihakikishe kwamba sisi pia watoto wetu watapata nafasi ya kuelemishwa na ambaye hatakuwa anaelimisha achukuliwe ile hatua ambayo inafaa. Viwe viko dani katika sheria. Kwa sababu tusipofanya hivyo huenda tukawa nakupungukiwa sana katika hali ya kielimu.

Kwa hivyo katika hali hii ya maneno ambayo tumeyazungumza yaliotajwa hapa mimi nilikuwa nasimama sitaki kuchukuwa

wakati mwingi nataka raia waseme maoni mengi zaidi lakini mfumo wa Serikali tunaotaka uwe wa namna hiyo, Rais yuko pale, Vice President yuko pale, Waziri mkuu huko pale, mawaziri wachaguliwe, kila mtu na kazi yake. Uwezo mkubwa uende katika Serikali za mitaa na uangaliwe huko uwe unaweza kuwa na nguvu za kuzaidia. Ardhi iwe ni moja ya zile muhimu katika hali ya vile ambavyo itaweza kuangalia Katiba katika ardhi zinaweza kuangaliwa vipi. Zinaweza zikawa ziko kivipi kwa raia wanao husika. Wengine wametaja watu wanakaa muda mrefu, wanakuja wanaondelewa na mambo kama hayo. Hii haki hii huwa inapunja wengine katika hali hii. Kwa hivyo ikiwa kutakuwa na uwezo wa kwamba ardhi imewekwa katika sheria zinazofaa itakuwa inasaidia. Kwa hivyo nimechangia kidogo kwa mambo ya ardhi lakini sitaki kuzungumza kiasi cha kwamba niwe ninazungumza kupita kazi ya tume ambayo imeundwa ya Serikali ambayo imefanya ya kuzunguka ama iliozunguka na kuweza kuangalia ni vipi sheria za ardhi zitakavyo faa. Kwa hivyo sitaki kuzungumza kiasi ya kwamba niwe ninatoa maanani kama waziri wa ardhi na makao. Mambo ya tume ambao iliudwa na Serikali, lakini natoa maoni ya kwamba ardhi ni muhimu watu walipigania uhuru na ardhi ni kuwa jambo moja.

Na ni lazima watu waweze kufikiriwa na kuheshimiwa katika mambo ya ardhi kwa sababu ni kitu ambacho ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu. Kwa hivyo ni muhimu kitu hicho katika Katiba inayokuja kiweze kufikiriwa na kupangiwa pahali pake special na sheria zake ziwe ziko wazi na ziwe hazina utatizi na utetanishi kati ya mtu na mtu. Iwe inawekwa kama sheria ambaye itakuwa niya kuweleka kisawa sawa. Kwa hivyo mimi singependa kuchukuwa wakati mrefu nimesema nilikuwa nasimama kuunga mkono yale yaliosemwa na yule ambaye alisema kwa niaba ya ile kamati ambayo iliunwa na ikaanza kufikiria kwa niaba ya watu wengine kidogom kidogo. Hatukupanga hiyo kuwasemea lakini kamati nayo ilikuwa inafikiri sisi ni kamati basi, tunakazi pia nasi tutoe kule maoni katika hali hayo. Kwa hivyo hiyo ndio sababu nimesema kwamba nimesimama kuchangia maoni hayo. Ama kwa kweli nasema asanteni kwa kuja endeleeni kutoa maoni yenu mkijisikia mko huru. Asanteni sana. (clapping)

**Com. Abubakar Zein:** Ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wetu wa ardhi Mheshimiwa Ngala kwa maoni aliyotoa pamoja na kazi kamati yake iliyofanya hapa halaiki hii kubwa imekuja na mavuno tunayopata kutokana na kazi ya kamati hiyo. Asante sana waziri. Namuomba sasa Fundi wa Baya. Fundi uko karibu. Simba Mwarandu. Karibu Mzee.

**Simba Mwarandu:** Asante sana kwa kunipatia wakati huu nizungumze maneno kidogo tu sio mengi sana. Jina langu mimi naitwa Simba Mwarandu nakaa hapa sehemu ya Bamba. Sina budi kusema asante sana kwa kuja kwa wengi kwa kuchangia Katiba yetu hii inayo kuja kwa kuipeleka kwa raia wa na iangaliwe taabu yao. Serikali inayokuja ijue taabu yetu tulioyo nayo hapa Bamba. Hapa kwetu tuna taabu kubwa sana. Taabu ya kwetu hapa kwanza ni maji. Maji hatuna kabisa Bamba. Utaona wakubwa wakija, siku hiyo utakuta maji kwa mifereji inatiririka moja kwa moja, lakini wakubwa wakishaelekea kisogo kidogo basi maji hukatika ikawa hakuna. Sisi huwa na taabu kubwa sana. Hatuna budi tuzungumze mbele ya wakubwa wetu walio kuja hapa na wajue shida yetu na tuwaeleze kweli kwa haki Katiba mpya inayokuja kwani mmekuja kutaka maoni kwa raia.

Basi taabu yetu kubwa nyingine ya pili hapa Bamba ni machifu na manaibu wao. Kwa haki wanatutatiza sana. Bwana

mwenzangu ametoa maoni yake, nimemsikiza vizuri sana. Amesema kwamba machifu na manaibu wake wachaguliwe kama vile ma councillor. Hiyo ni sawa kabisa. Kwa sababu utaona misaada tunaletewa hapa kwetu inagawanywa kwa upande wa machifu, kisha utaona wataambiwa yule hafai kupata, yule afaa kupata. Leo utakuta wewe unakwenda kusimama msaada unatolewa pilau, ni mahindi, ni unga na utaona watu wako hawapati ati yule ana ng'ombe yule, yule ana mnazi yule. Hiyo hakuna. Serikali haijui hiyo. Inatoa msaada kwa kila mtu. Apate riziki yake, maskini, tajiri pia apate. Leo utakuta unaambiwa una mnazi wewe, hupati wewe. Watu wako wanaondoka na taabu zao wanakwenda kulala na jaa. Basi mimi nikitoa maoni yangu ninasema kwamba, wale ambao wamesema kwamba machifu na manaibu wao wachaguliw, hiyo ni haki kabisa kwa taabu tulionayo hapa.

La pili, tumesema kuhusu maji kwamba pana taabu, nimezungumza hayo, tumekuja kupewa fursa moja hapa la kuchimba mabinsi haya. Kuchimba shimo. Nafikiri kuna wazee wetu wamefika hapo Muyuni pia na wakapita moja kwa moja mpaka wakafika sehemu za sijui Kabateni huko na walijionea kazi inayoendelea. Basi kwa haki kazi ile inaletwa na watu kwa mikono yao kwa kutaka mwenyezi Mungu apate mvua ndio tupate maji yale. Mungu ikiwa hakuleta mvua huwa sisi tuko hali ya taabu. Taabu kabisa. Isitoshe kazi ile inayofanywa vifaa pia hatuna. Tunataka Serikali ijayo ikiwa tutafanya kazi kama ile itupatie vifaa tutafanya wenyewe. Na huo mfereji kabla haujafika, sijui twachimba mabinsi yale kwa kungoja Mungu tunataka Serikali itusaidie kwa mambo ya mfereji kutuletea maji. Huu mfereji wetu huu kwa haki unatutatiza watu wa Bamba. Watu wa Bamba tuna shida kubwa sana. Kwa haki tuna shida. Hatuna budi kuzungumza, yaliopita yashapita lakini Katiba mpya inayoundwa Serikali ituangalie. Tuko tayari sisi wananchi wa Bamba kuchimba mfreji hapa mpaka kufika Longobaya. Tutachimba wenyewe machifu wetu wakae nyuma yetu watuangalie. Na wafanye msaada kutuletea pipe ili tupate maji kutoka na njia hii. Pana njia nyingi za kuja Bamba. Nafikiri hapa tuna njia karibu nne hapa.

Tuna njia ya kutoka Malindi kuja Bamba, tuna njia ya kutoka Kilifi kuja Bamba pia ndio ya kwenda Mombasa. Tuna njia ya Mariakani kuja Bamba, tuna njia ya kutoka Kaloleni kuja Bamba. Basi tunataka angawa ya moja wapo tupate maji. Tupate maji kisha na lami mtutilie jia moja ile maanake tumechukua muda mrefu. Jia ile yetu tuaipita kwa jua. Leo njia ile ikiwa kuna mvua basi sisi huwa hatuna mawasiliano. Hivi sasa mvua ikinyesha hapa nyingi ya kutosha kwa haki nyinyi mtakuja kuchukuliwa na ndege. Hiyo yote ni taabu tulionayo. Hatuna mtu wakumpa taabu yetu ila nyinyi mlio kuja hapa ndio watu wakuwapa shida yetu. Twato shida yetu kwenu nyinyi, mtuangalie hapo kesho na kwa siku sijazo. Yaliyo pita yashapita, tumekosa mengi sisi watu wa Pwani lakini Serikali mpya ijayo, ituangalie. Lakini masubchief na machifu wao wote watachaguliwa na raia kama vile councillors. Sina mengi.

**Com. Abubakar Zein:** Asante Mzee. Mzee ungeenda pale ukaandika register jina. Pale. Sasa kwa heshima zenu zile mlizonipa mimi kuniambia kuna wakati mtanipatia ruhusa ya kubadilisha utaratibu kumpa mtu anayestahili kuzungumza naanataka kutumia nafasi hiyo kumuita mama Jumwa Kazungu Nyiro. Amekaa kwa muda akisubiri. Ningemuomba mama atoe maoni yake. Hata mnaweza kumpa microphone hapo. Esther uje karibu. Mshikie mama.

**Jumwa Kazungu**: *Ndimi Jumwa wa Kazungu Nyiro***.**

**Bi. Esther:** Anaitwa Jumwa Kazungu nyiro.

**Jumwa Kazungu:** *Nina tabu.*

**Bi. Esther:** Ana taabu.

**Jumwa Kazungu:** *Tabu ya kwangu ni ahoho wa kwangu mudzukulu wangu babaye kana kazi.Vikara anahenza kushoma lakini kafuna uwezo.*

**Bi. Esther:** Her main problem is her grandchild. She does not do any work. She wants to go school but there is no money. The father is not employed.

**Jumwa Kazungu:** *Kwa vizho* ***nasema vizho huna shida,***
*be bomu sana***.**

**Bi. Esther:** So she is insisting that there is a problem and a big one.

**Jumwa Kazungu:** *Sina zaidi bule ni vizho tu ndo vidzonifisha ninenenenda na lalamiko ra kwangu na riro ra mudzukulu wangu yunahenza kushoma lakini kakuna nafasi.*

**Bi. Esther:** That's all she has to say. Her main problem is the fact that her grandchild wants to learn but there is no money for that education so that is her major problem. Her son is not employed.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Mwambie mama nimesema asante sana. Halafu uje na register pale umuandikishe. Asante. Turuni kwenye utaratibu wetu ule wakuita majina kwenye orodha. Kitsao Katana? Katana Lugo? Muneni Chengo? Kahambi Charo? Dada nimekuita? Umesikia jina lako dada? Muneni? Karibu Dada.

**MuneniChengo***:* *Kwa dzina rangu naifwa Muneni. Sina mengi yangu ni machache. Kwehu sisi ni shida ya madzi kuku Bamba hunaenza madzi.*

**Com. Abubakar Zein:** Ningewaomba mumpe fursa dada yetu atoe maoni yake kwa makini. Tafadhalini tunyamaze naye apate fursa ya kusema. Kwa hisani zenu. Wana dada wanataka kukusika pale nyuma uweke microphone kwa mdomo wakusikie. Asante..

**Muneni Chengo:** *Ni shida ya madzi kuku Bamba funahenza madzi funahenza mfereji.*

**Esther:** She is saying that their main problem is water. There is no water in this area so they need some water. That's all she has. That is her major problem.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana dada. Nilikuwa nimemuita Kahambi Charo? Katana Charo? Ndugu ndio Katana? Mzee wangu

**Katana Charo:** Asante sana kwa kuja hapa. Jina langu mimi naitwa Katana Charo kutoka hapa Bamba. Sababu ya kuja hapa, naunga mkono wenzangu kusudi ya Katiba ya majimbo. Naunga mkono sana wanaosifu sana majimbo.

Sasa basi tunashida huku Bamba, shida ya maji. Mrefeji uko kweli lakini huu , ni wa wageni. Sio wetu. Tunataka wetu na sisi. Maanake huu ulio hapa uko leo mkirudi huko, maji yatafungwa. Hautufai sisi. Sasa tunataka mfereji wetu tuwe na raha hata sisi.

La tatu na la mwisho, watu hufa mara mbili. Unakufa mgonjwa ama unakufa ghafula. Hii ghafula ina taabu sana. Maanake mtu akijitia kamba hiyo ni shida kubwa. Mnaita polisi wamchukue waende Kilifi. Mwenye pesa atakwenda kutoa mara moja kwake amrudishe kwao. Ukiwa huna pesa inakuwa ni shida kabisa. Mwenye pesa hana shida, asiyekuwa na pesa kama mimi je? Utamzika kule basi. Hapo nataka Katiba hii iangalie sana. Sina zaidi ni hayo tu basi. Asante sana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Charo. Tunakuomba uandike jina lako pale. Datia Karisa? Hayuko ,Masha Gona? Mdzomba Kanda? Kazungu Fondo? Nathaniel Kathengi? Karibu Mzee.

**Nathaniel Kathengi:** Mimi kwa majina naitwa Nathaniel Kathengi natoka area ya bali ambayo ni sehemu ya kutoka Mbaba. Nimekuja hapa kuchangia mambo ambayo ni kama vile ambavyo Katiba ilituruhusu kila mtu aje atoe maoni yake hapa ili kwamba maoni haya ikachukuliwa na Katiba yetu na tuone tutajibiwa namna gani. Kwanza ninapendelea Rais awe na vikao viwili vya miama mitano mitano. Kisha kuendelea mbele ninapendelea uwezo wa Rais upunguzwe. Kwa sababu mjumbe ama mtu alietaka kuchaguliwa kama mjumbe anaweza kuanguka kwa sababu raia hawamtaki. Mtu huyu Rais atarudi amachague kama mteule. Na hali yule mtu hatakikani. Hatujui raia hawamtaki kwa sababu gani. Mtu huyo anarundishwa Bunge. Kwa nini?

Tatu, kuna maneno hapa ambayo inasemwa mara kwa mara. Maneno haya ni habari za kuwapiga akina mama. Maneno haya hata huku Bunge juzi yaleta mgogoro. Je ninauliza ikiwa nimempiga bibi amenikosea aende kwa polisi akapige report nije nichukuliwe nikafungwe. Mtu huyu nikirudi atakuwa mgeni wa nani nyumbani? Nataka shida hii iachwe kabisa. Wale ambao

wanasema mabibi wakikosa wasipigwe labda kwao wao ndio ambao mabibi zao wamechukua funguo ya nyumba. Tunataka Serikali isiingilie kabisa mambo ya bibi na bwana. Mambo kama haya ya achiwe either pande mbili, wazazi wa bibi ama bwana au family ya bwana ama family ya bibi kutatua jambo kama hili. Lakini sasa naona tunataka kuletewa sheria za Kiingereza hapa. (laughter) Je nikimwambia bibi anipikie chakula akisema sitaki pika mwenyewe na hali mimi najua yeye ni mzima. Nimfanye nini? Naomba tume neno kama hili la mabibi kupewa uwezo zaidi uwe ndio uwezo wa bibi kusikizana na bwana sio bibi kukosana na bwana.

Naendelea mbele. Nimesikia wenzangu hapa wakitaja mambo ya masubchief na Chief mwenyewe. Ningeunga mkono sana jambo kama hili la Chifu na naibu wake wachaguliwe wasiandikwe rasmi. Pengine Chifu hafanyi kazi yeyote. Sub-chief hafanyi kazi yeyote. Kazi yao tu ni kuvurugana na wananchi ambao wanataabu. Lakini hawezi kufanya chochote hatafukuzwa Raia hawamtaki na ni yeye mpaka afike makamo ya miaka hamsini. Tutakao tunasumbuka ni sisi raia. Kwa hivyo ninaunga wenzangu waliosema kwamba Sub-chief na Chief wawe wakichaguliwa kila baada ya miaka mitano. Akiwa hatoshi aondolewe. (clapping)

Naendelea mbele na fungu la tano. Kuna kitu moja ambacho sio mimi peke yangu hata wenzangu pia wananchi jambo kama hili lina wasumbua. Ni ya kwamba tuna ma auditor wa Serikali yaani wakaguzi ambao wanakagua pesa za Serikali. Utaona mkaguzi fulani anasema kwamba wizara fulani ilitumia milioni thelathini, haijulikani pesa siko wapi. Wizara fulani ilitumia milioni tisaini, haijulikani pesa ziko wapi. Mpaka ziende pengine wizara tano. Baadaye utasikia kwamba Serikali imenyamaza kimia. Watu hawa wana mu-enjoy huyo auditor ama ni kitu gani kinacho fanyika. Hakuna yeyote atakaye hojiwa kuhusu pesa hizi. Ni kwanini? Tunataka tume ichunguze sana pesa hizi ikiwa mawaziri wako above the law, basi Serikali ituambie.

Naendelea mbele na habari za afisa wa Agriculture. Tunapata taabu sana huku kwetu nani ngetaka tume utufanyie msaada. Maafisa hawa wetu wa Agriculture tunashukuru wanafanya kazi nzuri sana lakini saa nyingine wanatuudhi. Anafanya report kwamba mfugo fulani umeharibu mmea wa mtu fulani. Mzee yule atakuja vizuri sana aje aongee halafu wewe mwenyewe kuharibiwa mmea utapata jawabu ambao ni zero. Utangoja karibu miaka miwili kupata jawabu lolote. Kwa hivyo napendelea kitu kama hiki hawa ma officer wa agriculture wasichukuwe hatua yeyote juu ya mimea, wapitie kwa wazee wa vijiji wafanye kazi hii wakiwa chini ya uangalizi wa wazee wa vijiji ambapo baadaye mzee wa vijiji atapeleka report yake kuna kuhusika ili kwamba haki inatekelezwa kila upande.

Sehemu nyingine ambayo ninataka kugusia ni ya walevi. Tumepata kuona hata huko miji mikubwa mikubwa kama Mombasa, Kisumu, Nairobi, watu wanashikwa tu ovyo ovyo eti ni ulevi. Tukipatikana kwenye nyumba ambayo watu wanakunywa tembo, zote tunasombwa tunakwenda. Pengine mtu amekaa kwa veranda hivi wakati wa jioni lakini nyuma ya hiyo nyumba pengine huuzwa tembo. Wote wanakuja kushikwa na wanapelekwa. Tuna sheria ambazo tunajua katika ulevi. Kuna mlevi ambaye anaitwa drunk and capable na kuna mlevi mwingine anaitwa drunk and disorderly Watu hawa wanaoshikwa na kupelekwa kule huwa amekaguliwa namna gani mpaka anachukuliwa kama mlevi. Naona sheria kama hii ni yakuonea watu

bure tu. Na unaona akikataa huko mbele atapelekwa rumande, hana budi ya kwenda kukubali maskini huyu. Maanake yeye atawekwa rumande kwa mwezi mmoja kisha yeye akubali na hali si mlevi. Nataka hii tume yetu tukufu ichunguze sana kitu hiki cha wananchi kusumbuliwa tu kwa sababu ni mlevi na hali mtu hakushukwa na chochote. Ikiwa amepatikana pahali pa tembo na si mlevi, kwa nini yule mwenye tembo hashitakiwi hawa wakaachwa ambao ni wananchi wanajenga nchi yao. Kesho waende kazini wakajenge nchi kama ni watu ishirini, ni thelathini wote wanasukumwa ndani wote kazi zao zinachelewa. Kuna faida gani ?

**Com Abubakar Zein:** Mzee Kathengi muda wako umekimbia sasa ungekuwa unafupisha.

**Nathaniel Kathengi:** Nipe dakika mbili

**Com Abubakar Zein:** ushapata hizo mbili.

**Nathaniel Kathengi:** Ninaomba ya kwamba hawa wazee wa vijiji wawe wakipewa nafasi ya kuzungumza na watu wa vijiji. Kwa sababu wazee wa vijiji ndio wanaojua taabu kila pahali. Labda chifu amekaribishwa, Sub-chief amekaribishwa lakini sheria nyingi ziachiwe wazee wa vijiji ambao wanaweza kuzitatua bila upendeleo wowote. Yangu yalikuwa ni hayo. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana mzee Kathengi. Julius Shida? Joseph Changawa Karisa? Karibu.

**Joseph Changawa Karisa:** Kwa jina naitwa Joseph Changawa Karisa kutoka Mitangani location. Maoni yangu ya kwanza, uchaguzi wa mlolongo uondolewe mbali kwa sababu huwa unaleta ghasia.

La pili, naomba manaibu wa Chifu na Sub-chifu wapigiwe kura.

Jambo la tatu, wasichana na wavulana wapate elimu sawa hasa. Hakuna mtu kurudi nyuma, wasomeshwe vilivyo.

La nne elimu ya msingi iwe ya bure kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Sina mengi ni hayo. Asanteni sana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee. Jonathan Karisa? Karibu. Jonathan endelea. Ushatoa maandishi? Sawa asante. Jonathan ashatoa maandishi kwa hivyo hataki kuzungumza. Changawa Kadzitu?

**Changawa Kadzitu:** Kwa jina naitwa Changawa Kadzitu. Maoni yangu ambayo nitayatoa ni kuhusu mambo ya wazee wa kijiji. Wazee wa kijiji ni watu wakuheshimika kule vijijini kwao. Lakini sasa kuna kitu ambacho hakiko sawa. Napendelea Serikali yetu iwachungulie sana wale wazee wa kijiji vile ambavyo wanaheshimika kule vijijini kwao pia Serikali iwachukulie hata mifuko yao pia maanake mifuko yao iko tupu. Hayo ni maoni ambayo nimeyatoa.

Pili, kuna elimu ile ya malezi ya watoto wadogo kabisa. Ambayo sasa inawachiliwa wazazi wenyewe ambao sasa huku kwetu ni shida. Tena shida sana ambayo ukienda vijijini utawakuta kweli watoto wako, utawaomba utawapata lakini yule mlezi mwenyewe ikifika mwisho wa mwezi anataka mumlipe nyinyi wazazi wenyewe. Ikifika hapo sasa, wazazi wanashindwa kulipa. Na hiyo pesa ni kidogo lakini wanashindwa. Kwa hivyo pia hapo ningependelea Serikali yetu iweze kutuzaidia wale wenye skuli zile za malezi. Watu kama wale pia waangalie. Pia nafikiri hapo ingekuwa ni sawa. Maoni yangu yalikuwa ni hayo tuu peke yake. Sina zaidi.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Tafadhali andika jina lako kwenye register. Mambo kukumbushana tu. Ikiwa kuna mtu ana maandishi yake anataka kutoka bila kuzungumza unaruhusia kufanya hivyo pia. Unakuja hapo unatoa maandishi yako una andika jina kwenye register halafu unaendelea mbele. Najaribu kwenda mbio mbio kwa sababu najua kuna watu ambao wana kaa sehemu bali sana na hapa. Na singetaka waende nyumbani kukiwa giza. Joseph Katana? Jina lako ni Joseph, Sio? Karibu. Halafu Stephen Kairaga akifuatiwa na Agnes Mweli.

**Stephen Kairaga:** Nimetoa maoni yangu tayari kwa karatasi.

**Com. Abubakar Zein:** Asante. Joseph ashatoa maoni yake kwa maandishi. Stephene Kairaga? Stephen anakuja? Agnes Paul Mweli? Jacob Njogu Ngozo. Ngolo? Asante Ngolo.

**Jacob Ngolo:** Mimi kwa jina naitwa Jacob Njogu Ngolo kutoka Ndigiria Sub-location. Maoni yangu ni kuhusu Chifu wachaguliwe na manaibu wao kwa sababu ni maendeleo ya hapa duniani.

**Com. Abubakar Zein:** Ukishatuambia pendekezo lako ni machifu wachaguliwe sisi tumeelewa. Endelea mbele.

**JacobNgolo:** La pili ni kuhusu ardhi. Kila mmoja apatiwe hati za kumiliki ardhi kwa sababu tunaona watu wanapokonywa ardhi ovyo ovyo. Kwa hivyo ardhi tukipatiwa zile hati za kumiliki tutakuwa tunapata makao vizuri.

Tatu ni kuhusu makaa na ngonge pendekezo langu ni kwamba wengine hawana kazi zozote hata wana pendekeza kukuata makaa na ngonge kuuza hapa Bamba ama pahali pengine wapate chakula. Kwa hivyo napendekeza wale ambao wanaishi kule karibu na msituni hawana chakula kingine ila hayo makaa na ngonge. Kwa hivyo pendekezo langu ni hayo makaa na ngonge ipitishwe ili sehemu zingine wapate chakula.

Nne, ni kuhusu hawa watakao chaguliwa, kila mmoja ajue kazi yake. Kwa sababu tunajua ya kwamba hata kama wale ambao wamechaguliwa utakuta umechaguliwa kiti fulani anawacha kile kiti chake, anaketi cha mwenzake. Kama wewe Diwani unawacha kiti chako na unakaa na kiti cha mwenzako. Kile kiti chako ki wazi na watu wanateseka. Kwa hivyo hiyo sehemu

nayo nataka iingie huko kwa uchaguzi.

La mwisho kabisa ni kuhusu kanisa. Mimi ni mmoja wapo wa watu wa kanisa . Makanisa mengine yanavuruga wenginei. Kuna makanisa mengine yanasema ya kwamba kuna kanisa fulani halina nguvu, kanisa fulani halina imani yoyote. Kwa hivyo wanavuruga wale waumini wengine. Kwa hivyo wana kanisa wale ambao wanapuuzi makanisa mengine basi hao waangaliw pia. Hilo ndilo la mwisho na Mungu awabariki sana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Jacob. Andika jina lako pale kwenye register tafadhali Jacob. Charo Mayo Mdzomba? Charo ni wewe? Karibu. Haraka haraka tafadhali.

**Interjection:** (inaudible)

**Com. Abubakar Zein:** Nafanya hivyo Mzee wangu. Nikiita jina na hayuko naenda kwa jina linalofuatia. Nitatumia ile fursa yangu ya kuwapa wazee fursa nikupe na wewe moja.

**Charo Mayo:** Kwa jina naitwa Charo Mayo Mdzomba. Mimi ninayo maoni kuhusu Katiba ambayo inaundwa. Kwa hakika katika sehemu zetu hizi kuna mambo fulani ambayo tunaona si mazuri hayaridhishi hata wananchi katika sehemu zetu.

**Com. Abubakar Zein:** Nitajie mambo hayo.

**Charo Mayo:** Kama uongozi. Viongozi wetu kwa mara nyingine wanapochaguliwa baada ya kile kipindi chao hakijafikia mwisho, wananchi mara nyingine huona kwamba hawafanyi ile kazi ambayo walichaguliwa nayo. Sasa badala yake kuwe na uchaguzi fulani kabla wakati haujafika ili waweze kuondolewa wawekwe wengine ambao hatimaye wataendelea vizuri. Kwa sababu hiyo tunaona kama wananchi hasa wale viongozi ambao tumewachaguwa hawakufanya lolote hasa. Si wote lakini baadhi yao hawakufanya lolote ambalo wananchi wanaridhiki nalo. Kwa hivyo inasikitisha kwamba mtu unachukua muda unakaa kwa sababu unasema basi baada ya pengine kipindi cha miaka mitano ama miaka kumi, yeye ata toka. Mimi naona ama napendekeza kwamba baada ya kipindi hicho pengine miaka mitano ama miaka kumi kama ambayo imewekwa, ikiwa kiongozi aliyechaguliwa haendelezi vizuri, kuwe na uchaguzi mwingine kabla hicho kipindi hakijaisha ili aweze kuondolewa na kuwekwa mwingine ambaye ataendeleza vizuri.

Jambo lingine katika sehemu zetu hizi ni bara bara. Bara bara huku zinahitaji kuwekwa lami kwa sababu kwa nyakati hizi inakuwa ni vigumu sana hasa kusafiri wakati wa mvua, kwenda sehemu moja ama nyingine inakuwa gharama. Mvua ikinyesha bara bara huwa zinabomoka, mtu huwezi kusafiri kuna sehemu nyingine ambazo zimewekwa lami.

**Com. Abubakar Zein:** Ndugu yangu, tushahamu kwamba unataka bara bara ziwekwe lami. Jambo lingine.

**Charo Mayo:** Jambo lingine ni elimu. Mimi nachangia sana hasa hii mambo ya elimu kuanzia darasa la kwanza elimu ya msingi iwe ya bure.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa Mzee wangu

**Charo Mayo:** Na katika shule za upili, hizi gharama zake si kwamba ziwe bure lakini gharama zake ziweze kupunguzwa ili kwa wale ambayo hawajiwezi vizuri wawe nao wataweza kusomesha vijana wao wamalize masomo yao sawa sawa.

Jambo lingine ni usalama. Tunahitaji hasa kuwe na hospitali, zijengwe baada ya kilometre mbili hivi, kwa sababu tunaweza kushikwa na ugonjwa hatari.

**Com. Abubakar Zein:** Tushafahamu tuende mbele.

**Charo Mayo:** Jambo lingine ni usalama na haki. Kule kunyanyaswa ni viongozi walio juu, huko nako Katiba inapaswa iangalie na ikiwezekana, kusiwe na mambo ya unyanyasaji.

Pia kuna mambo ya maji. Maji ni muhimu sana hasa kwa binadamu. Binadamu bila maji inakuwa ni vigumu sana kuishi. Kwa hivyo pia katika Katiba hii ambayo inaundwa iwe itafikiria sana katika sehemu hii zetu. Kila baada ya kilimetre mbili pia kuwe kuna kituo cha maji. Iwe benesi au mfereji. Kuwe na kituo cha maji ili wakaazi ama wananchi wajipatie maji katika sehemu za karibu bila kusafiri kwenda mbali. Naona yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Charo. Andika jina pale kwenye register. Ibrahim Juma Kitsao

**Juma Ebrahim Kitsao:** Kwa jina naitwa Ebrahim Juma Kizao natoka Mtangani, kijiji cha Ngongeni. Nina maoni kidogo hapa kuhusu Katiba ile tunayochangia leo. Nataka nizungumze, hivi nipe nafasi kidogo. Zile sheria ambazo ziko sasa ni za maonevu kabisa. Kwa sababu ziliundwa kwa ajili ya Mkenya asiweze kuendelea. Lakini sasa kama tunarekebisha, turekebishe tuone kweli Mkenya anaendelea. Nikichukulia mfano kama hivi, kama Serikali ama Katiba imepitisha kwamba ulevi i uendelee bia zitauzwa na marungi kutoka bar yaje. Naona kuna haja pia mnazi uendelee kuuzwa , kwa sababu pia tunajipatia riziki watu wa Pwani.

Tukijaribu kidogo kuangalia hali ya utawala tunapata kwamba polisi wanauonevu fulani. Kama wazee waliokuwa walivyo sema kwamba mtu anaweza shikwa hapa ukifika kule kortini, polisi anakueka ndani na anatoka. Halafu akaandikisha kwamba huyo nimempata akikojoa bara barani. Na huyo ataenda wewe utakabaki na judge na hukuako siku hiyo na ushtakiwe kwamba umekojoa bara barani na hali si haki. Na kama ni haki, ni kweli amekojoa bara barani ovyo ovya uma viko wapi ?

Ndio mtu asiweze kukojoa bara barani naye ametoka sehemu za bali kwenda mji mwingine. Kwa hivyo sheria kama hizi za udictator, ziweze kurekebishwa ili Mkenya akweze kufanya kazi na uhuru. Tusiwe kama mtu wa duka. Nasikia sasa leseni za duka ni shilingi elfu tano kila mwaka. Mtu labda ana kiosk chake barabarani, siku moja anaweza kukusanya shilingi ishirini tu na hapo hapo atalisha watoto wake na kusomesha watoto wake. Atapata wapi elfu tano kwa mwaka. Hiyo haiwezekani. Sasa kuweko na mpango maalum watu waweze kuendelea.

**Com. Abubakar Zein:** Pendekezo lako nini kuhusu jambo hilo? Unasema taabu ni gharama kubwa ya leseni. Wewe unapendekeza nini?

**Juma Ebrahim Kitsao:** Ninapenda kuwekwe kiwango ambacho kitakuwa ni kichache sana. Kwa mfano kama shilingi mia kwa mwaka. Pia naunga mkono hawa wenzangu waliosema kwamba ma-subchief na ma-chief wachaguliwe. Ni vizuri kabisa. Kwa sababu watachagua mtu mwenye heshima, mtu ambaye anaheshimu mali ya mtu na aweze kuchaguliwa sawa na watu vile wanavyotaka.

Jambo lingine ningependa sisi kama watu wa Pwani, huu utawala wa majimbo nauunga mkono. Ijapo sio kufukuza mwingine. Lakini mbona sisi tunadharauliwa kama Waafrika. Hata tukifika Mombasa, unapata kwamba Mwarabu anakuita ng'ombe eti kwa sababu ni mtu mweusi ama ni Mugiriama mlji panya unyika huo. Hiyo ni sheria za u-dictator. Yule kama mgeni amekuja na sasa amenunua mahali kwa sababu ana pesa. Tume ya sasa ikachunguze sasa huyu mtu hapa mahari amepa pata vipi ndio Mkenya naye mwenyewe aweze kutengewa mahali ambapo anaweza akafanyia kazi. Kama vibanda vilivunjwa vyote. Karibu watu wote wa Bamba wanategemea vibanda. Hawa wote mnawaona hapa hawajui watafanya nini kwa sababu hawa hapa, kama wawili,watatu lazima mmojawapo ana kibanda na familia yake inategemea kibanda. Sasa sheria kama hizo zilivunjwa ili Mkenya asiendelee lakini sasa tujaribu tuone kwamba tunaendelea. Asante sana.

**Com. Abubakar Zein:** Kitsao rudi nyuma. Andika jina hapo. Patric Kenga Gona? Yuko? Karisa Kitsao Maitha? Katana Mwaringa? Ndio wewe? Karibu bwana.

**Katana Mwaringa:** Kwa jina naitwa Katana Mwaringa Charo. Marekebisho ya Katiba ijayo ningeomba hasa kwa upande wa elimu wa skuli hizi za msingi, kuhusu waalimu. Waalimu ndio wnazorotesha watoto wetu (inaudible).

**Com.Abubakar Zein:** Pendekezo lako nini?

**Katana Mwaringa:** (inaudible)

**Com. Abubakar Zein:** Sawa tumesikia pendekezo. La pili?

**Katana Mwaringa:** Langu ni hilo moja tu.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa sawa. Asante. Andika jina hapo. Francis O Oreki? Hayuko? Julius Charo? Masha Chembe?

**Masha Chembe:** Mimi kwa jina Masha Chembe kutoka Mitangani location. Katika kuchangia Katiba hii ijayo kwa wakati huu mimi ningeonelea ikuwako mamlakani, ilikuwa inaumiza wananchi si sehemu zote,lakini ni sehemu fulani fulani. Hasa upande wa wanyama wa pori wamepewa uwezo mkubwa na Serikali kushinda mwananchi. Basi mimi ninaonelea Serikali ijayo akiwa mnyama yuko kwa shamba la Serikali, awe wa Serikali . Akiingia kwa shamba la mwenyewe, awe wa mwenyewe. Asiwe mtu ameu kadigidigi kwa shamba lake kinamuharibia mimea anashikwa na anapigwa ya kwamba ameua mnyama wa pori na ameua mali yake kwa sababu alikuwa kwa shamba lake. Kwa hivyo Serikali ijayo mamlaka ya wanyama wa pori irudi chini. Basi hayo ni maoni yangu.

Kuongozea pia kipindi cha Rais. Rais aweze kuchaguliwa hata kama ni miaka mia moja sababu akiwa anapendwa na wananchi, achaguliwe. Asiwe miaka kumi pengine bado anaendelea vizuri kwa wananchi na sheria haimuruhusu. Kwa hivyo ningeonelea achaguliwe hata akiwa ni miaka mia moja. Wananchi wenyewe wakiona hafai wata mwangusha. Hayo ni maoni yangu.

Pia niki rundi upande wa elimu, elimu ya shule ya msingi iwe ya bure kwa sababu pia tunaona kwamba watoto wengi wako nyumbani kwa sababu ya wazazi kushindwa.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa mzee tumeelewa unataka elimu ya bure ya msingi.

**Masha Chembe:** kwa hivyo hayo machache ndiyo yalikuwa yangu.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee wangu. Andika jina pale mzee. Kombe Mdzomba? Benard Babu? Mzee taja jina lako halafu uanze kutoa maoni tafadhali.

**Kombe Mdzomba:** Mimi jina langu naitwa Kombe Mdzomba, mzaliwa wa sehemu moja huko chini kunaitwa Bandani lakini kijijini kwenyewe ni Karimani. Wale watu watatu ambao waliuwawa mmoja alikuwa ni mkubwa wangu kwa hivyo na machache si mengi sana. Ameacha watoto na hakuna usaidizi wowote. Wengine wamesoma na wengine wameacha kwa sababu hawana pesa za kuendelea na shule. Yule aliyesema watoto wasome bure namshukuru sana.

Pili mambo ya mabenesi nataka yaendelee. Kuna sehemu moja, sehemu ya Mkong'ani. Nilikuwa nikikaa Karimani. Kuna sehemu moja hapa inaitwa Ndugu ni jembe hapa kwa hivyo tunachimba mabenesi. Mambo ya benesi, hata hakuna haja ya kusema. Kila mahala kumeletwa vyombo kama benesi ya Muyuni, kumeletwa benesi nyingi sana. Tena na mahindi yataletwa,

kwa hivyo hayai mambo ya mabenesi, yanaendelea.

Kitu cha tatu ni yule aliyesema tuchimbe mfreji wenyewe kutoka Lango Baya. Alisema vizuri hata mimi nataka hivyo. Ningezumnguza sana lakini hali yangu si nzuri. Juma pili ya tarehe saba mwezi wa nne, nyumba yangu iliunguwa. Hata sasa roho yangu saa ingine huenda mbio. Sina mengi ni hayo.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Kombe. Naomba Mungu atakupa faraja katika moyo wako. Benard Babu? Benard Babu uko? Waitwa je ndugu yangu ?

**Benard Babu:** Nimewasilisha karatasi tayari.

**Com. Abubakar Zein:** Ni Babu? Asante karibu Bwana. Joseph Menza? Joseph yuko? Peninah Kilindi? Karibu dada.

**Peninah Kilindi:** Kwa majina naitwa Peninah Kilindi. Mimi nataka kuzungumzia mambo ya elimu. Elimu ya primary iwe ya bure. Bara bara pia, bara bara zote ziweze kuwekwa murram vizuri ili tukienda katika safari zetu kuelekea Kilifi tuwe hatutapata matatizo. Ni hayo tu.

**Com. Abubakar Zein:** Asante Peninah. Andikisha jina hapo. Kahindi Nyiro. Nadhani Kahindi alikuwa ashatoa. Haujatoa bando? Mzee wangu ndio Kahindi?

**Kahindi Nyiro:** Kwa jina naitwa Kahindi Nyiro na nimzaliwa wa hapa Bamba, Kaziani Kathangani. Mimi maoni yangu si mengi. Ni mawili tu. Maoni yangu ya Katiba hii ya Kenya inayokuja. Wajibu wangu ni kuhusu wanafunzi wanaosoma mashuleni ambao huenda wakifika yale madarasa ambayo yanatakikana na Serikali, mtoto huenda mbele. Wazazi wengine tunashindwa kuwasukuma mbele watoto wale. Kwa hivyo Katiba hii inayokuja iangalie mahali hapo. Hapo ndio maneno yangu yamefikia mwisho na asanteni sana.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana mzee. Sasa ningeomba kutumia ile fursa mlisema akiwa kuna mzee amevumilia sana mpaka amechoka, tumpe fursa mzee Joseph Menza.

**Joseph Menza:** Mimi napenda kutoa shukrani kwa wale wageni wote ambao wamekuja hapa. Mimi naitwa Joseph Menza kutoka Kalongoni. Ninashukuru mheshimwa Katana Ngala kutuletea mgeni wetu wa heshima ambaye ndiye mwenye kuunda hii Katiba na wageni wengine pia. Langu ni kutoa shukrani na maoni yangu kueleza pia kwa sababu hapa ni Bamba. Bamba tuna shida nyingi, ya kwanza ni maji. Nafikiri Mheshimwa wewe ni mtu wa hapa na ni mzaliwa wa hapa na mambo ya hapa unayajua vile yanavyoenda kuanzia mwanzo mpaka mwisho unayajua. Mtu haishi bila maji na maji ya hapa ina vipengere ambavyo havistahili. Ni kwamba vipengere hivi utapata hivi, wakati ukija wewe maji yanapatikana na ukiondoka wewe maji

yanapotea. Hilo ni la kwanza.

Pili, tuna anzia wazee wa vijiji na ma-subchief ambao hawapatani kabisa na raia. Nikisema hivyo ni kwamba tumekuwa na historia ya kienyeji. Upigaji wa ngoma za kiasili kwa sababu tunatafuta mvua. Kulikuwa na wengine ambao ni ma-subchief. Walikuwa hawastahili kusikia ngoma inapigwa. Na mambo haya yamesababishwa na hii afis ya DO. Sisi tunatafuta mvua na yeye anasema ngoma isipigwe.

**Com. Abubakar Zein:** Pendekezo lako nini Mzee wangu ?

**Joseph Menza:** Sisi tunataka watu kama hawa ambao hawashirikiani na watu sawa hawa ni kutengwa. Kutengwa ni kufutwa. Kwa sababu Ki-giriama *kinaamba ukikala unakeresi mudzi lazima usikizane na atu. Ukikala kusikizana na atu karakara unda tengwa.* Kuanzia leo watu wanatoka Chira Mgadamani huko wanaenda kuteka maji Kajiri . Isitoshe, hali ya mvua ama hali ya kutegemea mvua imepita. Huu ni mwezi wa nne tuko mwezi wa tano sasa. Hakuna mtu aliyepanda na aliyepanda vimemekufa. Kile ambacho kita tuokoa sisi hatuna, tumebaki tuna njaa. Tunaohitaji hivi sasa ni msaada. Na huu msaada tunahitaji ni wa chakula kwa sababu hatuna chakula. Dakika hii ukisema hivyo utaambiwa wewe ni mrongo. Habari ya mahindi ya msaada hayagawanywi tena saa hii, isipokuwa benesi peke yake na hiyo benesi nayo niya kuchaguwa.

Nikiongoezea hata mimi nasema hivi, ikiwa wewe utakuwa unaongoza wananchi na hupatani na wananchi ama hutaki kuwatendea wananchi, wewe ni mtu wa kazi gani?

**Com. Abubakar Zein:** Pendekezo lako nini mzee wangu ?

**Joseph Menza:** Mimi nasema mtu kama huyu si mtu wa kueka. Katika Katiba hii tuliyonayo, hatutaki mtu kama huyo. Nakuomba kamaWaziri wetu ulioko hapa na wageni, Katiba inasema tupatane, tuheshimiane, katiba inasema ni vitendo. Kwa hivyo nimeomba kama ikiwezekana ikiwa utaturuhusu kuhusu sauti ambayo imetoka ya kwamba Sub-chief, ama Chief ama mzee wa kijiji ikiwa inawezekana watu hawa wachaguliwe. Lakini si kuenda kindani ndani. Sisi tumechoka na mambo hayo. Asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa mzee wangu. Tumesikia. Asante Mzee. Andikisha jina hapo mzee. Tuendelee mbio mbio, haraka haraka. Tuisikizane tafadhali. Ningependa kumualifu mheshimiwa Waziri kwamba walikuako watoto wa nursery hapa asubuhi wakaja wakatoa maoni yao kwa mashairi. Alfonse Kenga? Kenga Katana Mwaringa?Kature Kitso Yeri upo? Karibu.

**Kature Kitsao:** Kwa jina Kature Kitsao Yeri. Maoni yangu si mengi ni machache tu. La kwanza ni kuhusu mambo ya nafasi za kazi. La pili, ardhi zetu tupewe hati za kumiliki mashamba. Lingine ni mambo hayo hayo ya maji tunayo yazungumzia hapa. Ni hayo machache tu asante.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana. Tafadhali andika register hapo. Kafadzi Kadenge? Karibu mzee.

**Kafadzi Kadenge:** Mimi kwa jina naitwa Kafadzi Kadenge, mzaliwa wa Bamba. Nimetoka kijiji cha Pungu. Maoni yangu napendelea majimbokwa sababu yatatutengenezea mambo ambayo tunahitaji watu wa Pwani ,kama bara bara tutiliwe lami. Mambo ya maji huku kwetu ndio tunataka. Elimu ya msingi iwe ya bure,maanake hivi sasa hapa nilipo nina watoto wanne wananishinda kupeleka shule.

**Com. Abubakar Zein:** Abdalah Kadzitu? Caroline Sidi. Caroline njoo tafadhali.

**Caroline Sidi:** Kwa jina naitwa Caroline Sidi kutoka hapa Bamba. Mimi kwa kuchangia Katiba ningesema elimu ya msingi iwe ya bure kwa watoto wote, wavulana na wasichana. Upande wa elimu ya secondary pia Katiba iingilie ,kwa sababu kuna shule zingine ziko na malipo ya juu hata sisi wazazi tukijimudu hatuwezi kuwapeleka watoto wetu. Sasa hiyo Katiba iweke kiwango cha kuwa mtoto akimaliza darasa la nane kama ataenda secondary iwe tunajua tutatoa senti hizo na mtoto anasoma badala ya kila shule kuwa na taratibu zake.

Jambo la pili, ni upande wa urithi. Watoto wote wavulana na wasichana wote ni sawa. Kwa hivyo, kama wewe umezaa watoto wasichana na umezaa watoto wavulana, kila mtoto awe na haki ya kurithi mali ya baba yake. Kama ni shamba, kama ni mali Katiba iingilie mambo kama hayo. Ni hayo machache tu.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bi Caroline. Tafadhali andika register pale. Benard Dalu? Ameshatoa mswaada nimeambiwa. Isaac Chamoton ? Joseph Kalama? Antony Gona? Julius T. Kahindi? Na mtu wa mwisho kabisa katika orodha yetu ambayo tunayo sasa ni Samuel Kenga Rua. Wewe ndiye Samuel? Karibu Bwana.

**Samuel Kenga:** Majina yangu ni Samuel Kenga Rua. Mimi nilikuwa nimeandika kwa hivyo naona sina haja ya kurudia rudia kwa sababu tayari nilikuwa nimeandika na nitapeana kule kwa yule karani.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Kenga. Nimepatiwa listi ya mwisho. Charo Wanje Kapilo? Mwalimu Shikari Karibu mwalimu.

**Mwalimu Shikari:** Mimi naitwa Mwalimu Shikari. Ninatoka Ndingiria. Kule Ndingiria mimi ni chairman. Maoni yangu, ya kwanza ni maji. Maji yana shida kwetu zaidi sana. Hakuna maji tunataka mfreji kama inawezekana tusaidike. Hayo ni maoni ya kwanza.

Shida nyingine tena, wananchi wanalalamika zaidi. Kwa hivyo, tuwe vile tulivyokuwa tangu zamani. Zamani tulikuwa tukifanya

nini ? Mtu yuko na shamba lake amenunua ardhi yake tena watoto wake na bibi zake wanakaa mahali kwa ardhi yao. Na sasa tunataka tuwe vile vile. Jambo la pili kwetu kumekuwa na shida sana, majangili wanatutesa. Tena mimi nilitoa ardhi yangu tukaweka kituo cha polisi. Tuliweka kituo cha polisi kwenye ardhi yangu. Na Mheshimiwa Katana Ngala amefanya mambo mazuri sana. Ametusaidia sana sisi wananchi. Ameweka tani moja ya cement kwa kituo cha polisi. Hayo ni maoni yangu mimi na napendekeza sana. Sasa tena tunaona raha zaidi wale majangili hawafiki tena. Hayo ni maoni. Na tunafurahi kwa kusaidiwa.

Maoni ya nne ni ya shule. Wazazi wanalalamika kwamba pesa zimezidi kabisa.

**Com. Abubakar Zein:** Pendekezo lako nini Mzee ?

**Mwalimu Shikari:** Pendekezo lako mimi naomba zile pesa zipunguzwe kama inawezekana. Wazazi wamelalamika sana. Kama inawezekana zipunguzwe. Tukae vile vile kwenye mashamba vizuri kama zamani. Wale majangili wamekuja kutupokonya sisi. Wamesema ati tumenunua huku kote na hiyo ardhi ilinunuliwa na wazee wetu.. Hatutaki tena kabisa mambo hayo.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa Mzee.

**Mwalimu Shikari:** Maoni ya tano ni bara bara. Tunataka bara bara ifike Ndigiria. Ikitoka Ndingiria iende mpaka Mlachakwe ndio tutakuwa tuko sawa. Sasa hayo ndiyo maoni yangu.

**Mwalimu Shikari:** Ya sita, ni kwamba tupate nini? Hospitali. Kule Ndingiria kuwe na hospitali. Mtoto kama ni mgojwa tunampeleka Bamaba, aje kupata madawa. Yule mgojwa kama ugonjwa umemzidia hawezi kufika, anafariki hapo katikati. Tena tunasitikika sana. Kama inawezekana tupate hospitali kule Ndingiria. Asante.

**Com. Abubakar Zein;** Asante sana Mzee Mwalimu. Andikisha jina pale. Karisa
Katoi?

**Karisa Katoi:** Mimi kwa jina naitwa Karisa Katoi Charo kutoka location ya Ndingiria. Pendekezo langu ni kwamba, ningetaka hawa machifu na masub-chief wachaguliwe kama vile tulivyo chagua Wabunge wetu na mawaziri wetu. Ningetaka wakewe kiwango miaka ikifika, tuchague. Sio ati mtu andikwe afike mpaka miaka yake iishe. Sisi huwa tunateseka sana kwa sababu watu wengi huwa wanatudhulumu sana.

La pili, ningetaka itilie mkazo tupate maji kama vile wenzetu wanavyopata kule sehemu za Pwani.

Tatu, ningetaka hii mambo ya makaa, mnazi pia hulalalishwe. Kwa sababu pia mnazi huu haukuchanganywa na mambo ingine sio ati tunaweza kusema eti ile ni pombe ya halamu. Kwa sababu watu wengi huwa wanapata ridhiki kulingana na huyo manzi. Kwa hivyo tunataka hiyo muangalie.

Jambo lingine ningetaka piani bara bara ziangaliwe. Sina mengi zaidi ni hayo tuu asanteni.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Bwana Karisa. Fondo Lugo? Karibu. You want to give in your written memorandum? Okey please just sign in the register. Safari Charo?

**Safari Charo:** Kwa jina mimi naitwa Safari Charo mzaliwa wa hapa Bamba. Nimekuja kutoa mchango wangu kuhusu Katiba. Ama kwa kweli Katiba inayokuja inayofaa Serikali inayokuja, inafaa iwe Serikali ya majimbo. Nikisema hivi ninavuta picha ya marehemu Ngala kwamba yeye alitaka majimba lakini alikuwa na maana yake kusema hivyo. Haikuwa majimbo tu. Alikuwa kuna kitu anakiona huko mbele. Sasa kile kitu sisi, hatukukiona na sasa hivi kinaonekana wazi wazi. Kwamba Katiba ilioko sasa yatunyanyasa. Imekuwa ni msemo kwamba ikifika wakati fulani kila Mkenya atakuwa amepata kitu fulani. Ni urongo. Sasa tunaona Katiba hii ya majimbo, italeta maendeleo karibu sana na sisi. Haswa kwa upande wa kazi. Asilimia kubwa wakati wa majimbo, asilimia kubwa ya ujira iende kwa wenyenji. Si Katiba ya kusukumana. Si majimbo ya wewe nenda kwenu, la bora wewe ni Mkenya unaruhusiwa kufanya biashara hapa, unaruhusiwa kufanya chochote hapa, lakini basi ujue majimbo yanachukua nafasi kubwa ya wakaazi wa hapa. Sio wewe una kuwa allocated sehemu kubwa na wewe ni mgeni.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa tushakufahamu.

**Safari Charo:** Naweza nikaendelea kidogo?

**Com. Abubakar Zein:** Umezungumza mambo ya majimbo. Una hatua ya pili? Jambo lingine?

**Safari Charo:** Sina lingine zaidi maanake mimi lengo langu ilikuwa ni kurekebisha Katiba tu.

**Com. Abubakar Zein:** Yaani wataka majimbo. Sawa Mzee wangu. Tafadhali andika register. Hata shida ya maji ni mambo ya Katiba. Anderson Mwambogo? Charo Kukoto? Stephene Fundo Maitha? Karisa Mramba?

**Karisa Mramba:** Jina langu naitwa Karisa Mramba natoka Ndugu ni jembe Bamba. Napendekeza kuhusu maji. Kwetu hakuna maji. Lingine ni watoto washule pesa zimezidi kila siku unatoa pesa na wengine hawana, wanalalamika sana. Mimi sina mengi. Yangu ni hayo tuu.

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mzee Mramba. Tafadhali andikisha jina lako pale. Katoi Katana? Hapo ndio tmefikia mwisho wa orodha ya majina tuliopewa. Kuna Mkenya yeyote alioko hapa ambaye anataka kutoa maoni na hajapata fursa ya kutoa maoni? Sawa. Nitakupa fursa Mzee na nitampa fursa ya mwisho mama. Kuna mwingine Mkenya yeyote ambaye alikuwa kutoa maoni na hajafikiwa. Hawa wawili ndio watatufungia baraza letu la leo. Mzee wangu ungetaja jina halafu ndio uendelee.

**Joseph Karisa Gunzi:** Mimi kwa jina naitwa Joseph Karisa Gunzi. Nashukuru sana kwa tume leo kututembelea leo hapa Bamba, ninayo machache. Ni vizuri kukumbushana kwamba ile Katiba ambayo tulinyakuwa uhuru nayo sasa imekuwa haitusaidii vilivyo. Mwelekeo wa Katiba hii ni kwamba sasa tunataka kuungana kabisa, makabila arubaini na mawili yawe sawa sawa.

Nataka kuzungumza kuhusu uraia wa Kenya. Raia wa Kenya, ni yule ambaye amezaliwa kwa jadi amekaa hapa Kenya tangu tupate uhuru, raia halisi wa hapa Kenya. Kunao raia wengine ambao tungetaka waambiwe ni raia wa Kenya, ni wale ambao wanazaliwa na baba ambaye ni Mkenya. Tuseme mama ameolewa nchi nyingine ametoka tuseme Uganda kwa mfano, amekuja Kenya hapa Bwanake ni Mkenya, akizaa wale watoto wawe automaticaly Wakenya. Hayo ni maoni yangu. Lakini wale ambao wanataka kuwa raiai wa nchi mbili mbili, mimi siwaungi mkono. Maana mguu wake leo uko Kenya, ukiona matata kesho uko Uganda. Sasa huyu mtu aweza kuleta balaa. Kwa hivyo mimi maoni yangu mimi naona tuwe na Mkenya Mkenya. Atakuwa akizungumza na sisi tunazungumza Kikenya vizuri, isipokuwa mna mtu yuko hapa leo, kesho mnasikia yuko United States. Mimi hapo naona si vizuri. Mkenya halisi ni yule aliye na kitambuisho kwa sababu kile kitambulisho kinatoka kwa Chifu ajulikana kule alikozaliwa, akitemba nacho ni Mkenya kamili. Nafikiri kitambulisho cha Kenya kinaweza kumfanya mtu kujulikana kama ni Mkenya.

Nikiendelea nitagusia ulinzi na usalama wa nchi. M imi naona uwe juu ya Rais na Bunge liwe na jukumu la kutoa ushauri. Vyama vya kisiasa vigharimiwe na Serikali. Hii nafikiri itasaidia sana kwa hongo zinazofanyika wakati wa uchaguzi. Hapo hapo tunaweza kujua mtu fulani ametoa zaidi kiwango ambacho amefunja wananchi.

Nimeonelea tena nizungumze habari ya Serikali ya majimbo. Serikali hii mimi nataka hiyo afisi ya DC iwe itaondolewa na pawe na Governor ambaye anachaguliwa na raia. Lakini DC, DO, Chifu. Subchief tuwe nao. Mzee wa kijiji, awepo na tena alipwe. Hawa wazee wakiwa hivyo, tutakuwa tukitoka hapo kwa mzee wa kijiji tunaenda kwa DC mara moja tunaenda kwa Governor ambaye tunamchagua zote sisi hapa mkoani kama ni Pwani ,halafu matatizo yetu anaweza kuyasuluhisha. Hapo yale ambayo ni ya kuenda Central kama mambo ya ulinzi na fedha kule ,zitakuwa zikitoka kule zinakuja kwa District level.

Toka tupate uhuru tunashukuru wengi wamefanikiwa sana. Lakini tukiangalia sisi watu wa Pwani au Bamba kwa jumla tarafa ya Waziri wetu, tunasikitikika kwamba watoto wetu ambao wanasoma wakitafuta zile nafasi za kazi, wanazikosa. Kuna njia

nyingi sana ambazo zinafanyika ambazo unakuta mtoto amepita lakini hawezi kuenda. Unakimbia kwa waziri lakini tunampatia kazi nyingi. Je kwa nini basi Katiba yetu isiwe na utaratibu ya kuchukuwa hawa watu wa kutoka kila tarafa ya bunge wawe wakileta majina au number ya kwamba wapelekwe vijana fulani kwa training wale ambao wamehitimu na wana marks za kutosha. Badala ya kwamba tunaambiwa medical training centre unatakikana ulipwe mia tano na form ijazwe na ipelekwe kule na mia tano, non refundable fee. Sasa angalia ni Wakenya wangapi wanapeleka hizo pesa huko. Hasa tarafa ya Bamba kama itapeleka watajaza hizo form watoto mia tano na shilingi mia tano halafu hakuna hata mmoja atakaye chukuliwa. Hapo tunazungumza ni kama kuna corruption au nini? Maana hazitarundishwa zile pesa. Kwa hivyo tungependa tufaidike katika hii Katiba kwamba Mbunge wetu apate kazi rahisi apewe number ya watu kila college ili akituletea huku sisi tunajua baada ya miaka fulani tutapata daktari hapa, baada ya miaka fulani tutapata daktari wa vetinary hapa, hivyo hivyo, na sisi tutainuka kama Wakenya wengine.

Tungependa naye DC awe ni mtu wa hapa hapa kwetu. Tukiwa tunazungumza mambo ya majimbo maana atatuelewa zaidi. Pesa zikitolewa kutoka Central Government, basi zije direct kwa DC halafu tutaziona hapa watu wa Bamba. Ninashukuru sana kuona kitabu chenu hiki ambacho kiko na cover ya red. Red inaokana kwamba njia yetu kwamba ni hatari hatari. Ningependa mwangalie kwamba kila tarafa katika Katiba hii, ipewe uwezo wa kuwa na bara bara ya lami. Asante kwa hayo machache.

**Com. Abubakar Zein:** Bibi aliyekuwa pale. Huu ndiye atakuwa mzungumzaji wetu wa mwisho. Tafadhali andika jina lako pale mzee.

**Rachel Kadzo:** Kwa majina naitwa Rachel Kadzo. Nilikuwa tu na maoni mawili ama moja ijapo mengi ni yale ambayo yamesunguzwa. Nilikuwa nasema ya kwamba haya mambo huku kwetu yamekuwa ni kama mambo ya kiasili,lakini ninataka yakewe sheria kwa sababu yasipo wekewa sheria basi yataendelea hivyo hivyo na yatachangia umaskini.

Na lingine ni lile ambalo limezungumzwa hapa na yule mwenzangu ilikuwa anasema juu ya kuchukuwa urithi wa baba. Kama baba amekufa tunanyimwa haki zetu. Pengine hata mama alizaa wanawake watupu lakini ile mali inakuwa ni vigumu mpaka sasa yule baba wa ufa akiwa ana mtoto wa kiume, yule ndiye atarithi. Nafikiria tumenyimwa haki zetu kwa sababu hata mtoto wa kike pia anatakikana apewe haki yake. Mimi sina mengi ni hayo tu.

**Com. Abukar Zein:** Waitwa nani Mzee.

**Katoi Katana:** Katoi Katana.

**Com. Abubakar Zein:** Nimekuita sana na nikasema huyu ndiyo mtu wa mwisho. Niko karibu kufunga lakini siwezi kumzuia Mkenya kutoa maoni. Yapange yatoke haraka haraka.

**Katoi Katana:** Naitwa Katoi Katanantoka sehemu za Mitangani. Kwa hivyo pendekezo langu mimi, tumekuwa na waalimu wengi sana huko nyuma nyuma ambao walikuwa hawafanyi vizuri kabisa kusema kweli. Kumezungumzw mengi sana hapa lakini sasa hiyo yote ni ya ukweli. Mwalimu inafaa aheshimiwe na wanafunzi sio kuogopewa kama nyoka akiingia darasani. Tuhakikishe ya kwamba walimu wasiingie virasini wakiwa ni walevi. Maanake watu wengine ni wagonwa. Kuna fimbo ya mwalimu ya kisawa sawa ya kuchapa mtoto mpaka akirudi nyumbani awe ni mgonjwa. Hiyo hatutaki.

La pili, sehemu yetu ni mbali na hapa Bamba. Tunataka Serikali ijayo ijenge hospitali upande wetu maanake tunapata shida sana ugonjwa hauna time, wakati wowote waweza kukushika. Sasa unamkimbiza, pengine huna baiskeli.

**Com. Abubakar Zein:** Sawa mzee wangu unataka hospitali ijengwe Bamba.

**Katoi Katana:** Nataka hospitali ijengwe Mitangani.

La tatu ni shida ya maji imezidi mno hapa. Hiyo sijui tufanya nini lakini nataka Serikali ijayo itilie maanani sana hiyo kitu.

La nne, kumezungumzwa kitu hapa na mwenzangu, na mimi hiyo ilikuwa ni pendekezo langu. Kuna askari ambao wanaonea watu. Hiyo kitu ni kama kunyanyasana. Mtu anashikwa akiwa hana hatia yeyote anasukumwa anaenda akifika kule, anatishwa na maneno mpaka anatoa pesa ndio anaachiliwa. Hiyo kitu mimi ziungi mkono. Hata wenzangu hawaungi mkono. Kwa hivyo sina mengi yangu ni hayo.

**Com. Abubakar Zein:** Tafadhali andika register pale. Ningependa kumuomba Professor Ghai aseme mawili matatu kabla sijafunga kikao hiki lasmi. Professor.

**Prof. Yash Pal Ghai:** Thank you very much. We have not finished our hearing. I want to thank you all on behalf of the commission for coming here today and for your valuable contribution. As Commissioner Zein said, all the views that you have expressed will be considered very seriously by the commission. They have been recorded on audio and on video we shall make a written record of all the views you have given us and they will be analysed by the commission in Nairobi. We want to assure you that all the views that you have expressed will be considered very seriously by the commission. The success of this review process depends on the participation of the people of the country and I am very encouraged this afternoon to see that so many of you have come. I know some of you have come long distances and I want to thank you very much indeed for your contribution. Thank you very much.

**Com. Abubakar Zein:** Pengine ningetafsiri kidogo alioyasema Professor kwa Kiingereza. Professor Ghai amewashukuru sana kwa dhati, kwa nyinyi kuweza kufika hapa ili kutoa maoni yenu ili kurekebisha Katiba yetu. Angependa kutoa hakikisho lake kwamba maoni yenu yatatiliwa maanani nayatathaminiwa na yatatumika kujenga Katiba mpya. Pia amewashukuru sana

kwa sababu anajua baadhi ya wengi wetu tumetoka sehemu za mbali kwa njia ngumu ili tukifika hapa kufanya kazi hii muhimu. Pia alikuwa akitaka kuwakubusha kwamba kazi hii inafanyika Kenya mzima na kwamba tutaendelea kukusanya maoni yenu ili kurekebisha Katiba.

Ningependa tu mwisho kuwakumbusha alioyasema Professor Ghai hapo mwanzo, kwamba leo isiwe siku ya mwisho. Ikiwa umeenda nyumbani ukakumbuka mambo ambayo ungetaka kutuelezea lakini tukawa tushaondoka. Una haki kwa sababu tumetoa hivi vijitabu vidogo hivi kuwa mwongozo una haki kuandika maoni yako chini kwa mswaada na ukamletea mshirikishi wetu Daniel Mwaringa au mkatutumia moja kwa moja kwa sanduku la posta tulioliandika hapo katika hicho kijikitabu, zitufikie. Natungependa kuwashukuru sana kwa nyinyi kujitokeza kwa wingi manma hii.

Wengine ambao ningependa kutoa shukrani maalum kwao ni wana kamati wakiongozwa na waziri wetu Mheshimiwa Ngala kwa kazi kubwa waliofanya sehemu hii tunajua kuna matatizo mengi. Tumesikia matatizo ya watu waliozungumzia kuhusu hali ya mawasiliano, kuhusu maji, kuhusu huduma za afya na mambo mengine. Kwamba kazi hii wameifanya katika hali ngumu na kuja kwenu hapa ni ushahid ya hamu ya Wakenya kushiriki katika kujiamulia mambo yao wenyewe na kujenga jamii mpya itakayo ongozwa na Katiba ambayo kila Mkenya atakuwa na ari na majivuno ya kusema mimi nilichangia kujenga Katiba hiyo. Sijui kwamba Bwana Waziri una jambo la kusema.

**Hon. Katana Ngala:** Nataka nichukue nafasi hii tena kumshukuru Professor Ghai, kumshukuru Commissioner Zein na wale wote waliokuja wakiandamana na team ya Professor Ghai. Nataka niseme kwamba nyinyi wananchi leo mmefanya kitendo cha maana mmetupa sifa watu wa sehemu hii, kwa jinsi mlivyo kuja kwa wingi. Na kama alivyosema Commissioner pamoja na shida ambazo ziko za nyumbani na mambo mengine tumesikia mwito na mkaheshimu mwito mlioambiwa na viongozi wenu kwamb siku ya leo kutakuwa na wageni watakao fika na mkaona ni vyema muweze kuja hapa kuitikia mwito huo.

Nataka nichukue fursa hii niwashukuru sana nyote maana mmefanya kitendo cha heshima. Mmejionyesha kwa mwenye kiti huyu na kama alivyosema Commissioner Zein kwamba mmeonyesha kwamba mlikuwa na hamu ya kuchukua mambo haya kuwa yenu. Tulipokuwa tukizungumza tulikuwa tunasema ya kwamba nyinyi wenyewe mtakuwa watu wa kusema hamtakuwa watu wa kusikiza. Na mmeona ya kwamba Chairman na watu wake wote walikuwa ni watu wa kusikiliza kwa makini. Hawakutaka kusumbua mtu, kumtia mtu uoga wamempa kila mtu nafasi ya kusema na kwa hivyo mimi nasema ni vizuri kwamba mmepeta nafasi huu kuja hapa. Yale ambayo mmesema nataka kusema yote yana maana. Yote mlioyasema. Maana ni mambo ambayo yakghusa wewe nafsi yako na unaona ni vizuri kwamba yaweze kutoka yaweze kusikizwa. Kwa hivyo usiondoke hapa ukifiri kwamba mchango wako ulikuwa mchango wa vivu. Nina hakika hawa wataalamu watajua namna ya kupanga haya maneno na bila shaka watakua na kufurahia kwamba sisi pia tumekuwa na maneno muhimu, tumekuwa watulivu na tumekuwa watu wenye heshima na tumewakaribisha na wamejionea wenyewe. Kwa hivyo nataka nitoe tena shukrani kwenu kwa kuja hapa nataka nitoe shukrani kwa Professor Ghai na team yake yote kwa kuja hapa. Ni heshima kubwa maana Kenya nzima ikiwa Professor Ghai kati ya zile sehemu alizochagua pia Bamba ni moja wapo basi naona pia tumewekwa katika

hali ya juu katika siku ya leo.

Nataka ikiwa nitaruhusiwa na Professor Ghai niseme ya kwamba tunashukuru sana kwa uhusiano ambao tumekuwa nao na coordinator wetu. Coordinator wetu amekuwa ni mtu ambaye ni rahisi kusikizana. Mipango ya kazi ameifanya kuwa laini kwa sababu hakuna mvutano. Kwa hivyo tunataka kumshukuru Daniel Mwalinga pia kwa kujaribu sana kuhakikisha kwamba kazi za mambo haya ya merekebisho ya Katiba katika wilaya yetu na katika sehemu ninayowakilisha inaendelea bila kuwa na vikwazo vyovyote. Kwa hivyo tunamshukuru yeye na watu wake wote kwa kazi waliofanya.

Mpango huu hapo mbeleni na hata sasa ninafikri kumekuwa na misemo mingi muundo wa hii marekebisho ya Katiba. Tulikuwa na misemo ya aina mbali mbali, lazima iwe people driven na mambo kama hayo. Na nina hakika katika nyinyi kuja hapa, mmetimiza msemo wa kwamba hii Katiba marekebisho yake yawe people driven. Kwa hivyo nyinyi mnaisukuma hii Katiba kwa sababu ya kuja na pia mmekuja mkahusishwa katika usemi, participation yenu pia imekuwa ni ya muhimu. Kwa hivyo mimi nina jisikia kwamba nimeinuka sana kupitia nyinyi watu wetu kwa kuja hapa nakuja kusema kila mtu aliosema, aliyesikiza amesikisa kwa makini natumeonyesha kabisa kwamba tuna nidhamu nzuri na mimi nataka tuendelee hivyo wakati wowote ikiwa kuna mipango yoyote ya mazungumza katika siku sijazo. Tuwe watu ambao tunaweza kuonyesha kwamba tumekuwa na kukomaa katika mambo yetu. Mipango kama hii ya watu kuweza kuchuka mamlaka mikononi mwao na kuzungumzia mienendo na maisha yao ya baadaye ni mipango ambayo siku hizi inaanza kuonekana dhahiri katika mipango ya kiserikali na hata katika mambo ya Katiba. Kwa hivyo ni kitu cha maana kwamba unapewa nafasi ya kwamba unaweza ukajikatia maoni mwenyewe, unaweza ukachangia nafsi ya maisha yako ya siku sijazo bila kuwa na uoga. Na mimi nashukuru sana vile ambavyo mmefanya hivyo leo. Kwa hivyo tunawatakia la heri. Tunataraji ya kwamba Katiba ya Serikali ijayo itakuwa ni Katiba ambayo itakuwa na michango yetu dani yake. Ikiwa ni mtoto na kama ni mtoto ana miguu na kicha na tumbo na nini pia sisi tutakuwa na kitu dani yake katika maumbile ya mtoto yule. Kwa hivyo nataka niwashukuru sana katika hali hii. Na haya yote naona yanawezekana kwa sababu tuko katika hali ya kwamba nchi hii tuna amani. Na tukuwa tunajenga Katiba mpya ni lazima tukumbuke kwamba kitu muhimu katika wakati wowote ule tukiwa tunafanya mambo yote ya nchi hii msingi na kiungo kimoja muhimu ni amani. Kwa hivyo natuzidi kuizungumzia amani wakati wowote tunapopata nafasi natuweze kuiwekea manani amani ya nchi hii maana ndio inayoweze kufanya sisi kuketi hapa na sisi zote tumezungumzia serikali ya namna fulani. Lakini hatukuzungumzia Serikali ya majeshi. Hakuna aliyezungumzia hilo. Kila mmoja amezungumza tunataka Serikali ya aina fulani, ya majimbo, ya muungano, namna hii lakini hakuna aliye kosa njia akasema kwamba anataka Serikali ya majeshi. Ni kwa sababu anajua kitu ambacho ni muhimu katika uongozi wa Serikali, ni Serikali ambayo imechaguliwa na raia wenyewe kwa kupigiwa kura. Hiyo ndio serikali ambayo inaweze kudumisha uongozi wa siasa katika nchi. Kwa hivyo amani ni kitu muhimu na kila wakati tukipata nafasi kama hivi tunatakikana tuweze kuwaunga nakuweka kiungo cha amani kati ya shughuli zetu. Kwa hivyo hivi tunavyo wachana tukienda katika shughuli zingine muhimu na tujaribu kuwa wananchi ambao tutadumisha amani kila pembe ya tarafa hii ili tuangalia Katiba hii itakapo tengezeka itakuja kutufaa na nini tukiwa chini ya mazingira ya amani. Kwa hivyo kwangu mimi nikusema asanteni na kumshukuru tena Professor Ghai na Commissioner Zein na wengine wote ambao mmefika na nyinyi raia kwa kuja kutuinua jinsi mlivyo tuinua. Nina uhakika Professor Ghai hatasema hapa lakini akienda kando atasema

kuna kitu nimeona kidogo chenye kunipa moyo katika hali hii. Kwa hivyo nendeni nyumbani salama. Tutaonana wakati mwingine na kama walivyosema kama unakitu umesahau tafadhali kitoe ili kisibaki na wewe kwa sabababu wakati bado uko. Kwa hayo nataka kusema asanteni sana.

Ningetaka basi kwa sababu sisi ni raia wa hapa na huyu ni mgeni na wanaenda zao na pengine hatutawaona tena mpaka baada ya miaka mingapi sijui, maana huyu ni Commissioner, lakini tunamukaribisha wakati mwingine arudi. Pengine atarudi kwa mambo mengine. Ikiwa ni hivyo na kwa kuonyesha kwamba tumefurahia kutembelewa na yeye. Kuwacha sehemu zingine zote za Kenya nakuja hapa, hatuna kitu tunachoweza kumpa. Hatuna zawadi tutakayompa lakini makofi pia ni zawadi. Ama sivyo? Basi ningetaka nyinyi mtayarishe mikono yenu ili tumpigie professor Ghai na Commissioner Zein na team yake yote aliyokuja nayo kuonyesha kwamba pia tumeridhika kwamba wamekuja hapa. Basi tayarisheni mikono yenu ili tuwapigie makofi tukiwa tunawagana nao wakienda safari ya huko Mombasa na huko kwingine watakako endelea kufanya. Kwa hivyo makofi yetu twajua. Sii mkutano wa siasa huu. Siwezi kusema nyoosha kidole kimoja juu. Siwezi lakini makofi tutapiga. (Clapping)

**Com. Abubakar Zein:** Asante sana Mheshimiwa Waziri. Ninamuomba Daniel aombe mtu atuongoze kwa maombi halafu ndio tuondoke.

**Daniel:** Nitamuomba Mama Ruth Mramba tafadhali tufungie kwa maombi

**Prayer:** Baba katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo tunakuomba na kushukuru kwa vile ambavyo umechukua mkutano huu tangu mwanzo mpaka sasa tumefika mwisho. Tunashukurani kwa vile ambavyo umetuweka kwa katika hali ya utulivu tunakuuliza Baba wakati tukapo achana, wote ambao watakao safiri katika vyombo tofauti tofauti wapeleke salama katika mahali wanapo kwenda ili ile kazi tuliofanya hapa isiwe ni yetu wenyewe tu, Baba uyabariki yazidi kuwa mapya. Haya yote Baba tunakuuliza katika jina la Mwokozi wetu Yesu Kristo. Amen.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**